# UCHANGANUZI WA LUGHA YA AMANI NA MARIDHIANO KATIKA MUZIKI NCHINI KENYA (2008-2012)

**NA**

**MATARA PHILIP NDEMO**

TASNIFU ILIYOWASILISHWA ILI KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA MOI

KITIVO CHA FANI NA SAYANSI ZA KIJAMII

IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA

**OKTOBA, 2014**

# IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote kingine. Hairuhusiwi kuiga au kunakili sehemu yoyote ya tasnifu hii bila idhini yangu na/au ya Chuo Kikuu cha Moi.

**Matara Philip Ndemo** **……...………..** **………………**

SASS/PGK/02/11 Sahihi Tarehe

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa ridhaa yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Moi

**Prof. Nathan O. Ogechi** **………………..** **…………….**

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika Sahihi Tarehe

Chuo Kikuu cha Moi

**Dkt. Robert W. Oduori** **……………….** **…………….**

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika Sahihi Tarehe

Chuo Kikuu cha Moi

**CHUO KIKUU CHA MOI, ELDORET, KENYA**

# TABARUKU

*Naitabaruku kazi hii kwa familia yangu.*

*Wazazi wangu: Baba; Marehemu Geoffrey Matara, Mama; Rebecca kerubo Matara kwa hisani na malezi bora.*

*Kwa mke wangu mpendwa; Peris Moraa.*

*Umekuwa mhimili muhimu maishani mwangu na wajua kwa nini….*

*Kwa watoto wangu: Geoffrey Matara Junior na Becky Kerubo kama hamasa maishani ya kutaka mjiendeleze na mfanikiwe kitaaluma*

## ABSTRACT

This research sets out to analyse the language of peace and reconciliation in Kenyan music (2008-2012). The research aimed at analyzing the special use of language and the manner in which peace and reconciliation themes are presented in the sampled music. The study analyzed the special choice of lexemes, clauses and sentences by considering the paradigmatic and the syntagmatic relationships of these elements. It begins by outlining the background details of this research and the functions of music in the political, economic and social spheres of the society. In addition, the study explores the special use of language in presenting the message of peace and reconciliation and the manner in which themes relating to peace and reconciliation have been structured and presented in the messages of the sampled music. The study objectives were, to establish the music used to promote peace and reconciliation in Kenya between 2008 and 2012, to expound the unique diction in relation of musicians with regard to lexical, clause and sentences choices and finally to analyze the message expressed through music intended to promote peace and reconciliation in Kenya (2008-2012). Halliday's theory on functions of language coupled with Fairclough's thoughts on critical discourse analysis lay the theoretical base for this research. The various functions of music in presenting the theme of peace and reconciliation have been looked at by relating them with the functions of language. Interpretation on the language choices has been analyzed based on the thoughts on critical discourse analysis as a social process. Purposive sampling was used to determine the data for this study. Twenty secular Kenyan songs sang between 2008 and 2012 were analyzed. Open transcription was used to generate the data for analysis. A qualitative analysis was employed in analyzing the data. The research found that there is special choice and use of language in relaying the message of peace and reconciliation. It is also evident that these choices are dictated by the context in which the music is created and sang together with the intended function of the artiste. In addition, it has become evident through this research that language performs various functions in the society. These includes preaching peace and reconciliation, warning the society against trends that threaten peace and reconciliation besides advising the society on ways through which long lasting peace can be achieved among other functions. This research is important in understanding ways in which language can be used positively to enhance development in the society. The research recommends that the functions of music be recognized and expanded in dealing with important issues facing the society.

# IKISIRI

Utafiti huu ni uchanganuzi wa lugha ya amani na maridhiano katika muziki nchini Kenya (2008-2012). Ulilenga kuchanganua matumizi ya kipekee ya lugha na jinsi maudhui ya amani na maridhiano yanavyowasilishwa katika muziki tuliouteua. Utafiti huu ulichanganua upekee katika uteuzi wa maneno, vishazi na sentensi kwa kuzingatia uhusiano wa vipengele hivi kiwima na kimlalo. Unatanguliza kwa kueleza misingi ya utafiti na uamilifu wa muziki kisiasa, kiuchumi na kijamii. Aidha, umeangazia matumizi ya kipekee ya lugha katika uwasilishaji wa ujumbe wa amani na maridhiano jinsi maudhui ya amani na maridhiano yameumbwa na kuwasilishwa ndani ya jumbe anuwai kwenye muziki ulioteuliwa. Malengo ya utafiti huu yalikuwa kubainisha muziki uliotumiwa kuendeleza amani na maridhiano nchini Kenya kati ya mwaka wa 2008 na 2012, kupambanua matumizi ya kipekee ya lugha katika ubunaji wa wanamuziki kwa kuzingatia maneno, vishazi na sentensi na kufafanua ujumbe katika muziki wa amani na maridhiano katika muziki nchini Kenya (2008-2012). Nadharia ya majukumu ya lugha ya Halliday pamoja na mawazo ya Fairclough kuhusu uchanganuzi makinifu wa diskosi yalitoa msingi wa kinadharia kwa utafiti huu. Uamilifu anuwai wa muziki katika kuwasilisha maudhui ya amani na maridhiano umeangaziwa kwa kuuhusisha na majukumu ya lugha. Ufasiri wa uteuzi wa lugha umechanganuliwa kwa kuzingatia mawazo kuhusu uchanganuzi makinifu wa diskosi kama mchakato wa kijamii. Data ya utafiti huu iliteuliwa kimakusudi. Nyimbo ishirini zisizo za kidini zilizoimbwa nchini Kenya baina ya mwaka wa 2008 na 2012 zilichunguzwa. Mbinu ya unukuzi wazi ilitumiwa ili kuzalisha data iliyochanganuliwa. Nimetumia maelezo ya kinathari katika kuichanganua data. Utafiti huu ulibainisha kwamba kuna uteuzi wa kipekee wa lugha katika uwasilishaji wa ujumbe wa amani na maridhiano. Aidha, imebainika kuwa uteuzi huu aghalabu unatawaliwa na muktadha ambamo muziki unatungwa na kuchezwa pamoja na uamilifu unaolengwa kutimizwa na wasanii mbalimbali. Isitoshe, kupitia kwa utafiti huu imebainika kwamba lugha huweza kutekeleza majukumu mbalimbali katika jamii. Majukumu haya ni kama vile: kuhimiza amani na maridhiano, kuionya jamii dhidi ya mienendo inayotishia amani na maridhiano pamoja na kutoa wasia wa jinsi ya kuhakikisha kwamba jamii inapata amani ya kudumu miongoni mwa majukumu mengine. Utafiti huu ni mchango katika kuelewa jinsi lugha inaweza kutumika kwa namna chanya ili kuleta maendeleo katika jamii. Utafiti unapendekeza kutambuliwa na kupanuliwa kwa uamilifu wa muziki katika kuzungumzia masuala muhimu yanayoikabili jamii.

**YALIYOMO**

IKIRARI ii
TABARUKU iii
ABSTRACT iv
IKISIRI v
YALIYOMO vi
SHUKURANI x
ORODHA YA VIFUPISHO xii
SURA YA KWANZA 1
MISINGI YA UTAFITI 1
1.0 Utangulizi 1
1.1 Usuli wa Utafiti 2
1.2 SWALA LA UTAFITI 11
1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI 12
1.4 NADHARIA TETE 12
1.5 UMUHIMU WA UTAFITI 13
1.6 UPEO WA UTAFITI 14
1.7 MISINGI YA KINADHARIA 14

1.8 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA 18

1.9 MBINU ZA UTAFITI 25

1.9.1 Uteuzi wa Sampuli 25

1.9.2 Ukusanyaji wa data 26

1.9.3 Vifaa vya Kukusanyia Data na unukuzi wa Data 26

1.9.4 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data 27

SURA YA PILI 28

UAMILIFU WA MUZIKI KATIKA JAMII 28

2.0 Utangulizi 28

2.1 Muziki nchini Kenya 28

2.1.1 Muhtasari wa hali ya muziki nchini Kenya 28

2.1.2 Mtindo mpya wa muziki nchini Kenya 30

2.3 Uamilifu wa muziki kiuchumi 32

2.3.1 Muziki na mapato ya nchi 33

2.3.2 Muziki na Kilimo 34

2.3.3 Muziki na Ajira 37

2.4 Nyimbo katika siasa 40

2.4.1 Athari chanya za muziki katika siasa 41

2.4.2 Athari hasi za muziki katika siasa 45

2.5 Uamilifu wa muziki kijamii 46

2.5.1 Athari chanya za muziki kijamii 47

2.5.2 Athari hasi za muziki kijamii 55

2.6 Hitimisho 55

SURA YA TATU 57

LUGHA KATIKA MUZIKI WA AMANI NA MARIDHIANO 57

3.0 Utangulizi 57

3.1 Matini za uchanganuzi 57

3.2 Muktadha 59

3.2.1 Muktadha wa kiisimu 59

3.2.2 Muktadha wa hali 60

3.2.3 Muktadha wa kijamii 62

3.3 Upekee katika uteuzi wa lugha 63

3.3.1 Upekee wa kimsamiati 64

3.3.2 Upekee wa Vishazi. 73

3.3.3 Upekee wa sentensi 84

3.4 Hitimisho 92

SURA YA NNE 94

UJUMBE WA AMANI NA MARIDHIANO KATIKA MUZIKI: 2008 -2012 94

4.0 Utangulizi 94

4.1 Wakenya kuacha kupigana 95

4.2 Ukabila 111

4.3 Uchochezi 118

4.4 Wakenya waishi kwa upendo 121

4.5 Wakenya wasiharibu mali 126

4.6 Ufisadi 128

4.7 Wakenya Wasameheane 131

4.8 Uchaguzi wa Amani 133

4.9 Ujenzi wa Taifa 141

4.10 Hitimisho 144

SURA YA TANO 145

MUHTASARI WA MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 145

5.0 Utangulizi 145

5.1 Muhtasari wa Utafiti 145

5.2 Matokeo ya Utafiti 147

5.3 Mahitimisho 149

5.4 Mapendekezo ya Utafiti 150

MAREJELEO 151

VIAMBATISHO 158

KIBALI CHA UTAFITI 161

## MICHORO NA MAJEDWALI

Jedwali: 1Wasanii wa muziki wa amani na maridhiano 2008-2012 55

Mchoro : 1 Mchakato wa usimbaji na usimbuaji wa ujumbe 62

## SHUKURANI

Sina budi kutoa shukurani zangu za dhati kwa watu ambao nisingeshirikiana nao kazi hii haingefikia kiwango hiki. Ni mapenzi yangu niwataje wote kwa majina lakini haitawezekana.

Hata hivyo ni sharti niwataje baadhi yao. Kwanza ni wasimamizi wangu prof. Nathan Ogechi na Dkt. Robert Oduori ambao walijitolea mhanga katika kuniongoza na kunishauri wakati wa utafiti wangu. Ninasema shukurani kwenu.

Siwezi kuwasahau wahadhiri wangu wote katika idara ya Kiswahili wakiwemo Dkt. Mark Kandagor, Mwalimu Munyua, Mwalimu Mukuria na wengineo kwa kuniongoza vyema masomoni. Mchango wenu katika kunikuza kitaaluma umenifaa sana.

Sitawasahau wazamili wenzangu katika idara ya Kiswahili: Vincent Magugu, Kennedy Opindi na Arinaitwe Annensia. Namshukuru hasa Vincent Magugu kwa kuchukua muda wake na kuipitia kazi hii. Tusingeshikana pamoja na kufaana nisingefaulu.

Ninamshukuru Sorobi Moturi Erastus wa Royal Media na mpwa wangu Benson Bogonko Omwenga kwa kunifaa wakati wa kukusanya data za utafiti wangu nikiwa jijini Nairobi.

Shukurani maalum zimwendee mke wangu Peris Moraa kwa auni aliyonipa na kwa kustahimili upweke nilipokuwa masomoni.

## ORODHA YA VIFUPISHO

KANU –Kenya African National Union

KCB - Kenya Copyright Board

KHRC – Kenya Human Rights Commission

KNCHR – Kenya National Commission on Human Rights

KRCS – Kenya Red Cross Society

MCSK - Music Copright Society of Kenya

MOYAS – Ministry of Youth Affairs

NCIC – National Cohesion and Intergration Commission

PRSK – Performing Rights Society of Kenya

RTLM – Radiotelesion libre des milles collines

RoK – Republic of Kenya

Taz - Tazama

TY – Tafsiri Yetu

UKIMWI – Ukosefu wa Kinga Mwilini

URNG – Guatemalan National Revolutionary Unit

WIPO – World Intellectual Property organisation

# SURA YA KWANZA

# MISINGI YA UTAFITI

## 1.0 Utangulizi

Sura hii imeeleza misingi iliyotumika katika utafiti uliofanywa pamoja na uchanganuzi wa data. Sura yenyewe imegawika katika sehemu tisa ambapo sehemu ya kwanza inaelezea misingi ya utafiti huu kwa kutoa taarifa za kiusuli kuhusiana na mada ya utafiti. Katika sehemu hii, nimetalii suala la amani na maridhianio katika muziki nchini Kenya kwa muhtasari na kuweza kubainisha nafasi ya muziki katika kuchangia hali ya amani na maridhiano nchini. Aidha, hali ya amani ilivyo katika sehemu tofauti za ulimwengu sawa na hali hiyo ilivyokuwa nchini Kenya tangu nchi ijinyakulie uhuru wake hadi leo imeangaziwa.

Sehemu ya pili inaelezea suala la utafiti huu. Tasnifu hii imeonyesha jinsi lugha katika muziki inavyoweza kutumiwa katika kuhimiza wananchi kuishi kwa amani na maridhiano. Amani na maridhiano zimetajwa kama nguzo muhimu katika kustawi na kuendelea kwa nchi yoyote ile.

Katika sehemu ya tatu na ile ya nne, malengo ya utafiti huu na nadharia tete zilizoongoza utafiti huu mtawalia yamejadiliwa kabla ya kubainisha upeo wa utafiti huu katika sehemu ya tano. Katika kubainisha upeo, vyanzo vya data zilizotumika katika utafiti huu pamoja na cha uchambuzi wake zimeshughulikiwa.

Sehemu hii imefuatiwa na kipengele kinachoeleza ni kwa nini utafiti huu unapata umuhimu katika kuhimiza amani na maridhiano miongoni mwa wananchi kama ilivyobainishwa kwenye malengo ya utafiti huu. Katika sehemu ya saba, tasnifu hii imejadili mihimili ya kinadharia pamoja na mawazo ya kitaaluma yaliyoongoza utafiti huu. Sehemu ya nane imejikita katika kueleza baadhi ya maoni ya wataalamu waliofanya utafiti katika uwanja huu nayo sehemu ya tisa inajadili mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu.

**1.1 Usuli wa Utafiti**

Utafiti huu unalenga kuchanganua uteuzi wa lugha ya amani na maridhiano katika muziki nchini Kenya. Uchanganuzi huu unahusu muziki usio wa kidini, ulioimbwa baada ya mwaka wa 2007. Hii ilifuatia machafuko yaliyotokea baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka huo. Muziki ulioshughulikiwa unawalenga wanajamii mbalimbali wakiwemo vijana. Vijana wameelezewa kuwa watu wa makamo wenye nguvu wa kati ya umri wa miaka kumi na mitano hadi miaka thelatini na mitano (Longhorn 2009, MOYAS-Kenya 2012). Kundi hili hulengwa zaidi kutokana na sababu kuwa ndilo kundi linalokumbwa na changamoto ainati zikiwemo zile za ukosefu wa ajira, matumizi ya madawa ya kulevya, hatari ya kuambukizwa magonjwa yasiyo na tiba kama vile UKIMWI, na nyingine nyingi (Ogechi 2006; Kandagor, Kiprono & Simotwo 2012). Katika mazingira hayo, huwa ni rahisi kwa vijana hao kujiingiza katika vitendo vilivyo kinyume cha sheria za nchi kiasi cha kuvuruga hali ya amani na utulivu uliopo, kama ilivyoshuhudiwa baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2007.

Tafiti zilizofanywa kuhusu lugha ya amani na maridhiano zimedhihirisha namna lugha ilivyo muhimu katika kustawisha maendeleo ya nchi yoyote ile. Alexander (2003), akijikita katika nchi za Australia, Kanada, Ubelgiji na Uswidi anaichukulia lugha ya amani na maridhiano kuwa sehemu ya zile mali asili muhimu zinazoiwezesha nchi kuendelea. Umuhimu wa lugha ya aina hii unazingatiwa sana katika nchi hizi kiasi kwamba kamati maalum za kuhimiza matumizi yake miongoni mwa wananchi zimebuniwa na serikali za nchi husika. Aidha, kamati hizo zimetwikwa jukumu la kuhifadhi na kutunza lugha ya amani na maridhiano, kando na kusimamia kuajiriwa kwa wataalamu kama vile watafsiri, wafasiri, wajuzi wa istilahi na wanaleksikografia kwa ajili ya utunzi huo.

Kukosekana kwa amani na maridhiano katika nchi yoyote ile kunaweza kuzua hali ya msukosuko. Katika hali hiyo, nchi haiwezi kuwa na maendeleo yoyote (Chumbow, 1987). Hali hii ilipata kushuhudiwa katika nchi ya Guatemala kati ya mwaka wa 1981 na 1983 kulipozuka mapigano ya kikabila. Kulingana na Oettler (2006), mauaji ya halaiki ya watu nchini Guatemala yalilenga hasa wale wa jamii ya Maya na yalichochewa na tofauti za kikabila, kilugha, kijamii, kiuchumi na kidini (hasa kutokana na mwamko wa milenia ya kipentekoste). Katika kutekeleza haya maangamizi, makundi manne ya waasi yalijiunga pamoja na kuunda *Guatemalan National Revolutionary Unit (URNG).* Maovu yaliyotekelezwa na kundi hili ni pamoja na kuua viongozi wa kijamii, kuwabaka wanawake, kuteketeza mashamba na kuharibu sehemu takatifu za ibada. Eneo kama la Ixil lilishuhudia mauaji ya kati ya asilimia 70 na 90 ya wakazi wake. Zaidi ya watu 200,000 waliangamia kando na wengine wengi kutoweka wasijulikane walikoenda.

Mwishowe, hali ya amani na maridhiano ilipatikana nchini Guatemala katika mwaka wa 1996 kutokana na juhudi zilizoongozwa na tume ya ukweli na maridhiano ambayo ilihimiza matumizi ya lugha yasiyozua kutoelewana miongoni mwa wanajamii (Oettler, 2006).

Hali sawa na hii pia ilitokea nchini Rwanda mnamo mwaka wa 1994 ambapo licha ya kuzungumzwa lugha moja ya Kinyarwanda, lugha hiyo ilitumiwa vibaya kwa kuchochea mapigano ya kikabila kati ya jamii mbili kuu, Hutu na Tutsi (Ogechi & Bosire-Ogechi, 2011). Uchochezi huo ulifanywa kupitia kituo cha kurushia matangazo ya redio nchini Rwanda, *Radiotelevision libre des milles collines (RTLM*) (Thompson, 2007). Hatimaye, mapigano hayo yalisababisha mauaji ya watu 800,000 na uharibifu mkubwa wa mali katika kipindi cha siku mia moja pekee (Magnarella, 2001).

Ekuam (2006), akitoa mchango wake kuhusu migogoro tofauti inayoharibu hali ya amani barani Afrika, anasema kuwa migogoro hii inapotokea, wale wanaoathiriwa zaidi huwa ni wale wasio na uwezo mkubwa katika jamii hasa wazee, wanawake na watoto. Wanawake huathirika sana kwa kupigwa, kubakwa, na kukosa chakula na huduma muhimu za kutunza afya yao. Katika hali hii, huwa hawana hiari ila kutoa miili yao kama njia ya kuepuka dhuluma za kinyama kutoka kwa wanaume. Matokeo huwa ni kuambukizwa magonjwa ya zinaa kama vile UKIMWI na kuzaliwa kwa watoto haramu, hali inayochangia kuongezeka kwa matatizo mengi ya kijamii. Katika wakati huu ambapo ulimwengu unaendelea kushuhudia aina nyingi za machafuko, Masumi (2008), anahimiza kuhusishwa na kutumiwa kwa wanawake katika kuleta suluhu. Anaendelea kusema kuwa

wanawake watafaulu kufanya hivyo kutokana na uvumilivu wao katika kusuluhisha matatizo ya kijamii.

Tafiti zilizoendeshwa kuhusu vichocheo vya machafuko nchini Rwanda katika mwaka wa 1994, sawia na matokeo ya ripoti zilizoshughulikia ghasia za baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2007 nchini Kenya, zinabainisha dhima ya lugha katika kuchochea machafuko, yawe ya kisiasa au ya kikabila. Hata hivyo, lugha inachukuliwa kama upanga wenye ncha mbili na hukata kotekote (Ogechi, 2011). Kwa mintarafu hii, utafiti huu unalenga kuonyesha jinsi lugha mbali na kuwa chombo cha kuendeleleza uhasama, inaweza pia kutumika kama gundi ya kuunganisha jamii na kuhimiza amani na maridhiano.

Amani na maridhiano ni nguzo muhimu katika maendeleo ya nchi yoyote ile. Hivi viwili vikikosekana, nchi yoyote ile haiwezi kustawi kimaendeleo (Kriegler, 2008). Anavyodokeza Waki (2008), hali ya amani na maridhiano imekuwepo nchini Kenya kwa nyakati nyingi tangu nchi ijinyakulie uhuru wake. Hata hivyo, anatambua kuwa hali hii imetatizika katika nyakati fulani hususan nchi inapoingia katika shughuli ya kuchagua viongozi wapya katika uchaguzi mkuu. Aidha kumekosekana amani na maridhiano miongoni mwa makabila yanayopakana kutokana na tofauti za kila mara ambazo zimekuwepo kwa miaka mingi sasa (Nangulu, 2007). Katika nyakati hizo za kuzua vurugu, vijana kwa kiasi kikubwa ndio hutumiwa na wanasiasa (Kandagor, Kiprono na Simotwo 2012).

Vijana ambao aghalabu hutumiwa kuzua vurugu nchini Kenya hujumuisha asilimia kubwa ya wapigaji kura nchini. Kwa mujibu wa Kandagor, Kiprono na Simotwo (2012), katika uchaguzi wa mwaka 2007, kulikuwa na jumla ya vijana milioni 11 waliosajiliwa kupiga kura. Idadi hii ni takribani asilimia 75 ya watu wote waliosajiliwa kupiga kura wakati huo ambapo kulikuwa na jumla ya Wakenya milioni 14 waliosajiliwa kama wapigaji kura. Watafiti hawa walikisia kuwa wangesajiliwa takribani vijana milioni 16 katika uchaguzi wa mwaka wa 2013. Kundi hili sharti lithibitiwe vilivyo lisije likajiingiza katika machafuko sawa na yale yaliyoshuhudiwa katika mwaka wa 2007.

Kati ya mwaka wa 1963 nchi ya Kenya ilipojipatia uhuru wake kutoka kwa wakoloni hadi mwaka wa 1987, kulipokuwa na uchaguzi mkuu wa mwisho katika mfumo wa chama kimoja, kulikuwa na hali ya utulivu wakati wa kupiga kura katika sehemu nyingi za nchi (Elischer, 2008). Katika kipindi hiki, nchi hii ilipata kuongozwa na marais wawili, hayati Mzee Jomo Kenyatta, rais mwanzilishi wa taifa la Kenya na rais wa pili, Daniel Toroitich arap Moi. Katika kipindi hicho, kulikuwa na chama kimoja tu kilichoongoza nchi nacho kilikuwa Kenya African National Union (KANU). Wakati huo, rais hangepingwa kwenye kura. Kile ambacho labda kingemtoa uongozini wakati huo kingekuwa kifo au mapinduzi.

Mnamo mwaka wa 1991, kulikuwa na shinikizo kutoka kwa wanasiasa na makundi ya kijamii ili kuubadili mfumo huo wa uongozi wa chama kimoja (Mutua, 2008). Wengi waliuchukulia kuwa wa kiimla na uliopitwa na wakati. Kundi hili liliongozwa na wanasiasa kama vile Marehemu Jaramogi Oginga Odinga, Marehemu Martin Shikuku,

Kenneth Matiba, Raila Odinga, Marehemu George Anyona, Marehemu Masinde Muliro, Paul Muite, Kasisi Timothy Njoya miongoni mwa wengine wengi. Juhudi na kampeni zao zilipelekea kubadilishwa kwa kifungu cha 2(A) cha katiba ya wakati huo. Hii ilimaanisha kuwa chaguzi za baadaye zingefuata mfumo wa vyama vingi. Aidha, kiti cha urais nacho kingewaniwa kama vile vya ubunge kwa mara ya kwanza katika historia ya taifa la Kenya (Mara, 2009). Kuanzia wakati huu, hisia za uzalendo finyu wa kikabila zilichochewa ambapo viongozi wa upinzani waliitwa wenye ukabila na wale waliokuwa mamlakani (Ntabo & Ogechi, 2009).

Chaguzi zote zilizofanywa baada ya mfumo wa siasa ya chama kimoja kubadilishwa zilipata kushuhudia vurugu na vita baina ya makabila yaliyopakana (Kriegler, 2008). Maeneo mengi yaliyoshuhudia vita hivi yalikuwa sehemu zile zinazomilikiwa na makabila ya wawaniaji wa urais. Nchi ya Kenya ina makabila 42 (Ogechi, 2012). Kabila kwa mujibu wa *Kamusi Kamili Ya Kiswahili* (Longhorn, 2009) ni kundi la watu wenye mila na desturi moja na huongea lugha moja. Makabila ya Kenya yamegawika katika makundi matatu makuu ambayo ni Bantu, Nailotiki na Kushitiki. Mifano ya Wabantu ni kama vile Wakikuyu, Waluhya, Wakamba, Wakisii, Wameru n.k. Wanailotiki ni Waluo, Wakalenjin, Wamaasai, Waturkana n.k. Wakushitiki ni Warendile, Wasomali, Waborana na Wagabra. (Whiteley 1973, Githinji 2006 & Ogechi 2012). Katika makundi haya yote, makabila ya wasemaji wengi ni Wakikiyu (21%), Waluhya (14%), Waluo (14%), Wakalenjin (12%) na Wakamba (11%) (Elischer 2008, RoK 2010 & Ogechi 2012). Aghalabu wanasiasa maarufu wanaowania urais nchini Kenya hutoka katika makabila haya.

Kati ya chaguzi zote zilizofanywa baina ya mwaka wa 1992 hadi mwaka wa 2007, ule wa mwaka wa 2002 haukuripoti visa vingi vya vurugu. Kulikuwa na kiasi kidogo cha machafuko mara tu baada ya shughuli ya kupiga kura ambapo Mwai Kibaki alitawazwa rais. Wakati huo, wawaniaji wakuu wa urais waliokuwa na ushindani mkuu, yaani Mwai Kibaki na Uhuru Kenyatta walitoka katika kabila moja, la Wakikuyu. Hali hii ilibadilika kabisa katika uchaguzi wa mwaka wa 2007. Wakati huo, nchi ya Kenya ilipata kushuhudia machafuko ya kisiasa ambayo hayajapata kuonekana tangu hapo awali. Wapinzani wakuu wa kiti cha urais wakati huo walikuwa Mwai Kibaki (wa kabila la Wakikuyu) na Raila Odinga (wa kabila la Waluo). Matokeo ya vurugu hizo yalikuwa vifo vya jumla ya Wakenya takribani 1,500, wengine takribani 350,000 walihamishwa kutoka makwao, wanawake takribani 3,000 kubakwa na takribani Wakenya 10,000 wakapata kutorokea nchi jirani ya Uganda kama wakimbizi (Waki, 2008). Hali hii kulingana na uchunguzi uliofanywa ilisababishwa na matamshi ya baadhi ya wanasiasa na hata vyombo vya habari (KNCHR & KHRC, 2006, Waki, 2008, Mukhongo, 2009 na Njogu, 2012).

Licha ya kuwa vyombo vya habari ni muhimu sana katika kuwapasha wananchi habari kuhusu yanayoendelea ulimwenguni kote, vinaweza pia kutumiwa kutekeleza maovu kama vile kueneza chuki miongoni mwa wananchi. Utafiti wa Njogu (2012), ulidhihirisha namna redio ilivyotumiwa nchini Kenya kuendeleza uhasama baina ya wanajamii. Anasema kuwa kinyume na vyombo vingine vya habari, redio ina uwezo wa kusambaza habari zake kwa watu wengi na kwa muda mfupi sana. Hii ni kutokana na

sababu kuwa vituo vingi vya kurushia matangazo ya redio nyingi nchini Kenya havibagui kati ya waliosoma na wale ambao hawajasoma. Vingi vyao hutangaza kwa lugha za kienyeji na inakuwa rahisi kwa uchochezi kuenezwa kupitia kwa redio hasa pale ambapo msimbo unaoeleweka na kundi maalum la watu unatumiwa. Aidha, ni rahisi kutumia redio kwa kuwa inabebeka na inaweza kutumia nguvu za betri tofauti na vyombo vingine ambavyo huhitaji nguvu za umeme kuendeshwa (Kawoya & Makokha, 2009).

Jamii ya Kenya kwa jumla imegawika pakubwa katika misingi tofauti tofauti. Anavyohoji Mutua (2008), hizi tofauti ni pamoja na za kimaeneo, kielimu, kidini, kimapato, kiumri na kijinsia miongoni mwa nyingine nyingi. Anaongezea kuwa hizi tofauti huchangia kuendeleza zaidi uhasama uliopo baina ya makabila tofauti nchini, uhasama ambao umekuwepo kwa miaka mingi sasa. Njogu (2012), akizungumzia tofauti za kimaeneo miongoni mwa wanajamii zilizopo nchini Kenya, anahoji kuwa zimeenea sana kiasi kwamba makabila fulani nchini Kenya huhusishwa na maeneo fulani ya nchi.

Mathalan, kabila la Waluo huhusishwa na mkoa wa Nyanza, Waluhya na mkoa wa Magharibi, Wakalenjin na mkoa wa Bonde la ufa, Wakikuyu na mkoa wa Kati, Wakamba na mkoa wa Mashariki, Waswahili na mkoa wa Pwani na kadhalika. Wakati wa uchaguzi mkuu, wapigaji kura huunga mkono wawaniaji wa urais wa vyama vya maeneo yao ambavyo vingi husimamiwa na viongozi kutoka maeneo hayo. Njogu anaongezea kuwa katika hali hii, watu kutoka maeneo mengine waliohamia sehemu hizi wakijitafutia riziki huchukuliwa kama adui wakati wa kupiga kura kwa imani kuwa watawaunga mkono

wawaniaji wa uongozi kutoka sehemu walizotoka. Hivyo, huwa rahisi wao kulengwa kunapotokea mapigano ya aina yoyote ile hasa yale yanayohusisha makabila tofauti.

Makabila mengi nchini Kenya yanaishi katika hali ya kutoaminiana inayosababishwa na uchochezi kutoka kwa baadhi ya wanasiasa (Amuka, 2008). Hii imesababisha kuwepo kwa chuki bila sababu baina ya makabila tofauti. Baadhi ya wanasiasa hukataa kuwaunga wawaniaji wa uongozi kutoka kwa makabila mengine kwa visingizio visivyo vya maana kama vile vya viongozi hao kutoka kwa kabila lisilotahiri (Ibid). Aidha ukosefu wa amani baina ya makabila tofauti umechangiwa na visa vidogo vidogo kama vile vya wizi wa mifugo baina yao, na ung'ang'aniaji wa raslimali chache zilizopo kama vile maji na sehemu za malisho ya mifugo . Hapo awali, tofauti za aina hii zilishuhudia mapigano baina ya makabila tofauti kama vile Wapokot na Waturkana, Wakipsigis na Wakisii, Wamasai na Wakisii (Nangulu, 2007). Aidha mapigano yamewahi kutokea kati ya Wapokomo na Waorma katika eneo la Tana Delta (KRCS, 2012). Kufikia Septemba 2012, vurugu kati ya Wapokomo na Waorma zilikuwa zinaendelea na zimekuwepo tangu nchi ya Kenya ilipojinyakulia uhuru wake. Mapigano kati ya makabila haya mawili kulingana na ripoti zilizotolewa huzuka kila taifa linapojiandaa kwa uchaguzi mkuu. Mapigano kati ya makabila hayo yalishuhudia vifo vya zaidi ya watu mia moja katika mwezi wa Septemba pekee huku zaidi ya watu elfu moja wakitoroka makwao (KRCS, 2012).

Nchi ya Kenya ina miaka hamsini tangu ijinyakulie uhuru wake. Machafuko na ghasia za mara kwa mara baina ya makabila na makundi tofauti ya kijamii nchini ni jambo

linalokwamiza maendeleo na kuathiri kwa namna hasi ukuzaji wa amani na utangamano. Machafuko haya wakati mwingine yanatokana na kutowajibika kwa viongozi wa kisiasa katika matumizi yao ya lugha. Wanasiasa huitumia lugha katika hotuba zao na pia katika nyimbo za wanamuziki wenye jumbe mwafaka. Mathalan, mnamo mwaka wa 2002, wimbo *'Unbwogable'* wa Gidigidi Majimaji ulitumika sana katika kampeni za uchaguzi mkuu (Nyairo & Ogude. 2005)

Inavyoelekea, machafuko yanaweza kuzuiliwa na vile vile kuzimwa kwa kutumia lugha katika mikondo mbalimbali kama vile mazungumzo, muziki, redio na kadhalika katika nchi tofauti duniani. Kwa kuwa Kenya ilishuhudia machafuko baada ya uchaguzi mkuu wa 2007, tunajiuliza: Wanasiasa huchangia vipi katika machafuko? Je, machafuko yaliweza kumalizwa kwa mbinu zipi? Je, vijana walihusishwa vipi kuzima machafuko? Lugha ilitumika vipi katika juhudi hizo za amani na maridhiano? Wanamuziki na hasa vijana walitunga muziki wa amani na maridhiano? Iwapo ndio, lugha ya amani na maridhiano ilijitokeza vipi? Utafiti huu ulilenga kuyajibu baadhi ya maswali haya. Muziki wenye lugha ya amani na maridhiano ulilengwa huku umuhimu wake katika kuwapatanisha Wakenya ukizingatiwa.

## 1.2 SWALA LA UTAFITI

Utafiti huu unalenga kuonyesha jinsi muziki kupitia uteuzi wake wa maneno uliofanywa katika muziki unavyohimiza amani na maridhiano miongoni mwa wananchi nchini Kenya. Hususan umejikita katika muziki usio wa kidini, ulioimbwa kwa lugha ya Kiswahili na/au Sheng', baada ya mwaka wa 2007 na kufikia mwaka wa 2012. Utafiti

huu uliangazia uteuzi wa msamiati na uundaji wa tungo zinazohusiana na maudhui ya amani na maridhiano. Vilivile, uumbuji wa wasanii uliangaziwa kwa lengo la kufafanua uwasilishaji wa maudhui ya amani na maridhiano kwa wanajamii kupitia muziki nchini Kenya.

## 1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI

Utafiti huu unalenga:

i. kubainisha muziki uliotumiwa kuendeleza amani na maridhiano nchini Kenya kati ya mwaka 2008 na 2012.

ii. kupambanua matumizi ya kipekee ya lugha katika ubunaji wa wanamuziki kwa kuzingatia maneno, vishazi na sentensi.

iii. kufafanua ujumbe katika muziki wa amani na maridhiano nchini Kenya (2008 – 2012).

## 1.4 NADHARIA TETE

Nadharia tete zilizoongoza utafiti huu ni kama ifuatavyo:

i. kulikuwa na muziki uliotumiwa kuendeleza amani na maridhiano nchini Kenya katika kipindi cha kati ya mwaka wa 2008 na 2012.

ii. muziki wa amani na maridhiano huakisi uteuzi wa kipekee wa lugha.

iii. ujumbe katika muziki wa amani na maridhiano nchini Kenya (2008 - 2012) ulisimbwa ili kufanikisha amani na maridhiano.

## 1.5 UMUHIMU WA UTAFITI

Jamii mbalimbali ulimwenguni hukumbwa na changamoto anuwai za kimahusiano ambazo aghalabu husababisha kutokuwepo kwa amani na maridhiano. Mbinu mbalimbali zikiwemo mazungumzo ya kuleta mapatano, matumizi ya majeshi na kadhalika, zimewahi kutumiwa kusuluhisha matatizo hayo. Utafiti huu unachangia kwa kutoa mbinu ya ziada ya kusuluhisha migogoro katika jamii kupitia matumizi ya lugha kiumbuji katika burudani.

Aidha kwa vile lugha hutekeleza majumu mbalimbali katika jamii, utafiti huu utasaidia kuonyesha kuwa katika kuangalia majukumu ya lugha, si lazima majukumu hayo yajitokeze katika lugha ya kawaida tu bali pia yanaweza kujitokeza katika masuala ya kisanaa.

Vilevile, utafiti huu utakuwa mchango muhimu kwa watafiti wa baadaye wanaonuia kuendesha tafiti hasa katika uwanja huu kwa kudhihirisha ufaafu na ufanisi wa mbinu za kupata data katika lugha thabiti  na zile ambazo si thabiti.

Taaluma ya isimu jamii na taaluma zingine kama vile sosholojia na sayansi ya mawasiliano zinazotumia lugha katika kudhihirisha mahusiano tofauti ya kijamii pia zitanufaika kutokana na mchango wa utafiti huu. Hii inalingana na kile Kerlinger (2000) anachokipendekeza kuwa utafiti wowote ule sharti uzalishe maarifa mapya, uvumbue ukweli kuhusu dhana husika na uongezee uelewa bora zaidi kuhusu dhana hiyo inayotafitiwa.

## 1.6 UPEO WA UTAFITI

Utafiti huu ulilenga kuchunguza lugha ya amani na maridhiano katika muziki na jinsi wasanii wanavyoteua maneno na kuunda sentensi zao ili kuwasilisha dhamira katika muziki huo. Data za utafiti huu zilitokana na nyimbo 20 zilizoimbwa na wanamuziki vijana nchini Kenya kati ya mwaka wa 2008 na 2012. Nyimbo hizo ni zile zilizoshughulikia amani na maridhiano zilizoimbwa kwa lugha ya Kiswahili au/na Sheng' na zisizo za kidini. Data iliyotokana na nyimbo hizi ilichanganuliwa kwa kuangazia maneno, vishazi na sentensi zilizohusu amani na maridhiano.

## 1.7 MISINGI YA KINADHARIA

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya majukumu ya lugha kama ilivyopambanuliwa na Halliday (1973) na baadaye kuendezwa na wataalamu wengine kama vile Reagan (1992) na Moto (2004). Aidha utafiti huu ulikopa mawazo ya Fairclough (1992) kuhusu uchanganuzi makinifu.

Kuhusu nadharia ya majukumu ya lugha (Halliday, 1973) utafiti huu umetumia yale majukumu yanayozingatia malengo ya utafiti wenyewe. Haya ni yale yanayohusiana na kufahamisha, kutoa maelezo ya kukemea inapobidi, kutoa hisia na silika fulani na hatimaye kutathmini na kutoa hukumu fulani kuhusu jambo fulani katika jamii. Wasanii wa muziki hulenga kutimiza malengo fulani kupitia nyimbo zao. Hii nadharia ilikuwa mwafaka kwa utafiti huu kwa vile katika kuyatathmini malengo ya utafiti, vigezo mbalimbali vya majukumu ya lugha kama vinavyoelezewa na Halliday vimeangaziwa.

Halliday ameyaelezea majukumu ya lugha kwa njia butu bila kuhusisha jamii. Hata hivyo, utafiti huu umelenga kuhusisha jamii katika utalii wake. Hii ndiyo sababu tasnifu hii imejumuisha nadharia ya uchanganuzi makinifu wa matini kwa mujibu wa Fairclough (1992, 1995). Nadharia hii inapendekeza kuwa ni sharti matini yoyote ile ihusishwe na jamii ambamo inazalishwa. Kwa jinsi hii, nadharia hii imefaa katika utafiti huu hasa pale ambapo maana kutokana na matini zilizokusanywa ilikuwa inashughulikiwa.

Kwa mujibu wa Fairclough (1992), uchanganuzi makinifu wa matini unaweza kutokea kwa jinsi tatu tofauti. Kwanza, ni pale ambapo uchanganuzi huo unapaswa kujikita katika vipashio vya kiisimu kama vile vya leksimu, sarufi, muwala na muundo wa matini. Pili, ni pale ambapo uchanganuzi unashughulikia diskosi kama mchakato wa kijamii. Hii ni kutokana na sababu kuwa matini yoyote ile ni mali ya jamii na matini hiyo itatekeleza wajibu wake kutegemea matarajio ya jamii ambamo matini hiyo imezalishwa. Tatu, ni pale ambapo diskosi yoyote ile itashughulikiwa kama jambo la mazoea ya kijamii. Hii inamaanisha kuwa diskosi fulani hutokea katika muundo maalum katika jamii yoyote ile. Katika utafiti huu, msisitizo umewekwa kwenye vipengele vya uchanganuzi wa leksimu pamoja na uchanganuzi wa diskosi kama mchakato wa kijamii. Hii ina maana kuwa leksimu katika muziki ulioshughulikiwa zilichanganuliwa kwa kuzihusisha na muktadha zilimozalishwa. Hivyo basi, hapa uchanganuzi wa data uliangazia muziki kama mojawapo ya matendo ya kijamii yanayoashiria mipangilio ya kimahusiano katika jamii husika.

Nadharia ya uchanganuzi makinifu wa matini hulenga kudhihirisha namna mahusiano ya kijamii, utambulisho wa wahusika, maarifa au ujuzi pamoja na uwezo wa wahusika unavyoundwa katika jamii kupitia maandishi au mazungumzo. Hii ilipelekea Fairclough na Wodak (1997) kujadili kuhusu umuhimu mbalimbali wa uchanganuzi wa diskosi mojawapo ukiwa ni pamoja na kusaidia katika kushughulikia na kutoa suluhu kuhusu matatizo ya kijamii. Mawazo yao yalinisaidia kuchanganua uteuzi wa maneno katika muziki ili kupata maana zake kama zilivyonuiwa na watunzi wa muziki tofauti tofauti.

Uchanganuzi wa lugha kimakinifu ni mbinu ya kuchanganua diskosi zenye kujenga mahusiano ya kijamii kwa kurejelea uamilifu wa vipengele vya kiisimu. Wodak (1995:204) akitoa mchango wake kuhusu uchanganuzi makinifu wa diskosi anasema kuwa:

> Uchanganuzi makinifu wa diskosi hushughulikia kwa kiasi kikubwa mifanyiko ya kijamii ambayo mingi huchukua miundo ya kiisimu…Uchanganuzi huo huchunguza uhusiano uliopo kati ya lugha na jamii. (T.Y).

Anavyosema Odouri (2005), kanuni moja kuu ya uchanganuzi makinifu ni kuwa namna tunavyoandika na kile tunachokisema si dhahania. Tunachokisema au tunachokiandika huwa na lengo mahsusi hata kama uteuzi wa lugha unafanywa kwa njia razini au la. Ni katika muktadha huu ambapo uchanganuzi makinifu ulitumika katika utafiti huu ili kuweza kuelewa kilicholengwa na wanamuziki katika nyimbo zilizoteuliwa.

Nadharia ya uchanganuzi makinifu inahusisha mielekeo ya taaluma tofauti kama vile uamali, nadharia ya matendo kauli na semantiki miongoni mwa nyingine. Mikondo hii yote inatambua matini kama miundo maalum ya matendo ya kijamii ambayo hutokea

katika miktadha changamano ya kijamii. Uchanganuzi makinifu kwa hivyo hutalii lugha kama aina mojawapo ya matendo ya jamii. Inatambua kuwa matini huzalishwa na wanajamii ambao ni washiriki katika jamii kubwa inayowazunguka. Hivyo basi, utafiti huu haukuwa na budi ya kuzihusisha matini za uchanganuzi na jamii ambamo zilizalishwa ili kupata maana kamili iliyokusudiwa kuwasilishwa kwa hadhira iliyolengwa na nyimbo tofauti tofauti.

Uchanganuzi wa matini za utafiti huu uliendelezwa kwa kuzingatia vigezo viwili vikuu:

i). Kaida za matumizi ya lugha na uelewa kwamba, maana ya neno hurejelewa kwa kuhusishwa na maneno mengine katika sentensi, na kwa kuhusisha sentensi nyingine katika matini.

ii). Muktadha wa mazingira. Hapa niliongozwa na dhana kuwa maneno hayana maana moja tu lakini huweza kupata maana zaidi kwa kutegemea mazingira ambamo neno hilo limetumika. Isitoshe, maana ya neno inaweza kubadilika kutegemea matumizi yake katika sentensi na hata kupata maana zaidi kutokana na muktadha.

Anavyohoji Fairclough (1992), lengo kuu la uchanganuzi makinifu wa matini ni kuchunguza uhusiano uliopo katika matumizi ya lugha na muundo wa kijamii ambamo lugha fulani inatumika. Kwake, msisitizo upo katika uchanganuzi makinifu wa diskosi na na dhima yake katika kuuelezea ulimwengu na kufafanua mabadiliko ya kijamii ambayo hutokea kila mara.

Fairclough (1995), alitambua mihimili muhimu ya uchanganuzi makinifu ambapo alidokeza kuwa diskosi yoyote ile huundwa na kuongozwa na mambo yafuatayo:

i). muundo wa kijamii (unahusisha tabaka, hadhi, umri, kabila na uana).

ii). utamaduni.

iii). diskosi (kwa maana ya maingiliano ya lugha na muktadha). Hii inamaanisha kuwa diskosi tunazotumia huchangia katika kuunda utambulisho wetu, mahusiano yetu na mifumo ya maarifa na imani zetu. Fairclough (2004), anahoji kuwa matini ni zaidi ya yale maneno yaliyobebwa mle ndani bali ni namna maneno yanavyotumiwa katika muktadha mahsusi wa kijamii.

## 1.8 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Baadhi ya tafiti na wataalamu mbalimbali wamezungumzia umuhimu wa muziki katika kushughulikia maswala ya kijamii. Wells na Hakanen (1991), wakizungumzia ufaafu wa muziki katika kusuluhisha matatizo ya kijamii walielezea kuwa muziki unaweza kutumiwa kwa namna nyingi katika kuchangia amani na utulivu katika jamii. Unaweza kutumiwa na waimbaji katika kuzieleza hisia zao za ndani. Waliongezea kuwa muziki unaweza kuleta mawasiliano  na mahusiano ya karibu kati ya watu au makundi ya watu ambao hawakuwa wanawasiliana hapo mbeleni.  Isitoshe wataalamu hawa walihoji kuwa muziki unaweza kutumiwa katika kuleta maridhiano na kuhimiza msamaha kati ya makundi yaliyokuwa yanazozana. Wanasema kuwa hili linawezekana kutokana na sababu kuwa muziki haujui mipaka ya kitaifa, lugha au kabila.

Gekau (1993), anadai kuwa muziki ni kioo cha mambo yalivyo katika sehemu tofauti za ulimwengu. Yanayoimbwa ni yale ambayo kwa hakika yanatokea katika ilimwengu huu na wala si kuwa yanaimbwa tu bila kuwepo.

Hubley (1995), anapendekeza kampeni dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI kupitia kwa muziki. Anasema kuwa hii itasaidia katika kuwafikia watu ambao hawakuenda shule, walioacha shule na sasa wanafanya kazi na wale wote walio nje ya shule kunakofunzwa mambo kuhusu VVU/UKIMWI. Anahimiza vikundi vya wanamuziki waliosifika kuimba kuhusu maswala ya afya, likiwemo lile la VVU/UKIMWI. Maoni yake ni kuwa watu wengi wanaopenda muziki watapata fursa ya kuzipata habari muhimu kuhusu ugonjwa huu kupitia kwa muziki ule wanaousikiza. Anatoa mfano wa nchi ya Uganda ambako video ya muziki iliyohusu UKIMWI iliandaliwa na kusambazwa nchini kote. Muziki huo uliimbwa na wanamuziki waliosifika mle. Anaendelea kutoa mifano ya miziki zaidi huku akitaja ule wa mwanamuziki maarufu Remo Fernandes nchini India aliyeimba wimbo uliopendwa na wengi. Wimbo huo ulihusu 'Ngono salama.' Mfano mwingine anaotoa ni ule wa nchini Malawi ambako kulichezwa muziki aina ya 'Rap' ulioshabikiwa na wengi. Muziki huo uliohusu UKIMWI ulichezwa katika redio ya kitaifa na kusambazwa nchini mle kupitia kwa kanda.

Negus (1997), akizungumzia umuhimu wa muziki kule Uingereza anafananisha nyimbo na matini nyingine yoyote ile ambayo huangazia mambo kuhusu jamii inamotumika. Huu ufafanuzi wake unaelekea kulingana na kuafikiana na kile anachokielezea Fairclough (1992), kuhusu matini. Anajeleza matini kuwa chochote kile kinachotokea kuhusiana na

mtagusano wa kijamii, kiwe semwa au andishi. Kwa hivyo, nyimbo zote ni zao la kijamii katika jamii zinamotumika.

Kwaramba (1997), anashikilia wazo sawa na la Fairclough ambapo anadokeza kuwa matini hazishughulikiwi tu kama zao la ubunifu wa kifasihi bali ni zao la michakato ya kijamii na pia ni nyenzo muhimu ya kuumba na kuumbua michakato hii. Anaongezea kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya lugha, uwezo na itikadi. Kwa hivyo, mwanamuziki hutunga muziki wake kuhusiana na yale anayoyashikilia kuwa ya kweli kuhusu jambo fulani katika jamii anayoitungia.

Anavyosisitiza Barber (1997), kuwa methali haikamiliki mpaka ihusishwe na tukio maalum, ndivyo hali ilivyo kwa muziki. Anaeleza kuwa mbinu nyingi za lugha hutumiwa na wanamuziki katika uimbaji wa muziki wao. Maana ya maneno kupitia mbinu hizo hueleweka yanapotumiwa tu kwa kuhusishwa na matukio fulani ya kijamii ambamo muziki huo unachezwa.

Akitoa mchango wake kuhusu muziki, Fair (1997), anasema kuwa muziki ni nyenzo muhimu ambayo kwayo jamii inaweza kuangazia shida zake na kuzitafutia suluhu. Anaendelea kudai kuwa muziki ni kifaa muhimu sana kinachotumiwa na wenyeji katika kuwafikia watu wengine katika ulimwengu huu mpana. Kwa kufanya hivyo, hata na wao hujifunza mengi kuhusu jamii zingine kupitia kwa muziki. Anadai kuwa, bila muziki watu wangejua machache sana kuhusu ulimwengu wa nje na kwa njia hiyo, shughuli nyingi za kijamii zingekwamishwa.

Wekesa (2002), naye anadokeza kuwa kutokana na kusifika kwa wanamuziki maarufu katika nchi, wanasiasa huwatumia katika kuendeleza na kutekeleza shughuli zao za kisiasa. Anatoa mfano wa jinsi mwanamuziki Joseph Kamaru alivyotumiwa na serikali ya wakati huo nchini Kenya, anasema kuwa katika kilele cha kampeni za siasa ya vyama vingi nchini Kenya mnamo mwaka wa 1992, Kamaru aliyetoka kwa kabila la Wakikuyu aliaminika kuwa angekishindia chama cha KANU kura nyingi za Wakikuyu. Kwa hivyo, chama cha KANU kilimtumia katika kampeni zake katika Mkoa wa Kati ambapo wananchi wengi walihudhiria tamasha zake ambazo KANU ilitumia kama jukwaa la kampeni zake. Muziki wake ulichezwa sana kupitia shirika la utangazaji la KBC kupitia kwa redio na runinga.

Muziki wa Kamaru ulipata kusikilizwa na kushabikiwa na wengi kutokana na kile alichokielezea Street (1997), kuwa kupitia kwa muziki, watu hupata fursa ya kufurahi na kuonyesha hisia zao za kisiasa. Kutokana na muziki unaopendwa na wengi, watu hujihusisha na siasa kwa sababu ya hisia inazoziibua, utambulishaji unaotokana na muziki huo na matarajio mengi unayoyazua. Muziki na siasa kwa hivyo vitaandamana sambamba katika shughuli za kawaida za wanajamii.

Wakitoa mchango wao kuhusu umuhimu wa muziki, Gabrielsson na Juslin (2003), walisema kuwa watu wakiimba muziki au wakisikiliza muziki, hupata kueleza hisia zao pamoja na kupunguza viwango vyao vya mfadhaiko utokanao na shida fulani.

Wamitila (2003), anaeleza jinsi muziki unavyotumiwa kuendeleza shughuli tofauti za kijamii. Anasema kuwa nyimbo huwa na mawazo mazito na huonyesha uhusiano wa kijamii, mgogoro, kukejeli, kuliwaza, kubembeleza, kutumbuiza, kuongoa na kuburudisha. Takribani shughuli zote za binadamu kama vile kulima, kufuga, kuwinda ndege au wanyama shambani, kutwanga, kupalilia na kuvuna, kusuka, kufua, kujenga, kupasha tohara ( kwa jamii zinazohusika), kuoa, kulea na kubembeleza mtoto, kufariji na kuliwaza wakati wa mazishi na kuzika huandamana na nyimbo  na uimbaji. Anavyosema, kila shughuli katika msingi huu huwa na aina yake ya nyimbo.

Akiongezea, Wamitila anahoji kuwa muziki una historia ndefu katika jamii zetu. Tunaweza kusema kuwa muziki ulianza pindi binadamu alipopata lugha na kuweza kuzieleza na kuzifumbata hisia zake. Hisia zilizowasilishwa kwa njia ya kuimbwa huwa na athari kubwa. Pili, uimbaji wa nyimbo pia ni njia mojawapo ya kuzitoa hisia za kuumizwa na kukandamizwa alizonazo mtu, yaani hisia za ndani. Huwa ni njia ya kuutakasa moyo wake na kuziondoa hisia hizo mbaya na hasi.

Kulingana na utafiti wake, baadhi ya sifa zinazotambulisha muziki ni kama zifutazo:

i). Maneno yanayoimbwa au matini yenye mpangilo maalum.

ii). Hadhira inayoimbiwa.

iii). Muktadha unaofungamana na wimbo, na kadhalika.

Isitoshe, anapambanua kuwa mbali na muziki kuwa na umuhimu wa kuwawezesha waimbaji au mwimbaji kuzitakasa hisia zinazombana kama za chuki, hasira, huzuni, na kadhalika, majukumu mengine ya muziki ni kama yafuatayo:

i). Muziki huwa kama hifadhi au rekodi za matukio muhimu ya kihistoria katika jamii mbalimbali.

ii). Muziki hutumiwa kuhamasisha watu kutenda jambo fulani au kushirikiana katika matendo tofauti tofauti. Kwa njia hiyo, huweza kutumika kuchochea hisia za kuichangamkia shughuli fulani.

iii). Muziki huweza kutumiwa kama burudani. Muziki ni njia nzuri ya kumpa msikilizaji au hata mwimbaji burudani nzuri.

iv). Aidha, muziki hutumiwa kama nyenzo muhimu ya kupitisha thamani za kitamaduni katika jamii mbalimbali. Hii ni kusema kuwa nyimbo za jamii mbalimbali huakisi vipengele mbalimbali kuhusu utamaduni wa jamii hiyo.

v). Muziki ni njia nzuri ya kuelimisha na kupitisha maarifa mbalimbali miongoni mwa wanajamii.

Wamatila (ibid), anafafanua kuwa shughuli nyingi za kijamii hufungumana na matumizi ya nyimbo. Nyimbo hutumika kama kiungo kinachobeba ujumbe maalum. Aghalabu, lugha inayotumika katika nyimbo ni ya kimafumbo. Mafumbo ndiyo hubeba ujumbe unaolengwa. Hadhira inayolengwa hulazimika kutafakari kwa undani ndipo ipate ujumbe

uliomo kwenye mafumbo yaliyotumika. Isitoshe, nyimbo huimbwa kwa minajili ya matumizi au utendakazi wa aina fulani mahususi. Matumizi ya nyimbo hujikita katika kupasha maadili yanayoongozwa na kurekebisha tabia ya jamii husika. Yaliyomo katika muziki huongozwa na matukio ya kila siku katika jamii husika.

Kwa mujibu wa Hofmeyr (2004), ujumbe katika muziki wa wanamuziki maarufu huwafikia watu wengi na wa viwango tofauti kwa njia rahisi. Dai hili la Hofmeyr ni la ukweli hasa ukichunguza hali ya mambo ilivyo nchini mwetu Kenya. Utakuta kuwa muziki wa wasanii walio maarufu husikilizwa na watu wengi kote nchini. Hii ni kutokana na sababu kuwa jina la msanii linajulikana kote hata kama msanii huyo hajapata kuyatembelea baadhi ya maeneo ambako muziki wake unasikika. Huwa ni rahisi kwa habari muhimu kwa taifa kusambaa kwa urahisi na kwa haraka kupitia kwa muziki wa msanii kama huyo.

Umuhimu wa muziki kama kitulizo katika jamii umehusishwa na ukweli kwamba muziki hutumiwa kwa namna sawa katika tamaduni nyingi ulimwenguni kote. Kwa mfano, miongoni mwa jamii ya Wataita nchini Kenya, muziki maalum ulitumiwa kutuliza miungu nyakati za maafa ya aina yoyote ile yaliyoikumba jamii na yaliyoaminika kusababishwa na mapepo mabaya (Akombo, 2006).

Ntarangwi (2007), anasema kuwa muziki kama njia mojawapo ya kupitisha ujumbe kwa wasikilizaji una uwezo wa kuangazia maswala yote kuhusu jamii. Hii ni kwa sababu watunzi wa muziki huo huilenga hadhira yao na yote kuhusu jamii ya hadhira hiyo. Wao

hutunga na kuimba kuhusu mambo wanayoyaona na kuyashuhudia katika jamii yao. Muziki wao hutegemewa na wengi katika kusuluhisha shida za kijamii.

Anaongeza kuwa muziki hutumiwa ili kufahamisha watu kuhusu mambo yaliyo mbali nao. Mambo hayo huhusu maswala ya kisiasa, kiuchumi na kijamii yanayotokea kwingineko mbali na waliko. Wasanii hao pia hualikwa ili kwenda kuimba katika sehemu zingine. Wanapofanya hivyo, wanakuwa kama mabalozi wa kupeleka mazuri waliyonayo na kwa njia hiyo wakayasambaza kote.

Akombo (2009), anazungumzia namna muziki unavyoweza kutumiwa katika kutuliza nyoyo za watu waliokumbwa na maafa fulani kama yale yaliyotokea nchini Kenya baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2007. Anatumia mfano wa muziki ulioimbwa na Senior private Doris Chepchumba Tanui, mwanajeshi katika kikosi cha wanahewa nchini. Huyu mwanamuziki anahimiza amani na maridhiano miongoni mwa Wakenya kwa kutumia ucheshi, sawa na alivyofanya mwanamuziki marehemu Daudi Kabaka (1939-2001) ili kufanya ujumbe wake ueleweke. Katika wimbo wake, Chepchumba anauliza ni kwa nini Mungu hakuumba Waluo wakiwa na pembe, Wakikuyu wakiwa na mikia, Wakalenjin na mabawa  na jamii nyingine zikiwa na viungo tofauti iwapo Wakenya si sawa. Anashangaa ni kwa nini wakati wa machafuko ya kisiasa ya mwaka wa 2007 watu walichoma maghala ya vyakula, shule, misitu, hospitali na hata magari wakati ambapo hivi vyote ni vifaa muhimu kwao. Anauliza watakavyoishi bila hivi vyote.

## 1.9 MBINU ZA UTAFITI

### 1.9.1 Uteuzi wa Sampuli

Sampuli ya muziki iliyotumiwa kuzalisha data ya utafiti huu imeteuliwa kimakusudi. Hii ni kwa sababu data hiyo ilihusu maudhui maalumu, katika muziki usio wa kidini na uliotolewa katika kipindi maalum. Aidha muziki uliteuliwa kutokana na umaarufu wake katika kipindi kinachocheza miziki ya aina hii kinachojulikana kama *Mambo Mseto* katika idhaa ya Citizen. Kituo hiki kwa muda sasa kimekuwa kikipeperusha hewani kipindi hiki kinachohusisha wanamuziki walioimba nyimbo tofauti kuhusu amani na maridhiano. Nyimbo ishirini za wanamuziki ishirini tofauti zilitumiwa. Uteuzi huu uliongozwa na umaarufu wa wanamuziki walioimba nyimbo zilizokuwa na jumbe za amani na maridhiano. Wanamuziki hawa ni wale waliotumiwa zaidi na mashirika tofauti (likiwemo lile la utangazaji la Citizen) katika kampeni za kuhimiza amani na maridhiano kupitia kwa maonyesho ya barabarani katika sehemu tofauti nchini Kenya.

### 1.9.2 Ukusanyaji wa data

Baada ya kuwateua wanamuziki walioimba nyimbo kuhusu amani na maridhiano na kutambua zinakopatikana jijini Nairobi, nilizinunua sidii zilizo na muziki huo ili kupata data nilizolenga. Shughuli hii iliendeshwa jijini Nairobi kutokana na sababu kuwa ndiko wanamuziki wengi wanaishi na kuendeleza shughuli zao za kimuziki. Aidha, vifaa vingi vya uzalishaji wa muziki hupatikana jijini Nairobi na kwa hivyo gharama ya uzalishaji iko chini na nilipata sampuli yangu ya muziki kwa bei nafuu. Matatizo niliyoyapata katika ukusanyaji wa data ya utafiti huu ni kuwa baadhi ya matini hazikupatikana dukani

kwa urahisi. Ilinibidi nizuru sehemu nyingi jijini kwa muda mrefu ili kufaulu katika kuzikusanya.

### 1.9.3 Vifaa vya Kukusanyia Data na unukuzi wa Data

Baada ya kununua na kukusanya sidii zilizokuwa na data muhimu nilizonuia kuzitumia katika utafiti huu, nilizicheza katika tarakilishi ili kupata maneno yaliyokuwemo kwenye sidii hizo. Nilitumia vipokea sauti vinavyobanwa kichwani kwa usikilizaji mzuri. Wakati uo huo nilitumia kalamu na daftari ili kunakili maneno katika muziki ulioteuliwa. Nilitumia unukuzi wazi ili kupata maneno yaliyotumiwa katika muziki wa utafiti huu. Nilicheza sidii mbalimbali kwa kurudiarudia mara kadhaa ili kuyapata maneno vizuri. Ni kutokana na maneno haya ndipo data za utafiti huu zilizalishwa. Haja ya utafiti huu ilikuwa ni maneno kama yalivyotumika katika data zilizochanganuliwa. Nilinukuu maneno kama nilivyoyasikia bila ya kuyafanyia marekebisho yoyote  Hata hivyo, maneno katika baadhi ya muziki hayakusikika vizuri kutokana na matamshi ya waimbaji. Hii ilipelekea shughuli ya unukuzi kuchukua muda zaidi ya ilivyopangwa.

### 1.9.4 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Data ya utafiti huu imechanganuliwa kwa kutumia maelezo ya kina ambapo vipengele vya maneno, vishazi na sentensi vimeangaziwa kwa umakinifu. Nimefanya hivi kwa kulinganisha maneno yaliyotumiwa na jozi za vibadala vyake katika lugha sanifu. Aidha, maana anuwai za maneno mbalimbali yaliyotumiwa imeangaziwa kwa kuyahusisha maneno hayo na muktadha yalimotumika kama anavyopendekeza Fairclough (1992). Vilevile, nimehusisha uteuzi wa maneno, vishazi na sentensi na majukumu anuwai ya lugha yaliyojitokeza katika muziki ulioteuliwa kwa kuzingatia nadharia ya majukumu ya

lugha ya Halliday (1973). Hatimaye, data imewasilishwa kwa kutumia njia ya kimaelezo hasa kwa kuongozwa na nadharia za utafiti.

# SURA YA PILI

# UAMILIFU WA MUZIKI KATIKA JAMII

## 2.0 Utangulizi

Sura hii inajadili uamilifu wa muziki katika jamii. Inawekea msingi mjadala unaojengwa katika tasnifu hii kuhusu majukumu ya lugha katika jamii kwa kuangazia muziki unaohimiza amani na maridhiano. Kuna nguzo tatu muhimu ambazo hukamilisha maisha ya mwanadamu katika jamii. Nguzo hizo huhusu zile shughuli ambazo mtu anajishughulisha nazo na ambazo humwathiri kisiasa, kiuchumi na kijamii. Katika sura hii, uamilifu wa muziki umeshughulikiwa kwa kuzingatia sehemu hizi tatu huku athari chanya na hasi za sehemu zote tatu zikiangaziwa. Tasnifu hii imeanza kwa kutoa habari za kiusuli kuhusu hali na uamilifu wa muziki nchini Kenya kabla ya kuzamia uamilifu wa muziki katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Hata hivyo, msisitizo umewekwa kwa uamilifu wa muziki kijamii kama njia ya kuwekea msingi mjadala katika sura ya tatu na ile ya nne.

## 2.1 Muziki nchini Kenya

### 2.1.1 Muhtasari wa hali ya muziki nchini Kenya

Kwa mujibu wa Kiplang'at (2009), muziki ni njia mojawapo inayoweza kutumiwa katika kuzielewa jamii tofauti nchini Kenya. Hii ni kutokana na ukweli kuwa muziki, miongoni mwa dhima nyingi, hufichua mengi kuhusu historia ya jamii yoyote ile, kando na kufafanua shughuli zote za kijamii, kisiasa na za kiuchumi kuhusu jamii husika. Hii

husaidia katika kufanya mambo mengi kuhusu jamii hiyo kujulikana kitaifa hata na kimataifa.

Utafiti uliofanywa na Kiplang’at kuhusu muziki nchini Kenya ulionyesha kuwa nchi ya Kenya inajivunia mitindo tofauti ya muziki kulingana na idadi ya makabila tofauti yaliyopo. Mitindo hii ya muziki ya makabila tofauti pamoja na ile ya kigeni na ya benga hujumuika katika kukamilisha shughuli za kimuziki nchini. Kutokana na mitindo tofauti ya lugha iliyopo, si ajabu kupata aina tofauti za ala za kuchezea muziki huo zikitumiwa. Anavyosema Kiplang’at (ibid), ala hizo hutengenezwa kutokana na vifaa vinavyopatikana nchini. Vifaa hivyo huwa ni pamoja na vipande vya miti kama vile mwanzi, vibuyu, pembe, matawi, mikebe, ngozi za wanyama na kadhalika. Vyombo vyenyewe hutengenezwa na wenyeji, hali inayodhihirisha ubunifu wao wa kisanaa. Miongoni mwa hivi vyombo vyote, ngoma ndicho chombo ambacho aghalabu hutumiwa na karibu jamii zote wakati wa kucheza muziki. Mathalan, wanamuziki wa jamii ya Abaluhya kutoka magharibi mwa Kenya wana mtindo wa kipekee wa densi ijulikanayo kama “Isikuti,” jina la kiasili lenye maana ya ngoma. Aina hii ya densi huhusisha wasakataji wawili, wa kiume na wa kike. Densi hii huandamana na upigaji wa ngoma pamoja na kengele za aina maalum pamoja na upulizwaji wa pembe ndefu na firimbi.

Wakamba na watu wa jamii ya Chuka nao wana mtindo wa kipekee wa kucheza muziki. Wao hucheza ngoma ndefu inayofumbatiwa kwenye kiweo. Wakamba hasa wanajulikana kwa mtindo wao wa kisarakasi wa kucheza muziki. Nyimbo zao kwa mujibu wa Kiplang’at (ibid) zimegawanywa katika makundi matatu. Kuna zile nyimbo zinazohusu nasaha, nyimbo za kuabudu na nyimbo za sifa. Nyimbo za sifa zinajumuisha zile nyimbo za mafunzo ya jando, nyimbo za kukashifu na nyimbo za ucheshi. Zile za kuabudu

zinahusu masuala ya kidini. Kwa upande mwingine, nyimbo za sifa huwahusu watu mashuhuri katika jamii.

Jamii nyingine inayojulikana kwa nyimbo zake ni ile ya Waluo. Jamii hii inahusishwa na ala ya muziki ijulikanayo kama *nyatiti*. Hii ni ala ya nyuzi inayofanana na kinubi kilichochezwa katika enzi ya miaka ya kati. Miongoni mwa jamii ya Abaluhya, ala hii inajulikana kama *litungu*, ambapo Abagusii wanaiita *obokano* na Wakalenjin huiita *bugandit.* Ala hii inapochezwa, hutoa sauti nzuri na ya kupendeza kwa wasikizaji. Ala hii aghalabu huchezwa na mtu mmoja na wakati mwingine huandamana na mshindo na kengele.

Miongoni mwa wakazi wa pwani, muziki kule hufungamanishwa na utamaduni wa Waswahili. Utamaduni huu huegemezwa pakubwa kwa muziki wa mtindo wa Taarab. Hii ni aina ya muziki uliochanganya mshindo wa kiafrika na mahadhi ya Kiarabu. Muziki wa Taarab huwakilisha utamaduni wa wanajamii wa sehemu ya pwani. Hata hivyo, muziki wa Taarab umekopa mahadhi yake na mfuo wa filamu za kihindi na bhangra.

### 2.1.2 Mtindo mpya wa muziki nchini Kenya

Miaka ya sitini ilishuhudia kuanzishwa kwa mtindo mpya wa muziki nchini Kenya. Hii ilitokana na matumizi ya gita ya kutumia nguvu za umeme kwa mara ya kwanza. Mtindo huu wa muziki uliojulikana kama *Pop* ulitokea katika nchi ya Afrika Kusini na nchi ya Zimbabwe na baadaye kutoka nchi za kimagharibi. Aidha, kulianza kuchezwa mtindo mwingine mpya wenye mahadhi ya *rhumba* uliotokea nchi ya Kongo. Mitindo hii yote ya kigeni ilichanganyika na mitindo ya kienyeji na kukazalishwa mtindo wa *Benga*. Baadaye

wanamuziki nchini Kenya walianza kuimba kwa lugha zao za kienyeji. Miongoni mwao kulikuwa ni wanamuziki kama vile D.O. Misiani, Daudi Kabaka, Sukuma Bin Ongaro na Joseph Kamaru. Isitoshe muziki wa kidini nao ulikita mizizi yake kutokana na kupamba moto kwa shughuli za kidini. Mji wa Nairobi ulipata kuwa maarufu sana barani Afrika kutokana na wanamuziki wengi waliokuja kwa maonyesho ya muziki katika miaka ya sabini na themanini. Wengi wa wanamuziki hao walikuwa kutoka bendi za Zaire walioimba kwa Lingala. Muziki wa Kilingala ungali maarufu sana miongoni mwa Wakenya hadi leo.

Baada ya miaka ya themanini, muziki nchini Kenya ulipata kushuhudia mabadiliko makubwa kutokana na athari za muziki wa kimagharibi. Kuanzia miaka ya tisini hadi hii leo, mitindo mipya ya aina ya *Reggae*, *Rap*, *Rythym* na *Blues* ilishabikiwa na Wakenya wengi. Wanamuziki wengi Wakenya walianza mtindo mpya wa kuchanganya mitindo migeni na ile ya kitamaduni katika uimbaji wao. Miongoni mwa wanamuziki wa kwanza Wakenya kuchanganya mitindo ya kigeni na ya kitamaduni walikuwa ni Joseph Ogidi na Jahd Adonijah katika mwaka wa 1999. Walijiita Gidi Gidi Maji Maji na ndio walioimba wimbo maarufa *"Unbwogable"* uliovuma sana wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2002. Mwanamuziki mwingine Mkenya aliyetumia mtindo wa kienyeji na wa kigeni katika uimbaji wake alikuwa Eric Wainaina. Yeye aliimba nyimbo kama vile *Sawa Sawa* na *Nchi ya Kitu Kidogo*. Wimbo wake, *Mkenya Daima* alioimba katika mwaka wa 2008 umechanganuliwa katika kuzalisha data ya utafiti huu.

Uchunguzi uliofanywa na Situma na Ndeta (2010) ulibainisha kuwa muziki ni njia mojawapo muhimu inayotumiwa na Wakenya katika kujitambulisha miongoni mwao. Uchunguzi huo ulihusu muziki katika vituo vya FM vya kurushia matangazo katika lugha za kiasili. Wachunguzi hawa wanasema kuwa watu wengi katika jamii hutumia muziki kama uwanja wa kuzielezea hisia zao kuhusu mambo yanayowakabili katika maisha yao ya kila siku. Aghalabu hisia hizo huwa zinahusu shughuli za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Wao wanahoji kuwa kuna uwezekano mkubwa kwa mwanamuziki aliyezongwa na shida nyingi tofauti katika jamii kutumia lugha isiyofaa katika muziki. Hali hii, wanasema, inaweza kuchangia kuzorota kwa amani katika nchi. Katika uchunguzi wao, walipendekeza kuwa ni muhimu kwa vituo vya kurushia matangazo ya redio kwa lugha za kikabila kuwa macho kuhusu aina ya muziki vinaoupeperusha hewani. Utafiti wao uligundua kuwa hakuna njia iliyowekwa nchini Kenya ya kudhibiti aina ya muziki unaochezwa katika vituo hivi.

Tafiti zilizofanywa ulimwenguni kote zinadhihirisha kuwa muziki unaweza kutumia kwa namna nyingi tofauti katika kuendeleza wanajamii. Muziki hutumia kwa njia mbalimbali lakini muhimu katika hizo ni zile zilizo na athari za kiuchumi, kisiasa na kiuchumi kwa maisha ya wanajamii.

### 2.3 Uamilifu wa muziki kiuchumi

Uchumi kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004) ni dhana inayorejelea mfumo wa mapato na matumizi ya watu katika nchi. Aghalabu hii ni shughuli nyeti sana ulimwenguni kote hii leo. Hii ni kutokana na ukweli kuwa ni kupitia kwa uchumi ambapo

mataifa mengi ulimwenguni hupata uwezo wao kijamii na kisiasa. Mataifa yaliyoendelea kiuchumi yanaenziwa kuliko yale ambayo kiwango chao cha uchumi ni cha chini. Hata na watu binafsi walio na uwezo mkubwa wa kiuchumi katika jamii kushinda wengine hustahiwa sana. Muziki umechangia kwa kiasi fulani katika kuendeleza uchumi wa ulimwengu. Maendeleo haya yameshuhudiwa kutokana na muziki ulivyochangia katika kuongezea mapato ya nchi, kuendeleza shughuli za kilimo, kuimarisha shughuli za kilimo, kuimarisha utalii na kuongezea kiwango cha ajira.

### 2.3.1 Muziki na mapato ya nchi

Laing (1996), akiandika kuhusu utafiti wake uliochunguza umuhimu wa muziki kiuchumi katika mataifa ya Jumuiya ya Ulaya, anasema kuwa shughuli za muziki zimechangia pakubwa katika uchumi wa nchi wanachama wa Jumuiya hiyo. Anahoji kuwa Jumuiya ya Ulaya ina jumla ya mataifa kumi na matano. Katika mwaka wa 1995, mapato ya jumla kutokana na shughuli za kimuziki katika Jumuiya ya Ulaya yalikuwa Euro bilioni 18.8. Kutokana na kiasi hiki, sekta ya kurekodia sauti ikiwa na makampuni 3,000 na viwanda 85 vya kutengenezea sidi pamoja na maelfu ya studio za kurekodia, ilichangia kima cha Euro bilioni 3.6 kwa uchumi wa Jumuiya hii katika mwaka huo pekee.

Akiongezea, Laing (ibid), anasema kuwa kufikia mwisho wa mwaka wa 1995, mapato katika Jumuiya ya Ulaya kutokana na mauzo ya ala za muziki yalikuwa yameongezeka maradufu. Ala hizo zilikuwa ni pamoja na zile zilizotumiwa kurekodia muziki. Katika mwaka huo, mauzo hayo yalikuwa ya kima cha Euro bilioni 2. Kwa jumla, katika mwaka wa 1995, Jumuiya ya Ulaya pekee ilichangia asilimia 30.9 ya jumla ya mauzo yote ya

muziki ulimwenguni kote. Hii ilichangia katika kuongezea kitita cha Euro bilioni 31.25 kwa uchumi wa nchi za Jumuiya hii. Wakati huo, mauzo ya nchi ya Amerika ulimwenguni yalikuwa asilimia 31, Japan asilimia 19 na sehemu nyingine za ulimwengu zilichangia asilimia 22.

Nchini Kenya, muziki umechangia kwa kiasi katika kukuza uchumi wa nchi. Mhandisi Abdulrazaq Adan Ali akihutubia kongamano lililojadili manufaa ya muziki nchini Kenya tarehe 19-12-2011 kule Mombasa, aliweza kuonyesha kiasi cha pesa ambacho shughuli za kimuziki zilichangia katika uchumi wa Kenya. Kufikia mwezi wa Juni mwaka wa 2011, serikali ilikuwa imejipatia takriban shilingi bilioni 2.8 kupitia kwa shughuli mbalimbali za kimuziki. Alisema kuwa pesa hizo zilitokana na ushuru kutoka kwa wanamuziki. Zingine zilitokana na leseni walizopewa wanamuziki katika kuendeleza kazi yao kama vile kufanya maonyesho ya muziki katika sehemu tofauti za nchi. Isitoshe, pesa zingine zilitokana na ushuru uliotolewa baada ya mauzo ya ala za muziki na kutokana na mauzo ya muziki wenyewe. Haya yote yaliweza kuchangia pakubwa katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

### 2.3.2 Muziki na kilimo

Muziki umechangia kwa kiasi kikubwa katika shughuli tofauti za kuboresha maisha ya watu ulimwenguni kote. Moja ya shughuli hizi ni ile ya kilimo. Hii ni shughuli muhimu kwa maisha ya kila siku ya binadamu kiasi kwamba bila kilimo, maisha hayatakuwepo.

Bohlman (2002), anaeleza umuhimu wa muziki katika kuendelezea shughuli za kilimo kule Amerika. Anasema kuwa katika miaka ya 1930 kulipotokea mfumuko wa kiuchumi nchini Amerika, muziki ulitumiwa sana katika kampeni za kuwahamasisha Waamerika kuhusu umuhimu wa kuimarisha kilimo chao katika harakati za kufufua shughuli zao za kiviwanda zilizohusiana na kilimo. Kampeni hizo zilizoendeshwa kupitia muziki zilichangia sana katika kuboresha maisha ya wananchi wengi kando na kuinua mapato yao.

Wakati huo, nyimbo za jadi zilizokuwa zimechezwa kwa mitindo ya zamani zilichezwa upya kwa mitindo mipya ya wakati huo. Nyimbo hizo zilitumika kote Marekani katika shughuli nyingi za kuinua na kuendeleza uchumi, shughuli ya kilimo ikiwa mojawapo. Akiongezea, Bohlman anasema kuwa wakati huo, nyimbo za jadi aidha zilitumiwa katika shughuli za kuimarisha uchumi katika mataifa mengine kama vile Hungary, Romania, Czechoslovakia na Yugoslavia.

Summit (2006), akiandika kuhusu muziki kule Uganda, anaelezea kisa kilichotokea mnamo Septemba 11, mwaka wa 2001. Wakati huo, mkulima mmoja wa kahawa, J. J. Keki, kutoka Uganda, alialikwa Marekani kutoa mhadhara kuhusu “Abayudaya”, jamii yake ya Kiyahudi kule Uganda. Akijiandaa kutoa huo mhadhara, kulitokea shambulizi la kigaidi lililomlazimu kurudi Uganda na kuandaa tamasha ya muziki iliyojulikana kama “Mirembe Kawomera” (“Delicious Peace”). Tamasha hiyo ilihusisha jamii za Kiyahudi, Wakristo na Waislamu waliokuwa majirani kule Uganda. Alipanga tamasha hii kutokana

na imani yake kuwa wakati wa vita na vurugu, watu ni sharti washiriki katika shughuli yoyote ile ya kuhubiri na kuleta amani.

Nchini Uganda, muziki ni sehemu muhimu katika utamaduni na shughuli za kila siku za wananchi. Wakulima wa kahawa nchini humo hutumia muziki katika kujumuika na wenzao na katika shughuli za kuwaendeleza kiuchumi na kijamii licha ya kuwa wanatoka katika imani tofauti za kidini. Kutokana na juhudi za Keki, makundi tofauti ya watu nchini Uganda yalianzisha vikundi vya nyimbo za kuhimiza watu kuishi pamoja na kutangamana kwa amani na maridhiano.

Kutokana na umuhimu unaohusishwa na nyimbo za vikundi hivi kule Uganda, Jeffrey A. Summit, mhadhiri wa muziki katika chuo kikuu cha Tufts kule Marekani, alisafiri hadi Mbale, Uganda na kurekodi nyimbo za amani na maridhiano za vikundi hivyo. Kati ya hizo, alikusanya nyimbo kumi na sita na kuzirekodi katika kanda iliyojulikana kama "*Delicious Peace: Coffee, Music and Interfaith Harmony in Uganda.*" Nyimbo hizo hutumiwa katika kampeni za kuhubiri amani na maridhiano katika sehemu tofauti za ulimwengu ambazo zimewahi kukumbwa na vita na machafuko.

Summit anaelezea kuwa umuhimu mwingine wa nyimbo hizi kando na ule wa kuhubiri amani na maridhiano, ni watu kutia bidii katika shughuli tofauti za kuwanufaisha kiuchumi. Wakulima kule Uganda kupitia nyimbo, wanahimizwa kuhusu njia bora za kundeleza kilimo chao cha kahawa katika kuboresha mapato yao. Mapato wanayoyapata kutokana na kilimo cha kahawa yanawawezesha kuishi maisha mazuri, kupeleka watoto

wao shule nzuri, kununua nguo, kulipia matibabu yao na kutimizia mahitaji yao mengine katika maisha. Anaongezea kuwa muziki huwezesha watu wa misingi tofauti kutangamana na kuishi pamoja licha ya kuwa wanaweza kuwa wa imani tofauti. Kwa mfano, kupitia kikundi cha “Delicious Peace,” watu wengi nchini Uganda wa makabila na imani tofauti za kidini kama vile wa imani ya Kiyahudi, imani ya Kikristo na imani ya Kiislamu wameungana pamoja.

Kiplang’at (2009), anaonyesha namna muziki ulivyokuwa na umuhimu mkubwa katika shughuli za kuendeleza kilimo nchini Kenya. Anasema kuwa makabila mengi yaliyojihusisha na zaraa yalitumia muziki ili kuwahimiza washiriki wafanye kazi kwa bidii. Wakati mwingine, nyimbo hizo zilihusu watu wa jamii waliokuwa na bidii katika kazi zao na wakapata kufaulu maishani licha ya kuwa waliheshimiwa sana katika jamii. Kwa upande mwingine, kulikuwa na nyimbo zilizohusu wale waliokuwa wazembe katika kazi zao na walivyobezwa katika jamii. Anatoa mfano wa jamii ya Wakisii ambayo ilijihusisha sana na shughuli za kilimo. Nyimbo maalum zingeimbwa na jamii hii wakati wa kulima. Zilisifia wale waliokuwa na bidii shambani na kukashifu wazembe walioonekana kuwa wenye hasara kwa jamii. Wazembe wangedharauliwa na wengi katika jamii kiasi cha kutopata mchumba wa ndoa. Wakati wa sherehe tofauti za kijamii, mtu kama huyo alifukuzwa mbali kwa kuwa hakuwa na faida kwa jamii. Kutokana na muziki, wanajamii walitia juhudi katika kazi zao na hivyo kusaidia kuimarisha mapato ya jamii.

### 2.3.3 Muziki na Ajira

Kuna ukosefu wa ajira za kutosha kwa vijana wanaokamilisha masoma yao kutoka taasisi mbalimbali za masomo ulimwenguni kote. Muziki ni shughuli moja ambayo inaweza kutumia na serikali za nchi tofauti ulimwenguni katika kutatua shida hii, taifa la Kenya likiwemo.

Utafiti wa Laing (1996), unaonyesha kuwa kulikuwa na jumla ya watu 600,000 waliokuwa wameajiriwa katika viwanda mbalimbali vya kimuziki katika Jumuiya ya Ulaya. Kati yao, asilimia 75 walikuwa ni vijana. Nafasi za kazi katika jumuiya hii zilipatikana kupitia sekta mbalimbali zilizohusiana na muziki. Mathalan, jumla ya watu 30,000 walipata ajira katika viwanda vya kutengenezea ala za muziki. Sekta ya kurekodi muziki iliyokuwa na takriban kampuni 3,000 za kurekodia sauti na viwanda 85 vya kutengenezea sidi za muziki na maelfu ya studio za kurekodia muziki, ilitoa takriban nafasi 45,000 za ajira.

Laing anaongezea kuwa jumla ya watu 80,000 waliajiriwa katika uchuuzi wa muziki uliokuwa tayari umerekodiwa. Sekta ya maonyesho ya muziki nayo husaidia zaidi ya wanamuziki 100,000 kutoka kwa nchi tofauti za Jumuiya ya Ulaya. Wengi wa hawa ni wale wanamuziki chipukizi wanaotegemea mapato kutoka kwa maonyesho ya muziki katika kujikimu kimaisha. Sekta hii aidha huajiri takriban watu 25,000 wanaofanya kazi mbalimbali saidizi za kufanikisha maonyesho ya muziki kwa njia moja au nyingine.

Isitoshe, wanamuziki wengi hupata pesa nyingi kwa kufunza somo la muziki katika taasisi tofauti za elimu katika Jumuiya ya Ulaya. Takwimu zilizotolewa wakati huo zilionyesha kuwa wananchi wengi kutoka nchi wanachama katika Jumuiya ya Ulaya wanachukua mafunzo ya muziki. Baadhi yao wanajifunza kuwa walimu wa muziki, huku wengine wakijifunza kuwa wasanii wa muziki.

Katika mwaka wa 1995, watunzi wa nyimbo na wachapishaji wa muziki katika Jumuiya ya Ulaya walijiongezea kima cha Euro milioni 750 katika kipato chao. Hela hizi zilitokana na haki za kurekodi nyimbo zao. Katika mwaka huo, wanamuziki walijiongezea kitita cha Euro bilioni 1 kutokana na ada ya kiingilio katika tamasha za maonyesho ya muziki.

Katika kongamano lililofanyika jijini Mombasa tarehe 19 – 12 – 2011 na kuhutubiwa na David Stopps, Mkurugenzi wa shirika la WIPO lenye makao yake makuu kule Geneva, ilitambuliwa kuwa muziki unaweza kutoa ajira kwa vijana wengi wanaomaliza shule. Katika kikao hicho, shughuli mbalimbali kutokana na muziki ambazo zina uwezo wa kuongezea nafasi za kazi zilijadiliwa. Shughuli hizo ni pamoja na uimbaji wenyewe wa muziki, utunzi wa muziki, kushiriki katika maonyesho ya muziki, mauzo ya muziki kwa njia ya moja kwa moja au kupitia mtandao, ada za kiingilio kwenye maonyesho ya muziki, uchapishaji na kurekodi n.k. Kongamano hili lililofadhiliwa na shirika la World Intellectual property Organisation **(**WIPO), lilihudhuriwa na miongoni mwa wengine wengi, Angela Ndambuki, Meneja Mkuu shirika la  Performing Rights Society of Kenya (PRSK), wawakilishi kutoka Music Copyright Society of Kenya (MCSK), Kenya

Copyright Board (KCB) na aliyekuwa katibu wa wizara ya Biashara na Viwanda, Mhandisi Abdulrazaq Adan Ali.

### 2.4 Nyimbo katika siasa

Siasa ni itikadi inayofuatwa na kundi au jamii fulani ambayo ni msingi wa kuendesha uchumi, utamaduni na mwenendo mzima wa maisha ya jamii hiyo (TUKI, 2004). Ulimwenguni kote siasa ni sehemu muhimu ya maisha ya wanajamaii. Kutokana na mfumo wa kisiasa, sera za kimaendeleo huundwa na kutekelezwa pamoja na kulinda haki za wananchi. Licha ya kuwepo kwa umuhimu wa siasa katika jamii, taasisi mbalimbali za kisiasa zimekuwa na athari chanya na athari hasi sawia kwa wanajamii kutegemea jinsi viongozi wa kisiasa wanavyowajibikia majukumu yao pamoja na sera zilizomo zinavyotekelezwa. Kwa mfano, katika karne za kumi na saba na kumi na nane baadhi ya mataifa ya ulaya yalitawaliwa na wafalme ambao walikuwa na mamlaka juu ya wananchi. Mamlaka yao yaliaminika kutoka kwa Mungu. Barani Afrika, nchini Kenya kwa mfano, kila jamii ilikuwa na kiongozi wake ambaye alikuwa na mamlaka juu ya jamii aliyoitawala ila hakukuwa na siasa za kitaifa. Kufikia mwishoni mwa karne ya kumi na nane na mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa, bara la afrika lilijipata chini ya wakoloni wa kigeni ambao walichochea hisia za kisiasa miongoni mwa Waafrika na kusababisha vita vya kupigania uhuru ambao ulipatikana katika awamu mbalimbali kwa mataifa tofauti tofauti ya kiafrika. Nchi ya Kenya ilijinyakulia uhuru wake kutoka kwa wakoloni wa uingereza mnamo mwaka wa 1963. Licha ya kuwepo manufaa yaliyotokana na watawala wa kikoloni, wenyeji walighadhabishwa na hali za kukandamizwa na mali yao kunyakuliwa.

Licha ya kuwa nyimbo zenye maudhui ya kisiasa zilikuwemo tangu zamani, awali zikiwa za kusifia viongozi na mashujaa wa jamii, baada ya maajilio ya wakoloni maudhui ya nyimbo hizi yalipata sura mpya. Nyimbo zilianza kusheheni maudhui ya kimapinduzi. Viongozi wa kupigania uhuru waliweza kutumia nyimbo kuhamasisha jamii dhidi ya utawala wa kikoloni.

Tukiangazia nyimbo na siasa barani Afrika, inabainika kuwa nyimbo zimetumika kwa namna chanya na vilevile kwa namna hasi kisiasa.

### 2.4.1 Athari chanya za muziki katika siasa

Muziki barani Afrika uliweza kutumiwa kupigania ukombozi kutoka kwa utawala wa kikoloni. Kwa mfano, nchini Afrika Kusini, ambapo kulikuwa na mfumo wa ubaguzi wa rangi uliodumu kwa miaka 46, nyimbo zilitekeleza jukumu muhimu katika kuhamasisha uzalendo na haja ya kujikomboa. Olwage (2008), anaeleza kuwa, licha ya kuwa utafiti katika swala la muziki na ukombozi nchini Afrika Kusini umejikita katika nyimbo zilizotumiwa na vuguvugu la kimapinduzi, kuna nyimbo zilizotungwa na kuimbwa mashinani ambazo hazijapata kutaliliwa kutokana na wingi wake na ukosefu wa urasmi wa kiutunzi. Hata hivyo, anatambua kwamba nyimbo, iwe zilizotumiwa na vyama vya kisiasa au zilizotumiwa na waliokuwa uhamishoni, zilichangia pakubwa kuwahamasisha watu na kupinga mfumo huu wa kiutawala. Kwa mfano, mwanamuziki Lucky Dube wa mtindo wa Reggae alitunga nyimbo zilizohimiza haja ya watu nchini Afrika Kusini kusita kutengana kwa misingi ya rangi ya ngozi na badala yake kuungana na kuwa kitu kimoja.

Akichangia muziki kisiasa, Kiplang'at (2009), anasema kuwa muziki unatumika katika kupinga ukandamizwaji na uonevu katika jamii. Jambo hili lilidhihirika wakati wa ukoloni ambapo Mwafrika alitumia muziki kama silaha kupigania uhuru. Muziki ulitumiwa kuwahimiza watu wapinge tamaduni za wakandamizaji. Waafrika walifanya hivi na kuchukuwa nyimbo za kisiasa na kuzipa mahadhi ya kidini ambapo kwa hakika maana ilikuwa tofauti na ile ya kidini. Hivi sasa wanamuziki wa nyimbo pendwa wanaimba nyimbo zinazowaelimisha na kuwahamasisha watu ili watekeleze kwa ufanisi sera na maagizo mbalimbali ya chama kinachotawala na serikali kwa ujumla.

Makky (2007), anaeleza kuwa licha ya vikwazo vilivyokuwepo, makabila mbalimbali Afrika Kusini yalitumia nyimbo katika kupinga udhalimu ulioendelezwa na makaburu. Anatoa sehemu ya wimbo uliotumiwa kutekeleza jukumu hilo:

*Let's unite, let's unite*
*Let's unite fellow Africans*
*Down with infighting*
*Up with peace (Pollard 122).*
(Hebu tuungane, hebu tuungane,
Hebu tuungane Waafrika wenzangu
Tuache mizozo baina yetu
Tudumishe amani).**Ty**

Wimbo huu uliwahimiza Waafrika waungane licha ya kuwa makaburu walitumia kila hila na njama ya kuwatenganisha ndio wasifanikiwe katika kujipanga ili wakabaliane nao. Makky anasema kuwa kulikuwa na nyimbo nyingi zilizotumiwa na Waafrika katika vita dhidi ya wazungu. Baadhi ya nyimbo hizo ni wimbo wa *Senseni Na* na *Meadowlands*.

Hasa ule wimbo wa *Senseni Na* ulikuwa na lugha fiche iliyoeleweka na Waafrika pekee na ilikuwa na matusi kwa makaburu. Wimbo huo ulisema:

| | |
|---|---|
| Senseni na Senseni na? | (Tumefanya nini, Tumefanya nini? |
| Senseni na Senseni na? | Tumefanya nini, Tumefanya nini? |
| Senseni na Senseni na? | Tumefanya nini, Tumefanya nini? |
| Senseni na kulomhlaba? | Tumefanya nini katika nchi yetu? |
| Amabhulu azizinja | Makaburu ni mbwa |
| Amabhulu azizinja | Makaburu ni mbwa |
| Amabhulu azizinja | Makaburu ni mbwa |
| Amabhulu azizinja | Makaburu ni mbwa |
| Kuyisono ‘kubamnyama | Ni kosa kuwa mweusi |
| Kuyisono ‘kubamnyama | Ni kosa kuwa mweusi |
| Kuyisono ‘kubamnyama | Ni kosa kuwa mweusi |
| Kuyisono kulelizwe. | Ni kosa katika nchi hii) (Pollard 113) **Ty** |

Makky anasema kuwa wimbo huu pamoja na nyingine zilisaidia sana katika kuwaunganisha Waafika katika kupigania ukombozi wao.

Nchini Kenya, tunaweza kuugawa muziki katika makundi mawili makuu: miziki ya kidini na ile isiyo ya kidini. Kama anayoelezea Parsitau (2006) nyimbo za kidini nchini Kenya zinatekeleza dhima ya kijamii na kisiasa kwa wakati huo huo. Nyimbo hizi nchini Kenya zimeshamiri kwanzia mwanzoni mwa karne ya ishirini na moja na maudhui yake yanatanda kote kwanzia kuhamasisha, kuonya, kuelekeza na hata kuhimiza wanajamaii.

Katika miaka ya hapo awali (1978-2002), wakati wa utawala wa Daniel Arap Moi, nyimbo nchini Kenya zilitumiwa sanasana kuhimiza na kuendeleza uzalendo kando na kuuza sera za serikali. Miungano ya kwaya mbalimbali iliwatumbuiza wananchi katika hafla mbalimbali za kitaifa kwa nyimbo zilizosifia uongozi wa serikali ya wakati huo pamoja na kuhimiza uzalendo.

Baada ya majilio ya mfumo wa kisisasa wa vyama vingi, nyimbo zilipata dhima tofauti nchini Kenya huku zikitumiwa kwa uamilifu tofauti ambapo serikali ilizitumia kuhimiza uzalendo na kueneza sera zake huku makundi yaliyopigania siasa ya vyama vingi yakitumia nyimbo hizi kupinga serikali ya wakati huo pamoja na kuwahimiza wananchi kuhusu haja ya kubadili mfumo wa kiutawala uliokuwepo.

Matumizi ya nyimbo katika kuendesha kampeni za kisiasa nchini Kenya leo hii yameshamiri mno. Kwa mfano, katika uchaguzi wa mwaka wa 2002 ulioondoa uongozi wa chama cha KANU, muungano wa *Rainbow Alliance* ulitumia wimbo maarufu wakati

ule wa Gidi Gidi Maji Maji ulioitwa *Unbwogable* wenye maana ya kwamba hawatikisiki au kutishika.

### 2.4.2 Athari hasi za muziki katika siasa

Kuwepo kwa vituo vinavyopeperusha matangazo kwa lugha za kiasili nchini Kenya kumeibua hatari ya kugawika kwa jamii katika misingi ya kikabila. Idhaa hizi hucheza miziki mingi iliyotungwa kwa lugha mbalimbali za kiasili za humu nchini. Kama shirika la Peacenet – Kenya (2010) linavyoeleza, muziki una nguvu nyingi na uwezo mkubwa wa kuathiri vikundi mbalimbali katika jamii hususan vijana. Hali hii inatokana na kuongezeka kwa hali ngumu za kiuchumi ambazo zinafanya hali ya kulaumiana kuwa rahisi sana. Miziki iliyosheheni jumbe zenye matamshi ya chuki dhidi ya jamii fulani sawia na kuendeleza imani potofu kuhusu jamii tofauti tofauti zinaweza kuchangia kuvunjika kwa amani katika jamii.

Nchini Kenya, nyimbo zimetumiwa kueneza hisia za chuki dhidi ya kundi, mtu au hata jamii fulani. Kwa mfano, mnamo mwaka wa 2012, wasanii watatu kutoka jamii ya Wakikuyu walishtakiwa mahakamani kwa tuhuma za kuchochea uhasama baina ya jamii za Wajaluo na Wakikuyu. Hii ilikuwa ni kabla ya uchaguzi mkuu uliofanyika mnamo Machi 2013. Baadhi ya miziki, kama ule wa msanii Kamande wa Kioi, *Uhuru ni witu* (Uhuru ni wetu) ulisheheni matamshi yaliyosifia jamii ya Wakikuyu na kiongozi kutoka jamii hii, Uhuru Kenyatta, huku ukimsuta kiongozi kutoka jamii ya Wajaluo, Raila Odinga, na kuhimiza kuwa hafai kuchaguliwa rais kwa vile "hajatahiri". Kasumba kama hizi wakati mwingi huchochea hisia kali za kisiasa ambazo zisipodhibitiwa huenda

zikasababisha uhasama wa kikabila na hata vita vya wenyewe kwa wenyewe baina ya makundi yaliyoathirika.

Nyimbo nchini Kenya vilevile zimewahi kutumika kwa namna hasi kisiasa. Kwa mfano, katika enzi ya mfumo wa siasa za chama kimoja, nyimbo zilitumiwa kuwafanya watu kusifia sera na uongozi ambao uliwakandamiza na kuwanyanyasa kwa wakati huo. Kasumba za kuwa kiongozi wa wakati huo alikuwa bora na kwamba hangepingwa zilienezwa kupitia kwa muziki kwa vizazi vyote nchini kuanzia watoto hadi watu wazima.

Ingawa kumekuwepo vipindi na hali ambapo muziki umetumiwa kwa namna hasi kisiasa, ukweli ni kwamba muziki, na lugha inayotumika katika kuitunga, ni silaha ambayo ina uwezo wa kukata pande zote mbili. Hivyo basi, ni muhimu kwa wasanii kuamua na kuhimiza matumizi ya lugha kwa namna inayoibua utangamano na kuhimiza umoja na amani baina ya wanajamii. Katika kufanya hivyo, wanamuziki hawa hutumia lugha kwa namna za kipekee na ndio maana tasnifu hii iliazimia kubainisha mitindo hii ya kipekee katika uteuzi na matumizi ya lugha ya amani na maridhiano nchini Kenya.

**2.5 Uamilifu wa muziki kijamii**

Muziki kama utanzu wa fasihi una majukumu mbalimbali ambayo huyatekeleza katika jamii. Lengo kuu la fasihi ni lile la kuelimisha na hata kuburudisha jamii. Ndivyo ilivyo katika muziki kwa sababu kupitia kwake, wanajamii huburudika na kuelimishwa. Muziki ni utanzu ambao huwafikia watu wengi katika jamii. Kutokana na kutumia lugha ya

Kiswahili na zile zinazotumiwa na jamii ambamo unaimbwa, utanzu huu unaweza kueleweka na watu wengi katika jamii. Muziki huendeleza mahusiano ya kijamii ambayo hujengwa kutokana na historia, mazingira na shughuli za watu za kila siku pamoja na imani yao. Watu wa jamii moja mara nyingi husikilizana kwa lugha, mila na desturi. Misingi hiyo ya utamaduni na utamaduni wenyewe huwa ni vigezo maalum vya kumfanya mtu aitambue nafasi yake katika jamii na vile vile wajibu wake na majukumu yake.

### 2.5.1 Athari chanya za muziki kijamii

Muziki ni sehemu ya utamaduni wa jamii yoyote ile na hutekeleza majukumu mbalimbali katika jamii (Ngugi, 2000). Matumizi ya muziki yanaweza yakawa na athari ama chanya au hasi katika jamii kiutamaduni, kimila na hata kiitikadi. Kihistoria, miziki ya kiafrika iliathiriwa na mitindo ya kimuziki ya magharibi. Athari hizi ni katika ngazi ya midundo, ala za muziki zinazotumiwa na hata mavazi ya wasanii husika kwa ujumla. Miziki ya kiafrika leo hii imepata mahadhi na midundo ambayo ni ya kimagharibi zaidi. Kwa mfano, nyimbo za kitamaduni katika jamii mbalimbali nchini, kama vile Kikuyu na Kijaluo, zimesheheni midundo ya “pop” ambao ni muziki wenye asili ya kimagharibi. Vijana wa kizazi hiki nao wamechukua mitindo ya muziki wa aina ya “Hip hop” wenye asili ya Kimarekani pamoja na mtindo wa “Reggae” wenye asili ya Kijamaika.

Muziki umekuwa chombo ambacho kimewavutia binadamu. Jambo hili limewafanya watu wa matabaka mbalimbali wakiwemo wanafalsafa na watu wa kawaida kujaribu

kuelewa muziki – lakini hakuna fasihi ambayo imeweza kueleza muziki ni nini hasa: uasili wake haujulikani kama anavyodai Schuman katika Kofie (1994) kuwa:

> Sayansi hutumia hisibati na umantiki, ushairi nao hutumia maneno teule… muziki ni yatima ambaye babake na mamake hawajulikani kamwe. Hata hivyo, ni utata huu wa uasili wake ambao umefanya muziki uonekane kuwa kitu bora zaidi katika jamii. (**T.y**).

Kwa kutumia nyimbo, waimbaji wameweza kuhifadhi historia na utamaduni wa jamii zao. Uchunguzi uliofanywa juu ya muziki umeonyesha kuwa nyimbo ni kipengele muhimu sana katika jamii zote ulimwenguni. Muziki ni utanzu uliothaminiwa sana, na ulitawala katika mifumo yote ya jamii (Bandel, 1995). Akuno (1999), anasema kuwa muziki ni zaidi ya sauti tu ambazo huimbwa na kuchezwa. Muziki sio wazo la dhana fulani bali ni tajriba, ni tukio ambalo huwasilisha mambo mbalimbali yenye umuhimu wa jamii husika. Akuno anaona muziki ukiwa na uamali wa kiujozi: Kwanza kama kiburudisho, muziki huendeleza uhusiano wa mtu binafsi, humstarehesha na kumwezesha mtu huyo kuwasilisha hisia zake. Na kama tambiko, muziki huendeleza uhusiano wa kimazingira – kwa kuwahusisha wanadamu na viumbe vingine vinavyopatikana katika mazingira hayo.

Katika kuangalia upande wa kijamii, Akuno anaona muziki kama chombo ambacho hutumiwa kueleza historia ya jamii, hutumiwa kupasha ujumbe maalum kwa wanajamii hasa kizazi kimoja hadi kingine na hutumiwa hasa kuelezea historia, imani, itikadi na kaida za jamii. Nyimbo ni zao la mazingira ya jamii. Zinaweza kufananishwa na mtoto ambaye hufinyangwa na mambo mengi katika historia ya jamii yake. Hii ina maana kwamba muziki hauibuki katika ombwe tupu na hauwezi vilevile kujiundia mazingira yasiyo halisi. Nyimbo huathiriwa sana na mambo yanayotendeka ulimwenguni.

Chachage (2004), akionyesha umuhimu wa muziki kijamii kule Tanzania, anasema kuwa dhima ya asasi za kitamaduni ukiwemo muziki kwa ujumla ilikuwa imelenga katika kuwaamsha wananchi kwa ujumla kushiriki katika maendeleo, kujenga ujamaa na kupigania ukombozi wa Afrika. Na kutokana na mkabala huu, Redio Tanzania Dar es Salaam, ambayo ndiyo ilikuwa redio ya pekee, ilikuwa ikirekodi na kutangaza muziki uliokubalika kimaadili – ikiwa ni pamoja na *Taarab* (ambayo asili yake ni Mashariki ya Kati) na ngoma za asili. Kwa ujumla, kulikuwa na uhodhi wa vyombo vya utamaduni, ambao ulipelekea kuzuia na kupiga marufuku kile kilichoonekana kwamba kinaenda kinyume na maadili ya kiafrika.

Chachage (ibid), akiandika kuhusu vijana na migongano ya mitazamo kuhusu demokrasia anasema kuwa utamaduni wa sasa wa vijana ni ule wa kutoficha kitu. Wanaimba na kuongea wazi juu ya matatizo yanayowakabili, wanafanya utani na kudhihakiana na wakati huo huo wakisisitiza upendo na kupendana. Kadhalika, wanashirikiana , wasichana kwa wavulana katika *R & B* na *Hip Hop* na yote kwao ni *Bongo Flava.*Wao tangu mwaka wa 1995 walishatamka kwamba “Vijana ni taifa la Leo!” wakimaanisha kwamba wao ndio wengi zaidi na inabidi haki zao zizingatiwe. Ulikuwa ni utambuzi kwamba wazee walikuwa wameyahaini matamanio na mategemeo yao. Wakati wa uchaguzi wa mwaka wa 2000 nchini Tanzania, kwa mfano, kuna wimbo uliopigwa na Olduvai Gorge ukihimiza suala la uchaguzi. Wimbo huu haukudumu katika vyombo vya habari, kwani ulibainisha wazi unafiki na uongo wa baadhi ya wagombea, na ukawataka

watu wawakatae. Katika kibwagizo chake, vijana walifoka: “Wabunge hawa Bwana! Kura tumewapa! Bungeni Wamekwenda! Lakini, Laa! Balaa, Wanasinzia...”

Kama hilo halikutosha, Chachage anaonyesha namna vijana walizidi kuchakura baada ya hapo. Baadhi ya nyimbo zao zimekuwa maarufu katika kukabiliana na shida za kijamii. Anatoa mfano wa nyimbo kama zile za Unique Sisters wakiwaasa wenzao kuhusu janga ka UKIMWI. Wagosi wa Kaya kutoka Tanga nao waliimba kuhusu UKIMWI na matatizo yake (*Nitamtambuaje?*), matatizo ya wakulima na ukosefu wa masoko ya haki (*Wakulima*).

Nchini Malawi, mchango wa muziki katika vita dhidi ya UKIMWI ulidhihirika kupitia juhudi za msanii Saleta Phiri kupitia muziki wake. Yeye aliimba wimbo *‘Ili mu ufa’* (Upo katika unga wa kupikia). Unga wa mahindi nchini Malawi unatumiwa kuandalia ugali ambao ni chakula muhimu cha kila siku kwa Wamalawi. Nchini mle, iliaminika kuwa mtu asipokula ugali atakuwa na njaa. Mwanamuziki huyu alifananisha hali hii na kitendo cha ngono kilichofurahiwa na wengi. Basi, alinuia kuwafahamisha kuwa ugonjwa hatari ulikuwa umeingia katika ule ‘unga’ walioupenda sana.

Umuhimu mwingine wa muziki ulitokana na utafiti uliofanywa nchini Uganda na Konde-Lule (1993), ulionuiwa kubaini njia zilizotumiwa na umma ili kujifahamisha habari kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Iligunduliwa kuwa kando na njia za kutumia vipindi redioni, habari kutoka kwa marafiki au watu wa jamii moja, magazeti na vilabu vya uigizaji shuleni, muziki nao ulikuwa njia mojawapo muhimu iliyotumiwa katika kusambaza habari kuhusu ugonjwa huu. Mtafiti huyu aligundua kuwa wananchi wengi

walipenda kusikiza muziki wakiendelea na shughuli zao za kikazi. Wengine nao hawakuwa na hiari ya kutousikiza ulipochezwa. Kupitia njia hii, habari kuhusu VVU/UKIMWI zilienezwa kwa urahisi miongoni mwa wananchi, jambo lililochangia kupunguza maenezi ya ugonjwa huo nchini humo.

Nchini Kenya, jamii tofauti zilitumia muziki kwa namna mbalimbali wakati wa sherehe ainati katika jamii. Kiplang'at (2009), anahoji kuwa miongoni mwa Mijikenda, nyimbo zilitumiwa wakati wa sherehe kama vile ndoa na kutahiri. Baada ya sherehe ya kutahiri kwa mfano, nyimbo maalum ziliimbwa baada ya siku saba. Wakati wa mazishi, waombolezaji waliimba nyimbo ambazo zililenga kuwafanya watu wafurahi na wasahau masaibu yao. Katika sherehe hiyo, aina maalum ya densi iliyojulikana kama *msego* ilichezwa. Densi hiyo ilichezwa bila kuhusisha kupiga ngoma. Aidha, densi iliyojulikana kama *mabumbumbu* ilichezwa katika sherehe ya kutakasa boma. Densi ya aina hii ilihusu mambo mengi ya kisarakasi.

Miongoni mwa jamii ya Maa, nyimbo zilitumiwa kwa sherehe fulani maalum za kijamii. Maarufu miongoni mwa hizi ni wimbo uliojulikana kama *Engilanikoto*, wimbo wa kimasai wa kusheherekea ufanisi baada ya kuwinda simba. Wimbo huu uliimbwa na kiongozi wa kundi huku wengine wakiitikia kwa mahadhi ya kipekee wakiruka kwa nguvu juu hewani.

Jamii ya Waluo nayo ilitumia muziki katika sherehe nyingi za kijamii. Wao walikuwa na muziki uliosifika wakati wa sherehe ulioitwa *thum*. Lilikuwa ni jambo ka shuruti kucheza

wimbo huu katika sherehe nyingi za Waluo. Sherehe hizo ni kama zile za ndoa, mazishi na sherehe zingine za kufanya matambiko. Isitoshe, muziki ulitumiwa kwa kuwatumbuiza viongozi na wageni katika jamii na katika kusherekea mavuno mazuri waliyoyapata. Wanajamii walienzi sana *thum* na ilibidi kila mwanajamii ashiriki katika kuicheza. Kwa kufanya hivyo, waliamini kuwa walikuwa wameungana kama jamii katika kuulinda na kuutunza utamaduni wao (Omondi, 1983).

Akizungumzia muziki kijamii nchini Kenya, Ngugi (2000), anahoji kuwa umuhimu wake unadhihirika katika matumizi ya nyimbo katika wakati maalum kama njia mojawapo ya kuanzisha mabadiliko ya tabia za jamii au mtu binafsi. Anaongezea kuwa muziki umetumika kama njia mojawapo ya kufundishia utamaduni na aghalabu hutumiwa katika kuelezea mtu mazingira yake na jinsi anavyoweza kuyatumia na kuyatunza vilivyo. Isitoshe, Ngugi anasema kuwa nyimbo zimekuja kuchukuliwa kama chanzo cha elimu na jinsi ya kujieleza katika jamii na hasa katika sanaa ya mazungumzo. Nyimbo humfanya mtu ajenge kumbukumbu ya vitu au tukio kwa urahisi na kumbukumbu hiyo huweza kudumu kwa muda mrefu. Kwa mfano, masomo shuleni hufanikishwa kupitia nyimbo.

Sanaa ya uimbaji inaonyesha uwezo wa binadamu wa kusimulia au kupasha tajriba yake na ya jamii ya kila siku na kujaribu kuleta maana katika maisha ya kila siku. Mambo haya hufanyika kwa njia ya ukawaida mno – kupitia kwenye nyimbo pendwa. Nyimbo hizi huweza hata kuundwa upya na wananchi wenyewe kwa sababu mbalimbali (Makky, 2007).

Kama asemavyo Ngugi (2000), nyimbo zimeundwa kama sanaa nyingine ili kunasa makini yetu. Sanaa hii basi ina ukale, uleo na ukesho. Kupitia nyimbo pendwa, wanamuziki wa Kiswahili wanaweza kuangalia 'usasa' au dunia ya leo. Hapo baadaye, 'usasa' huu utakuwa kama ukale utakaotuelekeza kufahamu historia yetu ya wakati huo. 'Usasa' huu unaweza kutusaidia katika kutabiri "ukesho" wetu na kujua namna ya kukabiliana na ulimwengu ujao.

Muziki ni sanaa ambayo huwafikia watu wengi kupitia vyombo vya habari kama vile redio na televisheni. Nchini Kenya, vyombo hivi hasa redio, vimeupa muziki nafasi kubwa sana na hivyo kuipanua hadhira yake. Hii ni kutokana na sababu kuwa muziki unathaminiwa sana na wengi katika jamii. Nyimbo nyingi zinazosikika redioni zinahusu kuwahimiza watu kuwa na uwajibikaji, kilimo cha kisasa, uzazi wenye mpango, vita dhidi ya UKIMWI, kuchagua viongozi bora, kufanya kazi kwa bidii ushauri kuhusu maisha, n.k. Kutokana na umuhimu huu, Ngugi (2000), anasema kuwa vyombo vya habari vimetenga masaa kadhaa ya kuwaburudisha watu kwa kutumia nyimbo mbalimbali.

Nyimbo za kisasa zinaweza kutupa mwongozo kuhusu maisha ya watu duniani. Finnegan (1970), anasema kuwa nyimbo pendwa zina majukumu mbalimbali ya kutekeleza hasa katika kuangalia mitazamo ya jamii kiulimwengu, na nyimbo hizi hutekeleza majukumu haya kama zilivyo nyimbo za kijadi. Mtazamo huu umeungwa mkono na watu kama vile Kabira na Mutahi (1998) na Agovi (1989), ambao wanaona muziki kuwa utanzu teule unaodhihirika katika jamii hii inayobadilika. Nyimbo pendwa zimechukuliwa na wasomi

wengi kuwa kama mwingiliano wa masimulizi ya jadi na ukweli wa maisha ya hivi sasa. Nyimbo hizi hushughulikia mambo kama vile ukandamizwaji, kutamauka maishani, unyimwaji wa haki, umaskini, ubinafsi na kadhalika. Mambo haya ni ya kisasa na huathiri wanajamii kwa njia mbalimbali.

Sekella (1995), anasema kuwa wanamuziki hushughulikia nyanja tofauti za maisha kama vile dini, uchumi na siasa. Kwa mfano, wao wanashughulikia ndoa na mapenzi kwa kuonyesha mahusiano ya jamii na migogoro ya kimawazo baina wa wazee na vijana au baina ya mke na mume. Katika nyakati hizi za mabadiliko katika uchumi na siasa, waimbaji wamekuwa wakitunga nyimbo kwa kutuchorea picha ya jinsi mambo yalivyo. Wamekuwa katika mstari wa mbele kuwatahadharisha wanajamii kuhusu ugonjwa wa UKIMWI.

Chachage (2004), akizungumzia muziki kijamii anasema kuwa muziki pendwa katika Kiswahili ni sanaa isiyokuwa na ukabila. Ni sanaa ambayo huwaunganisha watu wa makabila mbalimbali kwa kutumia lugha inayoeleweka na kuzungumzia tajriba sawa wanazozifahamu. Nyimbo hizi pia zimetumika kuimulika jamii kwa kuonyesha maendeleo yaliyopatikana katika nyanja mbalimbali. Anapoikosoa jamii, mwimbaji huwa anachukua jukumu la kuhakiki jamii na hata kuielekeza. Nyimbo hizi pia zinatumiwa kuwazindua watu waweze kufahamu haki zao hasa pale wanaponyimwa, zinatumiwa kama ajenti wa ukombozi.

Hata hivyo, waimbaji wa nyimbo pendwa wamekumbana na vizingiti vingi. Kutokana na sababu kuwa wao ni wahakiki wa jamii, baadhi ya nyimbo zao zimepigwa marufuku

(Mwangi, 1992), na hivyo basi haziwafikii watu wengi waliolengwa na haziwezi kutumiwa kama njia ya kuwazindua watu. Katika kule kuhakiki jamii, wao hulenga kuikosoa, lakini mara nyingi wao huwa hawaafikiani na viongozi kuhusiana na maongozi yao.

### 2.5.2 Athari hasi za muziki kijamii

Licha ya kuwa maudhui ya nyimbo hizi yana uzito na yanashughulikia maswala ya kimsingi na muhimu katika jamii, kuna baadhi ya watu ambao wanahisi kuwa kuiga mitindo ya kigeni kunahatarisha utamaduni asilia wa kiafrika. Kama anavyohoji Chachage (2004), katika kuzungumzia muziki wa kizazi kipya nchini Tanzania, kuna wale wanaohisi kuwa muziki ule unatishia utamaduni wa wenyeji. Hata hivyo, kuathiriana kwa mitindo ya kimuziki ya mataifa na jamii tofauti tofauti ni jambo lisiloepukika hususan katika enzi hii ya utandawazi. Ingawa hivyo, baadhi ya athari hizi zinatishia hali ya kijamii na tamaduni za jamii za kiafrika. Kwa mfano, nyimbo nyingi, hasa za vijana, husheheni matumizi ya lugha ambayo awali haingetumika hadharani na kuzungumzia mada ambazo zilikuwa mwiko kitamaduni kujadiliwa kwa uwazi. Kwa mfano, maswala ya mapenzi na ngono yanatamalaki miziki mingi hasa ile ya mtindo wa “Genge” nchini Kenya. Licha ya kuwa wasanii wanatumia misimbo inayoficha aibu, kama vile matumizi ya Sheng’, bado mada wanazozishughulikia hazifungamani na utamaduni asilia wa kiafrika. Aidha, kumeibuka hali ambapo mavazi yanayovaliwa na wanamuziki, hasa wale wa kike yanatishia maadili ya kiafrika na yanamdhalilisha mwanamke.

## 2.6 Hitimisho

Sura hii imeonyesha namna muziki ulivyo na umuhimi wa kisiasa, kiuchumi na kijamii katika maisha ya watu katika jamii. Hasa umuhimu wa muziki kijamii umeonyesha namna muziki ulivyo na uwezo mkubwa kwa njia chanya au hasi katika kuathiri mahusiano mbalimbali ya wanajamii. Ni katika misingi hii ambapo tasnifu hii ililenga kubainisha matumizi ya lugha katika kuwasilisha ujumbe wa amani na maridhiano katika muziki nchini Kenya.

# SURA YA TATU

# LUGHA KATIKA MUZIKI WA AMANI NA MARIDHIANO

## 3.0 Utangulizi

Mojawapo ya malengo ya utafiti huu ni kupambanua matumizi ya kipekee ya lugha katika ubunaji wa wanamuziki kwa kuzingatia maneno, vishazi na sentensi. Matumizi ya lugha ya amani na maridhiano yamerejelewa kutokana na umuhimu wake katika kuwaunganisha Wakenya kutokana na hali ambapo visa vingi vya kuvurugwa kwa amani vilishuhudiwa nchini katika nyakati tofauti tangu nchi ya Kenya ilipojinyakulia uhuru wake. Tasnifu hii imejishughulisha zaidi na kuchanganua uteuzi wa msamiati, vishazi na sentensi katika miziki teule. Katika kufanya hivi, uchanganuzi wenyewe umehusishwa na nadharia ya majukumu ya lugha kwa kutambua kuwa, mojawapo wa masuala yanayoongoza uteuzi katika lugha ni uamilifu wa matini husika. Aidha, uhusiano wa maneno unaoongoza uteuzi wa msamiati miongoni mwa wasanii kwa kuzingatia mawazo ya Saussure (1916), kuhusu uhusiano mlalo na uhusiano wima wa maneno katika lugha umechunguzwa. Vilevile, suala la muktadha na jinsi linavyoathiri uteuzi katika lugha limeangaziwa.

### 3.1 Matini za uchanganuzi

Sababu za kuchagua matini hizi imeelezwa katika sura ya kwanza. Matini za utafiti zimegawanywa katika makundi matano kulingana na miaka zilipotolewa na hatimaye uchanganuzi wao umefanywa kulingana na ujumbe unaowasilishwa na kila matini. Matini hizo zimewasilishwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali: 1Wasanii wa muziki wa amani na maridhiano 2008-2012**

| MSANII | WIMBO | MWAKA |
|---|---|---|
| 1. Dogo Biggie | Amani Tunataka | 2008 |
| 2. Brasso | Wakenya Tumeamua | 2008 |
| 3. Jimw@t | Stand Up | 2008 |
| 4. Skool Fizz | Kenya ni Yetu | 2008 |
| 5. Eric Wainaina | Daima mimi ni Mkenya | 2008 |
| 6. Joey | Mwanzo Mpya | 2009 |
| 7. Masai Worriors | Kenya Moja | 2009 |
| 8. Naxis | Kenya ni Yetu | 2009 |
| 9. Jublak | Spoken Word | 2009 |
| 10. DJ Parexy | Amani Kenya | 2010 |
| 11. Juliani | Kenya Yetu | 2010 |
| 12. Rhumba Success | Amani Kenya | 2010 |
| 13. Millenium Band | Amani Kenya | 2011 |
| 14. Jua Cali | Kenya we Pray | 2011 |
| 15. Kachela | Amani Tunataka | 2012 |
| 16. Skippa Mistari | Mkenya Daima | 2012 |
| 17. Rabbit | Uhuru | 2012 |
| 18. Aram Ara | Ukabila | 2012 |
| 19. Eric Omondi | Raundi hii | 2012 |
| 20. Zak Mtumishi | Sitaki Noma | 2012 |

## 3.2 Muktadha

Dhana ya muktadha ni tata na imeweza kushughulikiwa kwa namna mbalimbali na watalamu tofauti tofauti. Kwa mfano, Massamba (2004), anafafanua muktadha kuwa ni mazingira ambayo kipengele fulani cha kisarufi hujikuta ndani mwake na kikaathirika nayo ama kichanya au kihasi. Mawazo haya yanahusiana kwa karibu na kile Halliday (1978), anakirejelea kuwa muktadha wa kiisimu. Katika mazingira haya ya muktadha wa kiisimu, neno hufasiriwa na kupata maana kwa kulihusisha na maneno mengine yanayotokea katika mazingira jirani nalo. Kwa mujibu wa Bateson (1972), neno ni muktadha wa fonimu lakini neno lipo tu na hupata maana katika muktadha wa usemi na linapata maana tu katika uhusiano na maneno mengine. Halliday pia anatambua kuwepo kwa aina nyingine mbili za muktadha, muktadha wa hali na muktadha wa kijamii.

Fafanuzi hizi za dhana ya muktadha zinaweza kugawika katika ngazi mbili kuu, muktadha katika misingi ya kiisimu na muktadha katika msingi wa ulimwengu ulioko nje ya isimu, muktadha wa hali na muktadha wa kijamii. Katika sura hii, tunatambua dhima ya muktadha katika kuongoza uteuzi wa msamiati, vishazi na hata sentensi. Tumeugawa muktadha na kuushughulikia katika ngazi tatu kuu; muktadha wa kiisimu, muktadha wa hali na muktadha wa kijamii.

### 3.2.1 Muktadha wa kiisimu

Hii ni dhana inayorejelea mazingira yanayokizunguka kipashio fulani cha lugha (TUKI 1990). Kimsingi muktadha huu unahusiana na mazingira ndani ya matini yenyewe pasi na kuzingatia ulimwengu wa nje, usio wa kiisimu, unaozunguka matini husika. Katika kuunda tungo, sentensi ni muktadha wa neno huku aya ikiwa muktadha wa sentensi.

Yaani, neno kiisimu linapata ufasiri kwa kuzingatia matumizi yake katika sentensi huku sentensi ikifasiriwa kwa kuihusisha na aya ilimotumiwa. Muktadha huu wa kiisimu una uhusiano wa karibu na mgao wa Saussure (1916), wa jinsi maneno yanavyohusiana kimlalo na kiwima. Anaubainisha uhusiano mlalo kuwa ni ule uliopo baina ya kipashio katika sentensi na maneno mengine yaliyopo. Huku uhusiano wima wa maneno akiutambulisha kuwa uhusiano uliopo baina ya elementi ya kiisimu na nyingine ambazo zinaweza kuchukua nafasi yake katika muundo wa tungo. Aghalabu uhusiano wima hujumuisha matumizi ya visawe, vinyume na hiponimia miongoni mwa mengine. Visawe kwa mujibu wa kamusi ya isimu na lugha (1990), ni maneno mawili au zaidi yenye maana zinazokaribiana sana. Vinyume kwa upande wake ni maneno yaliyo na maana kinyume na neno jingine (Massamba, 2004). Hiponimi kwa mujibu wa Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha (TUKI, 1990), ni neno ambalo maana yake imejumuishwa katika maana ya neno jingine. Kuna uhusiano wa karibu baina ya dhana hii na hiponimia ambayo ni dhana inayorejelea uhusiano uliopo baina ya neno maalum na neno la jumla.

Katika kuchanganua uteuzi wa kipekee wa lugha kwenye matini zilizoteuliwa, muktadha wa kiisimu umefaa katika kuelewa baadhi ya teuzi za kimsamiati hasa kwa kuangazia uhusiano wake na maneno mengine kimlalo na kiwima.

### 3.2.2 Muktadha wa hali

Halliday (1994) anauelezea muktadha kuwa ni dhana ambayo ndani mwake inajumuisha vipengele vitatu vifuatavyo:

**Uwanja-** ni dhana anayoitumia Halliday kurejelea kile kinachozungumziwa au sajili inayohusika katika matini fulani. Kipengele hiki kina uhusiano wa karibu na kile baadhi ya watalamu wanakiita muktadha wa mada. Katika tasnifu hii, matini zinazorejelewa zaidi zinajihusisha na suala la amani na maridhiano. Hivyo basi, uteuzi wa msamiati katika matini hizi unafungamana kwa namna ya moja kwa moja na unaongoza teuzi za wasanii hawa katika kuwasilisha ujumbe wao.

**Wahusika-** Halliday anatumia dhana hii kurejelea washiriki katika matini iwe semwa au andhishi kwa kuzingatia mahusiano yao. Kwamba katika mchakato wowote wa kimawasiliano, kuna mwasisi na mpokeaji ujumbe. Aidha, mahusiano baina yao huathiri pakubwa uteuzi wa lugha itakayotumiwa na ufasiri wa ujumbe. Katika kutunga muziki, msanii huwa na hadhira ambayo anailenga. Inaweza kuwa vijana pekee, wazee au hata hadhira mseto. Wakati mwingine wanalenga wananchi huku baadhi yao wakilenga viongozi. Katika kushughulikia mahusiano baina ya wahusika hawa, uteuzi wao wa msamiati hufungamana na dhamira yao pamoja na uamilifu wa matini wanayozalisha.

**Mbinu -** Halliday anatumia dhana hii kurejelea mbinu ya uwasilishaji ambayo aghalabu inaweza kuwa ama semwa au andishi. Katika muktadha wa matini tulizozishughulikia, kuna uchangamano katika mbinu ya uwasilishaji. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, muziki huandikwa ili uimbwe. Hivyo basi, msanii katika kuteua msamiati, vishazi na hata sentensi, sharti azingatie uumbuji wa tungo atakazoibua. Lazima atimize mahitaji ya utanzu huu ya kuwepo kwa muwala na mdundo maalum katika matini yake. Ili kutimiza matakwa haya, wasanii wanateua msamiati pamoja na miundo ya tungo kimakusudi

jambo lililojadiliwa katika kuchanganua uteuzi wa kipekee wa lugha katika matini husika.

### 3.2.3 Muktadha wa kijamii

Tukirejelea lugha kama mfumo, vipashio vyake vya kileksia pamoja na kategoria za kisarufi zinahusiana na muktadha wa kijamii. Katika jamii ndimo kaida na masharti ya kutumia lugha huwekwa na kwamba lugha ni kipengele mojawapo cha utamaduni wa jamii yoyote ile.

Wasanii walioshughulikiwa katika utafiti huu wanapatikana katika muktadha fulani wa kijamii. Ndani ya muktadha huu, kuna mila, tamaduni, desturi na imani ambazo zinatawala na kuongoza matumizi ya lugha. Kwa mfano, baadhi ya wasanii kama vile Naxiz (*Kenya ni yetu -2009)* anatambua kwamba, licha ya kuwa kikaida viongozi katika jamii wanapaswa kujali masilahi ya wananchi, hali nchini Kenya wakati huu ilikuwa kinyume ambapo viongozi hawa, hasa wale wa kisiasa, wanawapuuza watu wa matabaka ya chini na kujilimbikizia mali bila kujali hali za wanaowaongoza. Hali hii anaizungumzia kwa mfano anaposema:

*Can't u see kuwa inakuwanga scandalous*
*Politicians hao hawajali wanajibamba marvelous*
*magguzlers, ma one-pack na polygamous….*

Katika kifungu hiki, Naxiz anachora taswira ya viongozi ambao hawajali maslahi ya wananchi jambo ambalo huenda linasababisha kutokuwepo kwa amani na maridhiano miongoni mwao. Anawarai wananchi waweze kumaizi ukweli huu, kwamba viongozi

hawawajali, na badala yake wanapaswa kuishi kwa amani na maridhiano. Kwa mfano anasema:

*...natamani siku moja akili zetu ziwe fit*
*Tuwachange hii balaa ya kuchoma nchi hii*
*Kuvunja kwa maduka na kuiba maTV...*
*Kuingia kwa boma na kunajisi mabinti*
*Kupewa 50 bob kufikiri we ni tajiri…*
*Niaje unanihanda kwa sababu ya lugha yangu?...*

Hali hii huenda imechangia kutokuwepo kwa amani na maridhiano nchini Kenya kutokana na utepetevu wa wanasiasa katika kuwajibikia majukumu yao waliyotengewa. Yale anayoyarejelea katika muziki wake yataeleweka tu katika muktadha wa jamii anayoirejelea. Nchini Kenya, wanasiasa hujilimbikizia mali kisha huigawanya jamii kwa misingi ya kikabila na huwalipa vijana pesa kidogo, kutokana na hali zilizopo za umasikini, ili wazue vurugu na vita ambavyo husababisha uharibifu wa mali na kuleta dhiki miongoni mwa wanajamii kutokana na vitendo kama vile vya ubakaji.


### 3.3 Upekee katika uteuzi wa lugha

Hali fulani maalum huhitaji matumizi fulani ya lugha (Oduori, 2005). Kulingana naye, Diskosi hizi maalum na za kipekee huwa ni namna ya kusuluhisha au kutuliza hali. Upekee unaofanywa katika matumizi ya lugha huwa na nia maalum, mojawapo ikiwa ni kuhamasisha. Upekee wa kuafikiana kama matokeo ya matumizi ya lugha huhitaji uzingativu wa kina wa hali maalum ya matukio ya wakati huo. Kwa mujibu wa mada, waimbaji wote katika nyimbo zilizoteuliwa kwa ajili ya utafafiti huu walitambua kuwepo

kwa haja ya amani na maridhiano nchini Kenya. Hata hivyo, namna wanavyoteua lugha kupitia msamiati, vishazi na sentensi, na kuuwasilisha ujumbe wao inajitokeza katika mitindo tofauti.

### 3.3.1 Upekee wa kimsamiati

Lugha hutekeleza uamilifu tofauti tofauti katika jamii kama anavyoelezea Halliday (1973) katika nadharia ya majukumu ya lugha.  Ili kufikia uamilifu lengwa, mtumiaji lugha sharti afanye uteuzi wa kimakusudi katika ngazi ya kimsamiati na kimuundo. Kwa kawaida, mtu anapotumia lugha huwa na wazo au dhana fulani anayolenga kuiwasilisha na hulazimika kufanya uteuzi wa kimakususdi katika ngazi za mofolojia na sintaksia ili kufanikiwa katika lengo lake. Yaani, katika kusimba ujumbe, mzungumzaji huifinyanga lugha atakavyo ili kuibuka na maana fulani anayotaka kuiwasilisha. Mchakato huu ili ufanikiwe hutegemezwa kwa vitengo vya fonolojia, sintaksia, mofolojia na semantiki. Mwasisi wa ujumbe huchagua wazo kati ya mawazo mengi yaeleayo akilini mwake (semantiki) kisha huteua umbo litakalobeba maana hiyo (mofolojia) kisha huyapanga maneno katika muundo maalum (sintaksia) halafu hutoa sauti kutamka maneno yale (fonolojia). Hali hii hudhihirika ifuatavyo:




**Mchoro : 1 Mchakato wa usimbaji na usimbuaji wa ujumbe**

Saussure, (1916) katika kuchanganua lugha anapendekeza mwelekeo wa kimuundo ambapo anaiona lugha kama mfumo wa ishara. Kila neno aghalabu linasheheni sehemu mbili; ishara na kiashiriwa. Ishara ni sauti ya lugha inayotumika huku kiashirikwa ikiwa istilahi anayopendekeza kuashiria dhana inayorejelewa katika ulimwengu halisi. Anabainisha kuwa uhusiano baina ya dhana hizi mbili aghalabu ni nasibu. Katika

matumizi yetu ya lugha, hasa katika usanii, wakati mwingine tunavuruga uhusiano huu ili kujenga mguso wa kiusanii. Kwa mfano katika nyimbo, kwa kutegemea uamilifu wa wimbo, Msanii huenda akatumia ishara mbalimbali kurejelea viashiriwa ambavyo sio vya kikaida.

Matini nilizoshughulikia katika tasnifu hii zinalenga kuwasilisha dhana sawa, amani na maridhiano. Hata hivyo, uwasilishaji unatofautiana kutoka kwa msanii mmoja hadi mwingine katika ngazi tofauti tofauti ikiwemo uteuzi wa msamiati. Vichocheo vya upekee huu wa kiuteuzi vinaweza kueleweka kwa kuzihusisha matini hizi na muktadha ambamo zinazalishwa kiisimu, kijamii na kihali.

**Mfano A1**

- **Mnyonge**

Dogo Biggie (2008) katika wimbo wake *Amani Kenya*, anateua baadhi ya msamiati kimakusudi kuwasilisha ujumbe wake. Uteuzi huu unakiuka matumizi ya kawaida ya maneno. Kwa mfano, katika kuzungumzia wanaoathirika kutokana na ukosefu wa amani, anatumia neno ***"Mnyonge."*** Tukilichunguza neno hili tunapata kuwa, maana linalowasilisha katika muktadha huu wa matumizi ni tofauti kwa akali fulani na maana yake halisi.

Kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (TUKI, 2004) neno mnyonge lina maana ya; mtu dhaifu; mtu asiyekuwa na nguvu. Pia lina maana ya mtu mwenye tabia ya upole na ya kunyenyekea au mtu wa hali ya chini; kabwela.

Tukilinganisha maana halisi ya neno hili na maana yake kimatumizi katika muktadha huu, tunapata kuwa neno mnyonge limetumika kwa maana pana. Hii ni kwa vile, maana yake kwa kuzingatia muktadha wa kiisimu wa neno hili, limetumika kwa maana ya mwananchi wa tabaka la chini. Anaeleza kuwa:

> ***Mnyonge*** *analia, kila saa twakimbia,*
> *kila saa twaumia, kila saa twapigana*
> *watoto wanalia, wamama wanabakwa*
> *wazee wanakatwa, bila hata sababu.*

Nchini Kenya watu wanaoathirika zaidi kunapotokea vurugu huwa ni wanajamii wa matabaka ya chini hasa wanawake, wazee na watoto katika matabaka haya. Kwa kutumia neno wanyonge, anafanikiwa kuzungumzia hali zinazowakabili kila mara ghasia zinapotokea. Hata hivyo, uteuzi wa neno ***Mnyonge*** ni wa kimakusudi kwa vile matumizi ya maneno ya kawaida kama vile, wananchi yangewasilisha dhana ile ile. Kwa kutumia neno mnyonge ambalo katika muktadha huu wa matumizi ni hiponimu ambayo inabeba maana ya wazee, watoto na wanawake, anafanikiwa kuzungumzia hali za makundi haya hivi kwamba, anapoanza kuyaorodhesha, inakuwa anatilia msisitizo kwa hali yao ya unyonge. Hali hii inamfanya msikilizaji wa wimbo huu kuwaonea huruma “wanyonge” hawa na kutaka kuwakinga na kuwalinda dhidi ya maafa kama hayo. Anafanikiwa kuoanisha hali ngumu zinazowakabili wasiokuwa na nguvu katika jamii kila mara kunapotokea vurugu. Tukilinganisha uteuzi wa Dogo Biggie na ule wa Skool Fizz na Daluta (2008) katika wimbo wao *Kenya ni yetu*, tunapata kuwa huku Dogo Biggie akitumia neno wanyonge kurejelea kundi linaloathirika zaidi, Skool Fizz na Daluta wanatumia kishazi *mwananchi asiye na hatia* kurejelea wanaoathirika. Uteuzi wa Dogo

Biggie wa neno “wanyonge” hivyo basi unapata ufaafu hasa kwa kuzingatia utanzu wa matini hii, muziki, ambao sifa yake mojawapo ni matumizi ya lugha ya mkato. Anafanikiwa kutumia neno moja ambalo ndani mwake linasheheni maana nyingi na linaibua uzito wa kimaana na kunasa nathari ya hadhira na hivyo kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe wa amani na maridhiano miongoni mwa wananchi.

**Mfano A2**

- **Harambee**

Upekee katika uteuzi wa msamiati aidha umedhihirika kupitia kwa matumizi ya neno ***Harambee*** katika wimbo wa Juliani, *Kenya Yetu* (2010). Neno hili kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (TUKI, 2004) lina maana ya:

> Mwito wa kutia moyo watu ili kuweza kusukuma au kuvuta kitu kizito kwa pamoja: Harambee! Mwito wa kuhamasisha wananchi kushirikiana kuchangia maendeleo yao, uliohimizwa na aliyekuwa rais wa Kenya, Mzee Jomo Kenyatta.

Tukizingatia maana ya neno hili, tunapata kuwa msanii Juliani ameliteua kwa kuzingatia muktadha wa kijamii ambamo matini yake inalenga. Aliyekuwa rais wa kwanza wa Jamuhuri ya Kenya alilitumia neno hili kuwahimiza wananchi kuvuta kwa pamoja, kushirikiana na kuishi kwa umoja ili kuchangia katika kuleta maendeleo nchini. Matumizi ya neno hili yanawakumbusha wananchi kule walikotoka. Neno hili lilitumika zaidi nchini Kenya punde tu baada ya kujinyakulia uhuru. Msanii huyu kwa kulitumia neno hili, anaashiria kuwa ni pale tu ambapo Wakenya watakapokuwa na amani na maridhiano miongoni mwao ndipo wataweza kuwa na ushirikiano katika kulishughulikia jambo lolote lile baina yao. Bila wao kupendana, neno ***Harambee*** halitakuwa na maana kwao. Hivyo basi, wananchi wanakumbushwa matunda ya kushirikiana kwa vile kwa

umoja wao, waliweza kutimiza mambo mengi ya manufaa kwao kama vile kumtimua mkoloni. Matumizi ya neno harambee basi yanaibua hisia za kizalendo, kuhimiza haja ya umoja pamoja na kuwakumbusha wananchi haja ya kuishi kwa amani na maridhiano kwa manufaa ya kila mwananchi bila kubaguana.

**Mfano A3**

- **Aibu**

Neno aibu kwa kawaida lina maana ya; jambo livunjialo mtu heshima (TUKI, 2004). Katika matini tulizoshughulikia, neno hili limetumika kwa maana anuwai. Kwa mfano, Skool Fizz na Daluta katika wimbo wao *Kenya Yetu* (2008) wanalitumia neno hili kwa maana yake halisi. Wanaona kuwa wakenya walijitia aibu kwa kupigana baada ya uchaguzi. Neno hili pia limetumika na Millenium Band katika wimbo wao *Amani Kenya* (2011). Hata hivyo, tukilinganisha matumizi yake na maana ya neno aibu kwenye kamusi, inabainika kuwa wamelitumia kwa maana tofauti. Kwa mfano wanasema:

i. *Umoja pia amani tusilete <u>aibu</u> Kenya*
ii. *<u>Aibu</u> huharibu mali*
iii. *<u>Aibu</u> hupora mali*
iv. *Kupigana ni <u>aibu</u> sana*
v. *<u>Aibu</u> kuhangaishana*
vi. *Tutetee **heshima** zetu*

Tukizingatia maana ya neno aibu katika miktadha lilimotumika, tunapata kuwa katika sentensi i, iv,na v, neno aibu limetumika kwa maana yake ya kawaida. Yaani hali inayovunjia mtu heshima. Kwa kawaida, hakuna mtu anayependa aibu. Daima mtu hujitahidi kudumisha heshima miongoni mwa wenzake katika jamii. Hivyo basi, kwa kutumia neno hili, wanawarai wananchi kufuata mienendo ambayo itawadumishia heshima.

Kwa upande mwingine, matumizi ya neno aibu katika sentensi ii, na iii, yanaibua maana tofauti. Wanahusisha aibu na uharibifu na uporaji wa mali. Haya ni mambo ambayo hutokea pale ambapo jamii inakosa amani. Kwao, kutokuwepo kwa amani na maridhiano kunaileteа nchi fedheha na zaidi yake kuitumbukiza jamii katika mashaka kama vile ya kuharibu na kupora mali za wengine. Hali hii ndiyo wanayohimiza wananchi kuacha hasa tunapozingatia sentensi vi, "*tutetee heshima zetu*". Hapa wanahusisha heshima na kuwepo kwa amani na maridhiano katika nchi.

**Mfano A4**

- **Lahaja**

Lahaja ni istilahi inayotumiwa kurejelea kitarafa cha lugha kinachobainika ama kijamii au kijiografia na kudhihirishwa na vipengee maalum vya kisauti na kimuundo (TUKI, 1990). Hii ina maana kuwa aghalabu huwa kuna mfanano wa namna fulani baina ya vijilugha vinavyorejelewa kama lahaja. Massamba (2004) anaipambanua lahaja kuwa ni lugha mojawapo kati ya lugha ambazo kimsingi huhesabiwa kuwa lugha moja isipokuwa zinatofautiana katika mambo madogo kama lafudhi au msamiati usiokuwa wa msingi. Kinachobainika ni kuwa, tunapozungumzia lahaja tunatambua kwamba kuna mfanano

baina ya lahaja mbalimbali na kwa wakati huo huo, kuna tofauti zinazodhihirika katika ngazi mbalimbali.

Tukiangazia namna neno hili limetumika katika muziki wa Skippa Mistari, *Mkenya Daima* (2012) neno lahaja limetumika kwa maana tofauti ikilinganishwa na maana yake halisi japo maana inayozalishwa ina uhusiano na maana hii. Skippa anasema; "*Lahaja isitutenge…"* Tukiangazia nchi ya Kenya mojawapo ya sababu za kuwepo kwa vita huwa ni tofauti za kikabila. Kamusi ya Kiswahili Sanifu (TUKI, 2004) inafafanua kabila kuwa: ni kikundi cha watu wanaohusiana kwa lugha, mila desturi na utamaduni. Hivyo basi, tunaporejelea tofauti za kikabila kama sababu mojawapo ya kuzuka kwa uhasama na vita baina ya Wakenya, kwa namna fulani tunazungumzia tofauti za kilugha baina ya wananchi hawa. Kwa kutumia neno lahaja katika muziki wake, Skippa Mistari anamaanisha tofauti zetu za kilugha hazifai kuwa sababu ya wananchi kutengana. Hata hivyo, nchi ya Kenya inakadiriwa kuwa na makabila 42 tofauti (Ogechi, 2012). Hii ina maana kuwa, nchi ya Kenya ina lugha zaidi ya 42 ambazo baadhi yake hazina uhusiano wa karibu kiasi cha kuziita lahaja. Kuzirejela lugha hizi kama lahaja hivyo basi kuna maana kuwa, msanii huyu anatambua kwamba kuna kitu kinachofanana baina ya wazungumzaji wa lugha hizi tofauti, kwamba wao ni Wakenya. Mfanano huu ndio unaorejelewa na Juliani (2010) katika wimbo wake *Kenya Yetu* kuwa ni kabila moja analoliita ***Kikenya.*** Himizo hapa ni kwa wananchi kuona mfanano uliopo baina yao (kwamba wao ni Wakenya) na kuutilia mkazo badala ya kuangazia tofauti ndogo ndogo zinazowagawa katika makundi ya kikabila. Iwapo watafanya hivyo, basi nchi ya Kenya itakuwa na amani na maridhiano.

**Mfano A5**

- **Ubabiloni.**

Neno hili limetumika na Masai Worriors katika wimbo wao *Kenya Moja* (2009). Hili ni neno ambalo limetoholewa kutoka neno la kiingereza, Babylon. Huu ni mji uliotumika katika Bibilia ambapo wana wa Mungu waliteswa kwa sababu ya imani yao. Walipitia mateso mengi. Leo hii, hasa katika muktadha wa kimuziki, neno hili hutumika kurejelea mataifa ya kimagharibi sanasana yanayofuata itikadi ya kibepari. Inaaminika kuwa mataifa haya ndiyo yanayosababisha matatizo kwa mataifa yanayoendelea. Katika muktadha wake wa matumizi hapa, Masai Worriors wanawarai wananchi kukataa

ushawishi wa “kibabiloni” na badala yake waungane na kuishi kwa pamoja na kutia bidii katika kuijenga nchi yao. Wanasema:

> *tupinge* ***Ubabiloni*** *na tuwe na bidii…*

Katika kuliteua neno hili, wasanii hawa wanazingatia muktadha wa kijamii wa walengwa ambao asilimia kubwa ni wakristo na hivyo dhana ya babiloni sio ngeni mno kwao. Hata hivyo, kwa misingi ya imani zao, babiloni ni mahali pasipofaa na hivyo, kupinga ubabiloni ni wito wa kuelekea kunakofaa, kuwepo kwa amani na maridhiano. Aidha, kwa vijana wengi, babiloni ni kitu, mtu, sera au asasi yoyote inayowakandamiza. Hivyo basi kupinga ubabiloni huenda kunaashiria kupinga wanasiasa ambao huwatumia kuzua vurugu katika nchi na hivyo kuhimiza amani na maridhiano.

### 3.3.2 Upekee wa Vishazi.

Kishazi ni tungo ambayo ni ndogo yenye uanifu ndani mwake, na inaweza kusimama peke yake au kuwa sehemu ya sentensi (TUKI, 1990). Vishazi aghalabu hubainika katika sintaksia ya lugha. Mtu anapotaka kuwasilisha wazo fulani hulazimika kuteua maneno na kisha kuyapanga ili kuwasilisha maana anayolenga. Ili afanikiwe katika kufanya hivi, lazima tungo atakazotumia ziwe na muundo unaokubalika katika lugha husika. Katika ngazi ya kishazi, kuna uwezekano kikawasilisha dhana kamili au kikategemezwa kwa sentensi nyingine ili kipate ukamilifu wa kimaana.

Tukiangazia vishazi vilivyotumika na wasanii katika matini tulizoteua tunapata kwamba wanafanya uteuzi wa kimakusudi kwa msamiati na miundo ili kukidhi haja ya kuwasilisha dhamira walizolenga. Wanazingatia mahusiano ya maneno kwenye vishazi (uhusiano mlalo) na pia hadhira wanayoilenga pamoja na muktadha wa kijamii unozunguka matini husika.

Halliday (1973) anatambua kuwa mwanadamu hutumia lugha kutekelezea majukumu mbalimbali kama inavyodhihirika katika matini hizi ambazo zina uamilifu wa kukemea na kuionya jamii dhidi ya maovu yanayoikabili jamii na kwa namna hiyo kuielekeza. Fairclough (1992) anatambua kuwa ili tuelewe maana katika diskosi ni sharti matini zichanganuliwe kwa kuzihusisha na muktadha unaozizalisha. Vishazi tulivyoteua kushughulikia vimesanifiwa kimakusudi kwa kuzingatia muktadha wa kijamii pamoja na hadhira inayolengwa ili kutimiza malengo ya wasanii hawa. Kwa mfano:

**Mfano B1**

- **Kioo cha Afrika**
- **Lakini sasa vichwa chini ya meza (Skool Fizz na Daluta- *Kenya ni yetu;* 2008)**

Skool Fizz na Daluta wanatumia kishazi “kioo cha Afrika” kuashiria zile nyakati ambapo nchi ya Kenya ilikuwa na amani na utulivu. Wakati huo mataifa mengi barani Afrika na ulimwenguni kote yaliitazama nchi ya Kenya kama mfano mzuri wa nchi iliyokuwa na amani. Kenya wakati huo ilisifika kwa mambo mengi mazuri yakiwemo shughuli za kiutalii, kunawiri michezoni kama vile riadha, shughuli za kilimo za mazao kama vile kahawa, majani chai na pareto. Mengi ya mambo haya yalipata kunawiri kwa sababu ya hali ya amani na utulivu iliyokuwepo katika nchi. Wakati huo, nchi ya Kenya ilijulikana kote kama yenye amani kiasi kwamba hata vikosi vyake vya kulinda usalama vilitumiwa katika sehemu zingine za ulimwengu zilizokuwa na utepetevu wa amani.

Kutokana na ahali iliyokuwepo hasa baada ya machafuko yaliyotokea baada ya uchaguzi mkuu wa 2007 uliokumbwa na utata, watu wengi kote ulimwenguni walishangaa kilichojiri nchini Kenya kiasi kwamba vichwa vya wakenya “vilikuwa chini ya meza”. Hii ni licha ya kuwa katika miaka ya awali, wakenya walitembea “vichwa vyao vikiwa juu” hasa kutokana na ahali ya amani iliyokuwepo nchini. Haya yote yanadhihirika kupitia kwa wimbo *Kenya ni Yetu* (2008) pale ambapo tunaambiwa:

> Hapo majuu, tulitembea vichwa juu
>
> Tukidai si wakenya, waliokamilika

Nchi yenye amani, na **kioo cha Afrika**

Siasa zaendelea, na watu pamoja

Lakini sasa vichwa chini ya meza
Aibu kubwa, twaulizwa Kenya kulikoni?

Matumizi ya neno "kioo cha Afrika" ni ya kipekee na maana ya kishazi hiki inatokana na uamilifu wa kioo kama kifaa. Bara la Afrika kwa muda mrefu limekumbwa na migogoro ya mara kwa mara katika nchi kama vile: Somali (tangu 1985), Sudan (tangu miaka ya tisini), Sierra Leone, Liberia, Nigeria, DR Congo, Angola, Rwanda, Burundi, Uganda na mataifa mengine. Nchi ya Kenya katika ukanda wa Afrika mashariki kwa muda mfrefu ilionekana kuwa yenye maendeleo ya kiuchumi na mfumo wa kisiasa ulikomaa na uliohakikishia wananchi amani. Hivyo basi, ilikuwa miongoni mwa baadhi ya mataifa ya kiafrika ambayo yalikuwa ya kupigiwa mfano. Hata hivyio, baada ya ghasia za mwaka wa 2008, sifa ya Kenya kama nchi yenye amani ilitiliwa shaka na mataifa mengi huku ikilinganishwa na nchi ambazo awali zilikumbwa na migogoro na machafuko ya mara kwa mara. Hii iliwaletea wananchi fedheha na hivyo "wakaweka vichwa chini ya meza."

Hali hii ya machafuko nchini inaweza kunasibishwa na uongozi mbaya ambapo wanasiasa wanakosa kuwajibika na kutowajali wananchi. Wanajilimbikizia mali kwa njia zisizo halali, kuwagawa wananchi katika misingi ya kikabila kwa manufaa ya kibinafsi pamoja na kueneza ufisadi nchini, jambo linalorudisha maendeleo ya nchi nyuma. Suala hili linaibua hali ya kutuhumiana baina ya wananchi huku wakilaumiana kwa matatizo ya kijamii, kisiasa na hata ya kiuchumi yanayowakabili. Hali hizi ndizo anazokemea Skippa

Mistari katika wimbo wake *Mkenya Daima* (2012) tunapozingatia baadhi ya vishazi kama vile:

**Mfano B2**

- **Baada ya uchaguzi kwetu ni talaka**
- **Acheni kututenga**
- **Siasa zako sitaki tena**
- **Sitaki ukabila**

Skippa Mistari anawaelezea wananchi tabia za kibinafsi za viongozi wa kisiasa nchini. Tukiangazia kishazi “baada ya uchaguzi kwetu ni talaka”, anarejelea hali ambazo hutokea nchini kila baada ya uchaguzi mkuu. Wanasiasa baada ya kupigiwa kura hutoweka na hurejea baada ya miaka mitano wakija kuomba kuchaguliwa tena. Hata hivyo, wananchi huhadaiwa kwamba wanapaswa kumchagua “mtu wao” kwa maana ya mtu wa kabila lao huku wakichochewa dhidi ya watu wa makabila mengine. Haya ndiyo anayarejelea Skippa anaposema kuwa “viongozi hawatupendi, wanapenda kura zetu.” Katika kusema hivi, anawaweka viongozi katika kundi tofauti na wananchi. Anaeleza kuwa, kwa viongozi kilicho muhimu ni kura wanazopigiwa na wanaweza kufanya lolote ili wazipate ba;li hawana haja na wananchi wala hawajali masilahi yao. Aidha, anawahimiza wanasiasa waacha kuwatenga wananchi katika misingi ya kikabila. Haya yanadhihirika tukirejelea vishazi: “Acheni kututenga” na “Sitaki ukabila.” Inavyobainika ni kuwa, anawalaumu wanasiasa na kuwaona kama chanzo cha utengano na migogoro iliyopo miongoni mwa wananchi. Katika kuhimiza umoja, msanii huyu anatumia nafsi ya

kwanza katika kishazi "**<u>si</u>**taki Ukabila" kwa kutumia kiwakilishi na nafsi hii (si). Katika kufanya hivi anajinasibisha na wananchi ili kupinga ukabila ambao umekuwa donda ndugu nchini Kenya na huchangia machafuko yanayoshuhudiwa baada ya uchaguzi.

Suala la wanasiasa na uchochezi wao kama chanzo cha migogoro nchini Kenya pia limeangaziwa na msanii Aram Ara katika wimbo wake *Ukabila* (2012) anaposema:

**Mfano B3**

- **Wametuchochea**

Tukiangazia mfano huu, kuna wahusika wawili mmoja akilaumiwa kwa kusababisha uchochezi. Matumizi ya kiwakilishi "wa", ambacho ni kiwakilishi cha nafsi ya tatu wingi, yanarejelea wanasiasa. Hawa wanalaumiwa kwa kusababisha uchochezi kwa wananchi ambao mara nyingi hawana sababu yoyote ya kupigana. Ujumbe huu aidha

unapatikana katika muziki wa Naxiz *Kenya ni Yetu* (2009) ambaye anawarai wananchi waerevuke na kuona hila, udanganyifu na ubinafsi wa viongozi hawa. Anasema:

> Natamani siku moja, akili zetu ziwe fit
> Tuachange hii balaa ya kuchoma nchi hii…

Licha ya kuwa wanasiasa wanalaumiwa kuwa ndio wanaochochea uhasama baina ya wananchi, kuna baadhi ya wasanii ambao wanahisi kuwa, wananchi wanapaswa kujifunza kutokana na matamshi ya baadhi ya viongozi. Kwa mfano, Rabbit katika wimbo wake *Uhuru* (2012) anayanukuu matamshi ya aliyekuwa rais wa pili wa Jamhuri ya Kenya, Daniel Toroitich arap Moi. Anasema:

*Tujiepushe na siasa mbaya, ingawaje alikuwa mwanasiasa,*

*Man Toro aliieka visawa, Siasa mbaya maisha mbaya,*

Katika kuhubiri ujumbe wa amani na maridhiano, wasanii wanateua maneno yanayolenga kuwahimiza wananchi kuacha tabia ambazo husababisha migogoro. Kwa mfano,

**Mfano B4**

- **Tupilia mbali ufisadi**

Kishazi hiki kimetumika na wasanii Rhumba Success katika wimbo wao *Amani Kenya* (2010). Mojawapo ya sababu zinazochangia kuhatarisha amani nchini Kenya ni kuwepo kwa ufisadi. Hii ni kwa sababu, ufisadi umeifilisi nchi na kuikwamiza kimaendeleo jambo ambalo limechangia kuwepo kwa umasikini miongoni mwa wananchi. Mojawapo ya sababu zilizotolewa kama kichocheo cha vijana kujihusisha sana katika vita ni hali ya kupokuwepo na ajira (Waki, 2008). Hali hizi ndizo huwafanya vijana hawa kukubali kutumika vibaya na wanasiasa ili kuvuruga amani kwa manufaa ya viongozi wa kisiasa. Vijana hupewa pesa kidogo sana ili kuzua vurugu. Hali hii inakemewa na wasanii. Kwa mfano, Naxiz (2009) katika wimbo *Kenya ni yetu* anawarai wasikubali kutumika ili kutimiza mahitaji ya kibinafsi ya viongozi hawa. Anasema:

*Kupewa 50 bob kufikiri we ni tajiri,*

*Weka panga down na AKs kwa pipa*

Hivyo basi, kwa kuwarai wananchi kutupilia mbali ufisadi, baadhi ya hali ngumu za kiuchumi ambazo huwafanya vijana kutumika vibaya zitashughulikiwa.

Halliday, (1973) anatambua kuwa lugha hutekeleza majukumu anuwai katika jamii. Katika muktadha wa muziki nilioteua, wasanii wengi wanakemea hali mbaya iliyokuwepo nchini baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2007. Hata hivyo, zaidi ya kukemea hali hii na kuonyesha visababishi vyake, baadhi yao wanatoa mapendekezo ili kuhakikisha kuwa hali kama hiyo haitatokea tena. Wanafanya hivi kwa kuteua lugha inayoibua hisia za undugu, uzalendo pamoja na amani miongoni mwa wananchi. Tukiangazia muziki nilioteua katika tasnifu hii, kinachobainika ni kuwa, baadhi ya wasanii wanateua mitindo ya lugha ambayo haizingatii kanuni za kisarufi. Ili kuuelewa uteuzi huu, suala la muktadha pamoja na hadhira inayolengwa ni muhimu kuzingatiwa. Kwa mfano:

**Mfano B5**

- **You plus me, that’s a sensible solution,**
- **Leaders of tomorrow, ni uwongo usiwasikize**

Vishazi hivi vimetumika na msanii Jua Cali na wenzake (2011) katika wimbo wao *Kenya we Pray*. Tukiviangazia tunapata kwamba, kuna matumizi ya lugha ya Kiingereza, japo si sanifu, na matumizi ya Kiswahili. Mtindo huu wa kuchanganya ndimi unafaa hasa tukizingatia kuwa hawa ni wasanii wa kizazi kipya wanaolenga zaidi hadhira ya vijana. Licha ya kuchanganya ndimi na kutozingatia sarufi, ujumbe katika muziki huu una uzito wa kimaudhui hasa kwa kuwarai wananchi kuungana ili kutafuta suluhu kwa matatizo yanayowakumba. Kwa mfano: kishazi “you plus me” kina sehemu tatu. “You” ambalo ni

neno lililotumika hapa kurejelea mtu wa kikundi au kabila hilo lingine. Pili tuna “plus” ambalo kwa kawaida ni neno lililo na maana ya kujumuisha. Hata hivyo katika muktadha huu limetumika kwa maana ya kuleta pamoja na kuunganisha. Mwisho tuna “me” kwa maana ya mimi, kama Mkenya. Kishazi hiki hivyo basi kinahimiza wananchi wa makabila tofauti kuungana na kushirikiana. Tukikihusisha na kishazi “that’s a sensible solution” tunapata maana ya kuwa, iwapo wananchi wataungana na kushirikiana bila kujali tofauti zao za kikabila au nyinginezo, basi wataweza kuishi kwa amani na maridhiano.

Wasanii hawa vilevile wametumia kishazi “leaders of tomorrow ni uwongo usiwasikize.” Nchini Kenya, maneno “leaders of tomorrow” kwa muda mrefu yametumiwa kurejelea vijana na kuwahimiza kuwa na subira wakisubiri nafasi yao ya kuwa viongozi. Hii ni kwa sababu, viongozi aghalabu ndio wenye nyenzo za kuzalisha mali, na ni matajiri. Vijana hivyo basi wanahitajika kungoja nafasi yao ya kupata mali ifike “kesho.” Hata hivyo, wasanii hawa wamekitumia kwa njia ya kinaya kwa vile wanapinga usemi huu na kusema kuwa “ni uwongo usiwasikize.” Hii ina maana kuwa, wanawahitaji vijana kuwajibika na kuchukua nafasi za uongozi na kwa njia hiyo kuwajibika. Iwapo watafanya hivi, hawatatumiwa kusababisha ghasia na vurugu.

Iwapo wananchi wataitikia mwito unaotolewa wa kudumisha amani na maridhiano, basi jamii mpya itazaliwa. Jamii ambayo itakuwa na umoja, upendo na amani kama inavyodhihirika katika vishazi vifuatavyo:

**Mfano B6**

- **Kenya nchi moja (Brasso –*Wakenya Tumeamua, 2008)***
- **Kabila moja (Brasso –*Wakenya Tumeamua, 2008)***
- **Kenya moja (masai worriors – *Kenya Moja, 2009)***
- **Watu iko damu moja (masai worriors – *Kenya Moja, 2009)***
- **Chakula tukule pamoja (masai worriors – *Kenya Moja, 2009)***
- **Tucheze pamoja (masai worriors – *Kenya Moja, 2009)***
- **One tribe (Juliani –*Kenya Yetu, 2010)***
- **Tuko cut from the same cloth (Rabbit – *Uhuru, 2012)***

Tunapata kwamba, wasanii niliowarejelea hapo juu wanatumia vishazi teule kurejelea hali ambayo hakutakuwa na ubaguzi bali wananchi wataioshi kwa amani na umoja. Kwa mfano, msanii Brasso anatumia vishazi kama vile; Kenya nchi moja kuhimiza haja ya wananchi kudumisha umoja kwa kutambua kwamba wao ni kitu kimoja. Wasitengwe na tofauti za kikabila. Hii ndiyo maana anawarai wananchi kujiona kama "kabila moja" la wakenya. Wito huu unakaririwa na Masai Worriors katika wimbo wao *Kenya Moja* (2009) wanapohimiza haja ya kujiona kama taifa moja, "Kenya moja." Wanaongezea kuwa wananchi wa Kenya ni watu wa kizazi kimoja cha mama aitwaye "Kenya" na hivyo basi wao ni watu wa damu moja. Iwapo wakenya watasikia mwito huu, wataweza kushirikiana kwa pamoja na kufanya mambo yao kwa umoja. Masai worriors wanaeleza:

*chakula tukule pamoja, na tucheze pamoja.*

Ili wananchi wafanikiwe kufanya hivi, sharti wajione kuwa kitu kimoja, kabila moja. Rabbit anahimiza kuwa umoja unawahitaji kujiona kama watu ambao wako "cut from the same cloth." Juhudi hizi zitawahitaji kuvumiliana, kusameheana na kuthaminiana kama anavyopendekeza Skippa Mistari katika wimbo *Mkenya Daima* (2012) anaporejelea imani za watu kuhusu baadhi ya makabila yanayopatikana nchini Kenya. Anasema:

*…kwa maisha, natafuta kama* ***mkikuyu,***
*Pesa nikipata, swagger jo, ka* ***mjaka,***
*Shida kwa maisha naziruka ka* ***maasai,***
*Life mbio mbio nakimbia ka* ***mkale…***

Msanii huyu anapendekeza wananchi wachuje na kukopa kilicho bora kutoka kwa kila kabila ili kujenga nchi iliyo bora zaidi. Licha ya kuwa anatumia ucheshi, anapendekeza mambo kadhaa kwa kurejelea imani hizi. Kwa mfano, anahimiza watu wawe na bidii ya kujitafutia riziki kama watu wa kabila la **wakikuyu**, wakishapata wafurahie maisha wafanyavyo watu wa kabila la **wajaka (wajaluo)**. Aidha, anapendekeza kuwa wanapokabiliwa na hali ngumu au matatizo maishani, wakabiliane nazo vilivyo na kuziruka kama warukavyo **Wamaasai** na wawe watu chapuchapu maishani kama **Wakale (Wakalenjin)**.

Tukichanganua ubeti huu, tunapata kuwa Skippa Mistari ametumia imani kuhusu jamii hizi: wakikuyu ni wenye bidii, wajaluo wanapenda kufurahia maisha, wamaasai wana uwezo wa kuruka juu huku wakalenjin wakisifika kwa uwezo wa wa kukimbia. Iwapo

wananchi wataweza kukopa yaliyo mema kutoka kwa kila kabila, basi kutazaliwa jamii moja ya kabila liitwalo **Kikenya** kama asemavyo Juliani (*Kenya Yetu*, 2010)

Hali hii inahimizwa hasa kwa wananchi waweze kuizingatia watakapokuwa wakishiriki uchaguzi katika miaka itakayofuata. Kwa mfano Erick Omondi katika wimbo wake *Raundi Hii* (2012) anawahimiza wananchi wazingatie na kudumisha amani watakaposhiriki katika uchaguzi mkuu wa 2013. Anatumia vishazi kama vile:

**Mfano B7**

- **2013 wakenya tusimame**
- **Raundi hii**

Vishazi hivi vinatumiwa kuhimiza wananchi kudumisha amani katika uchaguzi wa mwaka wa 2013. Kishazi “Raundi hii” anakitumia kurejelea uchaguzi wa mwaka wa 2013 na kuhimiza kuwa:

*Naomba raundi hii tujali maisha*
*Raundi hii tushirikiane pamoja*
*Raundi hii tupige kura bila ukabila*
*Raundi tusing'oe mareli*
*Raundi hii tusipore maduka*
*Raundi hii tupendane*
*Raundi hii tusiuane*
*Tufanye uchaguzi kwa amani*

Haya yote yanayotajwa na msanii huyu ni mambo yaliyotokea katika mwaka wa 2008 baada ya nchi ya Kenya kuwa na uchaguzi mkuu uliokumbwa na utata. Anahimiza mambo hayo yasijirudie tena katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2013.

### 3.3.3 Upekee wa sentensi

Fairclough (1995) anaeleza kuwa, katika kuchanganua diskosi yoyote ile ni muhimu kuzingatia kipengele cha muundo wa kijamii (kuzingatia tabaka, hadhi, umri, kabila na uana). Vilevile, ni muhimu kuzingatia utamaduni wa jamii husika hivi kwamba tutaweza kuoanisha diskosi na maana inayojitokeza kwa kuzingatia muktadha wake.

Massamba (2004) anafafanua sentensi kuwa ni kipashio cha tungo kikubwa kabisa cha kimiundo chenye maana kamili. Katika kushughulikia upekee wa sentensi katika matini tulizoteua, mawazo ya Fairclough (1995) yalikuwa muhimu hasa kutokana na mitindo tofauti ya wasanii tuliowarejelea. Asilimia kubwa ya wanamuziki tuliowarejelea ni wale

wa kizazi kipya ambao matumizi yao ya lugha aghalabu yanasheheni ubadilishaji msimbo, uchanganyaji msimbo pamoja na matumizi ya misimbo isosanifu kama vile sheng'. Ili kuelewa uteuzi huu, sharti turejelee muktadha na katika kufanya hivyo tuuangazie kwa upana wake. Halliday (1994) katika kujadili muktadha wa hali anatambua kuwa, kipengele cha wahusika huwa ni muhimu katika kufasiri maana ya usemi au tungo yoyote ile. Mahusiano ya wahusika hawa wakati mwingine hudhihirisha utabaka katika jamii inayozungumziwa.

Suala hili ni muhimu hasa tunapochanganua matini hizi za amani na maridhiano kwa vile nchini Kenya, wananchi mara nyingi huwalaumu viongozi kama sababu za vita na matatizo yanayowakumba. Wasanii wengine wanatambua utabaka huu na pamoja na tofauti za kikabila zilizomo kama rasilimali ambayo iwapo wananchi wanawaweza kuitumia vizuri, basi nchi ya Kenya itapata amani na kuwa na maendeleo. Hali hii inadhihirika katika baadhi ya sentensi tulizoziteua. Kwa mfano:

**Mfano C1**

**Uzuri wa mama yetu Kenya ni tabaka tofauti (Jimw@t- *Stand Up*, 2008)**

Katika sentensi hii, Jimw@t anatambua kuwa nchi ya Kenya ina watu wa matabaka tofauti tofauti. Hata hivyo, kwake tofauti hizi ndizo zinaipamba nchi ya Kenya na kuipa nguvu za kujiendeleza. Katika muktadha wa matumizi yake, neno tabaka hapa linabeba maana pana ya tofauti mbalimbali zinazodhihirika miongoni mwa wananchi wa Kenya. Tofauti hizi zinajumuisha zile za kiuchumi, kikabila, kijinsia pamoja na kiumri. Awali, kuna nyakati ambapo baadhi ya viongozi wa kisiasa wametumia tofauti hizi

kuwachochea wananchi dhidi ya wenzao. Kwa mfano, kabla, wakati na baada ya uchaguzi mkuu wa 2007, wananchi walikuwa wamegawika katika misingi ya kikabila. Utengano huu ulikuwa sababu mojawapo iliyochangia kuzuka kwa vurugu zilizoshuhudiwa nchini mnamo mwanzoni mwa mwaka wa 2008. Tofauti za kiumri vilevile zimewahi kutumiwa kuigawa jamii katika matabaka ambapo vijana walihimizwa na wazee kusubiri wakati wao huku wakiohimzwa kwamba wao ni “viongozi wa kesho.” Jambo hili liliwakera vijana kwa muda mrefu kwa vile, viongozi (wazee) hawakujali masilahi yao. Hii ndiyo sababu kwa sasa baadhi ya wasanii kama vile Jua Cali na wenzake katika wimbo wao *Kenya we Pray* (2011) wanakemea dhana hii kwa kusema kuwa:

> …*leaders wa tomorrow ni uwongo usiwasikize…*

Tukirejea kwa sentensi iliyopo katika mfano C1, tunapata kwamba zaidi ya kusheheni dhana zinazorejelea utabaka japo kwa namna chanya, kuna himizo la kiuzalendo. Hii ni katika matumizi ya nomino “mama” kurejelea nchi ya Kenya. Katika kufanya hivi, Jimw@t anaibua dhana ya kuwa wananchi wote wa Kenya ni ndugu kwa vile wana mama mmoja aitwaye Kenya. Anaeleza kuwa, Kenya inapata uzuri wake kutokana na tofauti hizi. Mawazo sawa na haya yanaelezewa na msanii Brasso katika wimbo *Wakenya Tumeamua Kuishi kwa Amani* (2008) anapotoa mfano wa jinsi tofauti za wakenya zinaweza kutumiwa kufaa jamii nyingine. Anaeleza:

> *Lakini tushikane mikono, na tule mavuno yetu*
> *Kalenjin atoe maziwa, na mkisii atoe matoke na*
> *Jaluo alete samaki, na Kikuyu alete mukimo na*

*Tukae kwa kiti moja, tule kwa pamoja*

*Tuishi kwa pamoja, Kenya nchi moja*

Brasso anatumia vyakula vinavyohusishwa na jamii mbalimbali kama kielelezo cha tofauti hizi: Wakalenjin wanahusishwa na maziwa, Wakisii wanahusishwa na matoke huku Wajaluo wakihusishwa na samaki na Wakikuyu wakihusishwa na mukimo. Ujumbe unaojitokeza hapa ni kuwa, licha ya tofauti hizi, wote ni wakenya na kila mmoja anaweza akanufaika kutoka kwa mwenzake. Anaeleza:

*…tukae kwa kiti moja, tule kwa pamoja…*

Iwapo wananchi hawa watatambua kuwa tofauti zao ndio msingi wa maendeleo yao, basi wataweza kuishi kwa amani na maridhiano. Hata hivyo, baadhi ya viongozi wa kisiasa nchini Kenya hutumia tofauti hizi kuwachochea wananchi kwa manufaa ya kibinafsi. Hali hii ndiyo inakemewa Zak Mtumishi katika wimbo wake *Sitaki Noma* (2012) anapowarai wananchi kukataa ushawishi huu akisema:

**Mfano C2**

***Mapoliticians wa kuincite watu, wakenya tuwatie zii… (Zak Mtumishi- Sitaki Noma, 2012)***

Tukiuchunguza mfano huu, inadhihirika kuwa, msanii ametumia mseto wa lugha ambapo kuna matumizi ya Kiswahili (maneno *watu, wakenya*), kuchanganya msimbo (maneno *Mapoliticians, kuincite*) na Sheng' (*tuwatie zii*).

Ili kuelewa uteuzi huu wa lugha, sharti tuwaze kuhusu hadhira inayolengwa. Zak Mtumishi ni mmojawapo wa wanamuziki wa kizazi kipya. Hadhira kuu ya muziki wake

ni vijana. Hivyo basi, katika kuwasilisha ujumbe wake, amani na maridhiano, inambidi ateue mtindo wa mtumizi ya lugha ambao unatumika zaidi na kueleweka na hadhira anayoilenga. Waki (2008) anatambua kuwa, vijana ndio waliotumika kwa wingi kusababisha vurugu baada ya uchaguzi wa 2008. Ili kuwafikia vijana hawa, inambidi msanii huyu kutumia Sheng’ ambao ni msimbo maarufu miongoni mwa vijana nchini Kenya (Ogechi 2005, Githiora 2002, Momanyi 2009) ili kuwafikia. Aidha, kumeibuka mtindo miongoni mwa Wakenya wa kuchanganya msimbo kama ilivyo kwa maneno *mapoliticians* na *kuincite.* Hali hii hutokea katika jamii zenye wingilugha (Ogechi 2005). Uteuzi huu unahakikisha kwamba ujumbe wa amani na maridhiano unawafikia vijana kwa lugha wanayoitumia na kuielewa vyema.

Mfano C2 vilevile unasheheni dhana ya utabaka ambapo Zak Mtumishi anaigawa jamii katika makundi mawili; wanasiasa (*mapoliticians*) na Wakenya. Katika kufanya hivi, anawatenga wanasiasa na jamii anayoiita Wakenya. Hii ni kwa sababu, wanasiasa ndio huwachochea (*kuincite*) wananchi (*Wakenya*) kupigana. Anawaona kwamba wao ndio chanzo cha ukosefu wa amani unaoshuhudiwa nchini kila kunapokuwa na uchaguzi mkuu. Ili kurekebisha hali hii na kuhakikisha kwamba kuna amani na maridhiano miongoni mwa wananchi, anawaomba Wakenya wawakatae wanasiasa wachochezi (*tuwatie zii*).

Suala la wanasiasa kuwachochea wananchi na kutowajibika au kuwajali limeangaziwa kama kichocheo kimoja cha vita miongoni mwa wanananchi. Kwa mfano, Skippa Mistari katika wimbo wake *Mkenya Daima* (2012) anaimba kuwa:

> …*Viongozi hawatupendi, wanapenda kura zetu…*

Kinachobainika ni kuwa, ili amani idumu, sharti wananchi watambue hila na ubinafsi wa wanasiasa ambao huwatenga kwa misingi ya tofauti zao ili kujinufaisha wenyewe. Wasanii wanalenga kujitambulisha na wananchi kwa kujiweka katika kundi moja nao. Hii inafanya sauti yao kuwa sauti ya mwananchi. Kwa mfano, wanatumia nafsi ya kwanza wingi katika sentensi zao kama inavyodhihirika katika mfano C2 (sehemu zilizokolezwa rangi):

> …*Mapoliticians wa kuincite watu,* ***wakenya tu****watie zii..*

Hivyo basi, wanaibuka kama sauti ya mwananchi na kwa wakati huo huo kutoa mapendekezo ya jinsi ya kukabiliana na changamoto zinazokumba amani nchini Kenya. Katika kufanya hivi, wanaielimisha hadhira yao kwamba amani inapovurugwa wananchi ndio huumia. Kwa mfano:

**Mfano C3**

> **Fahali wawili wakipigana nyasi ndizo huumia. (Jublak –*Spoken Word,* 2009)**

Jublak katika wimbo wake *Spoken Word* anawatahadharisha wananchi kwa kutumia methali: fahali wawili wakipigana, nyasi ndizo huumia. TUKI (2004) wanafafanua methali kuwa ni:

> Usemi wa kisanii wa kimapokeo unaofikiriwa na jamii kuwa kweli na u unaotumiwa kufumbia au kupiga mfano na huwa umebeba maana pana kuliko maneno yenyewe yanayotumiwa.

Methali aliyoitumia Jublak inatokana na jamii ya waswahili amabo ni kabila mojawapo nchini Kenya. Katika jamii, methali hutekeleza majumu mbalimbali yakiwemo kuhimiza

jambo fulani, kuelimisha, kuelekeza, kuasa na kadhalika. Katika muktadha huu, methali hii imetumiwa kwa maana yake ya ndani kwamba, watu wawili wenye nguvu au mamlaka wanapotengana, kukosana au hata kupigana wanaoumia ni wale walio chini yao wasiokuwa na uwezo. Uteuzi wa methali hii ni faafu kuhubiri ujumbe a amani na maridhiano miongoni mwa wananchi wa Kenya hasa tukirejelea hali ilivyokuwa katika uchaguzi wa mwaka wa 2007. Waliokuwa wawaniaji wakuu wa wadhifa wa urais (Mwai Kibaki na Raila Amollo Odinga) katika uchaguzi huu walikuwa watu wenye uwezo, kifedha na kisiasa. Waliweza kushawishi watu wengi upande wa kila mmoja wao kuwapigia kura hali iliyoigawa Kenya katika makundi mawili makuu yaliyotoshana nguvu. Hata hivyo, ukweli ni kwamba, licha ya kuwa wawili hawa, bwana Kibaki na bwana Odinga, ndio waliokuwa sababu kuu ya kuzuka kwa vurugu, walioumia walikuwa ni wananchi ambao hawakuwania wadhifa wowote. Jublak anawatahadharisha wananchi dhidi ya kurudia hali kama hii kwa vile iwapo kutatokea vita tena baina ya mafahali (ushindani wa kisiasa) zitakazoumia zitakuwa nyasi (wananchi wenyewe).

Hali hii ya wanasiasa kuwachochea wananchi kupigana kwa sababu ya uchaguzi inaibua kinaya kwa vile, licha ya kuwa baadhi yao hushindwa kwenye uchaguzi, wenyewe hawapigani. Badala yake, wao huketi pamoja na kupongezana na ikibidi kugawana mamlaka. Hali kama hii ndiyo anayorejelea Skippa Mistari katika wimbo wake *Mkenya Daima* (2012) anapoimba kuwa:

> *…Mwaka huu nimesema, sitakuwa kibaraka*
>
> ***Huku mtaani tukizidi kupigana**, **viongozi kwa ikulu***
>
> ***Wanapop champagne na kugawana mamlaka….***

Hali kama hii ilitokea mwaka wa 2008 ambapo wakati wakenya walikuwa wakiuana na kuharibiana mali, viongozi wawili wakuu waliosababisha suitafamu iliyozuka pamoja na marafiki wao wakaribu walijifungia kwa hoteli za kifahari wakijadiliana namna ambavyo wangegawana mamlaka. Kwa kurejelea ukweli huu, wasanii hawa wanatumai kuwa wananchi watafumbuka macho na kuona haja ya kuishi kwa amani na kukataa kuchochewa na wanasiasa. Hii ni kwa sababu, bila ya amani, hakutakuwepo na nchi iitwayo Kenya. Juliani katika wimbo wake *Kenya Yetu* (2010) anahimiza kuwa:

**Mfano C4**

- **Bila amani tutavunja Kenya yetu…**
- **Tuijenge nchi yetu kwani ndio wajibu wetu**

Anatambua kwamba wakenya wasipotafuta njia ya kuishi kwa amani, basi nchi itasambaratika na wao ndio watakaoumia. Ni jukumu la wananchi wenyewe kuilinda amani na kuijenga Kenya. Katika kufanya hivi, wanahitajika kutumia kila mbinu kuhakikisha kwamba amani inadumu. Kwa mfano Masai Worriors katika wimbo wao *Kenya Moja* (2009) wanawahimiza wananchi kutumia hata mtandao kueneza amani:

…*facebook na twitter, amani pia twasambaza…*

Wasanii hawa wanapendekeza kuwa, kwa pamoja, wakenya wanaweza kudumisha amani nchini. Kwa mfano:

**Mfano C5**

- **Kuja ndani kwenye basi, twende journey safari ya amani... (Rabbit-*Uhuru*, 2012)**

Rabbit anatumia analojia ya watu wanaosafiri katika basi. Uteuzi huu una mashiko tukizingatia hoja kwamba awali, Kenya kulikosekana amani. Hivyo basi anahimiza wakenya waje pamoja (kuja ndani kwenye basi) ili waweze kujenga amani nchini. Katika kufanya hivyo, anatumia analojia ya safari kumaanisha kuwa, kupoatikana kwa amani ya kudumu nchini Kenya ni mchakato ambao huenda utachukua muda ila utaanza kwa hatua moja kama ilivyo katika safari. Umoja wa wakenya ndio utakaokuwa nguzo ya kujenga amani ya kudumu. Kauli hii inashadidiwa na msanii DJ Parexy katika wimbo wake *Amani Kenya* (2010) anaposema kuwa:

> …*together as one we can make it, Kenya…*

### 3.4 Hitimisho

Katika sura hii,Utafiti ulilenga kupambanua matumizi ya kipekee ya lugha katika ubunaji wa wanamuziki kwa kuzingatia maneno, vishazi na sentensi. Uchanganuzi wenyewe ulijikita kwa masuala yanayoongoza uteuzi wa misamiati pamoja na miundo ya vishazi na sentensi. Kilichobainika katika sura hii ni kuwa, katika kutunga nyimbo za amani na maridhiano, wanamuziki walioteuliwa wamefanya uteuzi wa lugha ambao walihisi ungefaa katika kuwasilisha dhamira yao kwa hadhira waliyokusudia. Matumizi ya hiponimi, antonimi pamoja na sinonimi yamebainishwa katika kurejelea dhana za amani na maridhiano. Hali hii hasa imejitokeza katika uteuzi wa msamiati. Vilevile, suala la

muktadha limeweza kutathminiwa katika kuchanganua uteuzi wa msamiati, vishazi pamoja na sentensi. Imebainika kuwa wasanii wakati mwingine wanateua mitindo isiyo sanifu ya lugha kuwasilisha ujumbe wao kwa kuzingatia hadhira yao. Miongoni mwa mitindo iliyotumika ni pamoja na uchanganyaji msimbo na Sheng'. Kutokana na uchanganuzi uliofanywa, imebainika kwamba licha ya kuwa dhana inayowasilishwa ni sawa kwa wasanii walioshughulikiwa, wanateua lugha yao kwa namna tofauti jambo linaloibua upekee kwa kila msanii. Hata hivyo, ujumbe wa amani na maridhiano umefumbatwa katika nyimbo hizi ambazo zimehimiza haja ya kuishi kwa amani, umoja na upendo bila ya kutengana kwa misingi ya kikabila au kitabaka.

# SURA YA NNE

## UJUMBE WA AMANI NA MARIDHIANO KATIKA MUZIKI: 2008 -2012

### 4.0 Utangulizi

Katika sura hii, ujumbe wa amani na maridhiano katika jumla ya nyimbo 20 zilizoimbwa kati ya mwaka wa 2008 na 2012 umechanganuliwa. Katika kufanya hivi utafiti huu ulilenga kutimiza lengo la kuweza kufafanua ujumbe wa amani na maridhiano katika muziki. Nyimbo hizi zote zilikuwa na jumbe mbalimbali zilizowahimiza Wakenya kuishi kwa amani na maridhiano. Jumbe hizi za amani zilidhihirika kupitia maudhui mbalimbali katika nyimbo hizo. TUKI (2004) wanaeleza maudhui kuwa ni; mambo muhimu yanayoelezwa kama vile katika hadithi, riwaya, hotuba au makala. Katika tasnifu hii nilijikita katika nyimbo zilizolenga kuhimiza amani na maridhiano na ndani mwake, maudhui mbalimbali yalibainishwa. Maudhui hayo yalihusu Wakenya kuacha kupigana, ukabila, ujenzi wa taifa, Wakenya kuishi kwa upendo, kutoharibu mali, kufanya uchaguzi wa amani, wanasiasa kutowatumia wananchi vibaya, ufisadi, Wakenya kusameheana, uchochezi, miongoni mwa mengine.

Kama anavyoeleza Halliday (1973) katika nadharia yake ya majukumu ya lugha, lugha hutekeleza majukumu mbalimbali katika jamii. Nyimbo zilizotumiwa zinatekeleza uamilifu mbalimbali katika jamii iliyolengwa. Hata hivyo, zinalenga kuleta hali ya amani na maridhiano katika jamii ya Kenya. Tukiangazia maudhui mbalimbali yaliyoshughulikiwa, wasanii teule wametumia mielekeo tofauti katika kuwasilisha

ujumbe wao huku baadhi yao wakikemea maovu katika jamii, wengine wakiirai jamii, kuielimisha na hata kuielekeza ili kufikia hali ya amani na maridhiano.

**4.1 Wakenya kuacha kupigana**

Ripoti ya Waki (2008) inaelezea kuwa baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2007, kulitokea machafuko ya kisiasa baina ya makabila tofauti tofauti nchini Kenya yaliyojumuisha mapigano. Kupigana kwa Wakenya ni mojawapo ya sababu nyingi zilizosababisha kuwepo kwa ukosefu wa amani na maridhiano nchini Kenya. Tukizingatia muktadha nchini Kenya uliozunguka nyimbo zilizirejelewa, kipindi kati ya mwaka 2008-2012, wasanii wanarejelea hali iliyotokea punde tu baada ya matokeo ya uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2007 yalipotangazwa. Wakenya kutoka makabila tofauti tofauti walipigana kutokana na utata uliozunguka matokeo hayo. Himizo kwa Wakenya waache mapigano baina yao lilitokea katika nyimbo nyingi tulizozichunguza katika utafiti wetu. Katika miaka mitano iliyoshughulikiwa katika utafiti huu, ujumbe wa Wakenya kuacha mapigano miongoni mwao ulidhihirika katika nyimbo nyingi zilizoimbwa na wanamuziki wengi. Miongoni mwa nyimbo zilizosheheni ujumbe huu ni *Amani Kenya* ulioimbwa na mwanamuziki Dogo Biggie (2008). Mwanamuziki huyu kupitia wimbo huu, anaonyesha kuwa kila wakati wananchi wanapopigana, wanyonge ndio wanaoumia zaidi katika jamii. Anasema kuwa:

*1. Mnyonge analia, kila saa twakimbia*
*Kila saa twaumia, kila saa twapigana,*
*Watoto wanalia, wamama wanabakwa,*
*Wazee wanakamatwa, bila hata sababu,*
*Tuletee amani, kwa nchi yetu ya Kenya,*
*Oh tulete amani, kwa nchi yetu hoo!*

Kutokana na ubeti huu, watoto, wamama na wazee ndio huumia zaidi kunapotokea vurugu katika nchi. Katika hili kundi baadhi ya maonevu yanayowakumba ni kama vile wamama kubakwa. Kwa mfano, katika machafuko yaliyotokea nchini Kenya baada ya uchaguzi uliokumbwa na utata wa mwaka wa 2007, jumla ya visa takribani 3,000 vya mama waliobakwa viliripotiwa. Vingi huenda havikuripotiwa. (Waki, 2008).

Msanii huyu anawahimiza Wakenya wasipigane kwa kuwahimiza waishi kwa amani. Hili linajitokeza wazi katika kiitikio cha wimbo wake ambapo anasema:

*Tusipigane tusiuane, sisi wote tuwe na amani*
*Tusipigane tusiuane, sisi wote tuwe na umoja.*

Dogo Biggie anatumia lugha ili kuhwasilisha ujumbe huu. Katika kufanya hivyo, anateua lugha kwa njia ambayo inaipa uamilifu wa kuhimiza ambapo anawaomba wanajamii wasitishe vita na mauaji miongoni mwao kwa vile wote ni Wakenya. Iwapo watafanya hivi, basi nchi ya Kenya itakuwa na amani na umoja.

Mwanamuziki Brasso katika wimbo *Tuishi kwa Amani* (2008), anashangaa ni kwa nini Wakenya wanapigana licha ya kuwa wameishi pamoja kwa maelewano kwa miaka mingi. Anasema:

*Mbona tuelewane halafu si'i tupigane?*
*Wakenya halafu mnajivunia kuwa Wakenya.*

Kulingana na msanii huyu, Wakenya wanastahili kujivunia kuwa ni Wakenya iwapo tu kuna maelewano miongoni mwao. Kwa hivyo, ili hili litimie, ni sharti wakomeshe mapigano miongoni mwao' Kulingana na mwimbaji Jimw@at katika wimbo *Stand Up*

(2008), Wakenya wanastahili kutumia makabila tofauti yaliyomo ambayo ni zaidi ya arobaini na mawili (Ogechi, 2012) kujengana na kukuzana na wala si kuuana. Anasema:

*1. Ndugu zangu, dada zangu nisikizeni*
*uzuri wa mama yetu Kenya ni tabaka tofauti*
*arobaini na mbili tulizopewa na mwenyezi mungu*
*kwa amani na upendo tushikane tusitengane*
*tukuzane tusiuane,tusitengane tusichukiane*
*maana wokovu wetu ni sisi; mimi na wewe.*

Kwa kusema kuwa wokovu wetu ni “sisi, mimi na wewe,” mwimbaji huyu anawafahamisha Wakenya kuwa wasitarajie kusaidiwa na mtu yeyote kutoka nje katika kujiimarisha na kujiendeleza bali wasaidiane wao kwa wao. Hii itawezekana tu katika mazingira ya amani na utulivu katika nchi. Himizo hili la Jimw@at kuhusu makabila tofauti ya Wakenya kukuzana ni sawa na kile alichokisema mwimbaji Brasso katika mwaka wa 2008 kupitia wimbo wake *Wakenya Tumeamua Kuishi kwa Amani* ambapo anasema:

*1. Wakenya – tumeamua sote*
*Wakenya – tushikane mikono*
*Wakenya – wameamua wote*
*Wakenya – tuishi kwa pamoja*
*Mimi hapa ni Mkalenjin, na wewe una kabila lako*
*Lakini tushikane mikono, na tule mavuno yetu*
*Kalenjin atoe maziwa na, Mkisii atoe matoke na*
*Jaluo alete samaki na, Kikuyu alete mukimo na*
*Tukae kwa kiti moja moja, tule kwa pamoja*
*Tuishi kwa pamoja, Kenya nchi moja.*

Kwa kurejelea aina mabalimbali za vyakula vinavyonasibishwa na jamii zilozotajwa katika wimbo huu, Brasso anaonyesha ni vipi makabila tofauti yanaweza kunufaika kutoka kwa mengine. Anasema kuwa Mkalenjin atatoa maziwa, Mkisii atoe matoke

(ndizi), Jaluo alete samaki na Mkikuyu alete mukimo (chakula cha jamii ya Wakikuyu kinachoandaliwa kwa kutumia viazi, matawi ya boga na pure).

Anacholenga Brasso ni kuwaelimisha wanajamii na kuwaonyesha kuwa hakuna kabila moja lililo na uwezo wa kujitegemea na kujitosheleza pasi na kuyategemea yale makabila mengine. Kutegemeana miongoni mwa makabila tofauti kutakuwepo tu iwapo hakuna mapigano kati ya makabila tofauti na kuna amani. Mwimbaji DJ Parexy katika ubeti wa pili na wa tatu wa wimbo wake *Amani Kenya* (2010) anakemea hali ya wakenya kupigana kwa misingi ya kikabila na anawahimiza Wakenya waufunike ukabila kabisa:

*2. Sina haya ya kusema mi Mkenya, language na kabila si hoja*
*Japo kuishi kwa pamoja, tusonge mbele kwa pamoja*
*Umoja ni nguvu utengano udhaifu, ukabila sio jibu aah aaah*
*Kwa furaha na upendo tuungane, nchi bora tuijenge*
*Together as one we can make it, Kenya.*

*3.Dj Parexy nimeinuka, siongei chafu mdomo utanuka*
*Sikushiki matai, shati itararuka*
*Sichochei vita, damu itamwagika*
*Wakenya tuinuke, maze tujanjaruke*
*Ukabila tufunike, kuumizana tuepuke*
*Tension isishuke, jina la Mungu lisifike hee*
*Jina la Mungu lisifike*
*Mwenyezi mungu, twaomba amani*
*Hatutaki ya kale kujirudia*
*Enda nasi, utuongoze sisi wakenya*
*Tuungane kwa pamoja, hatuwezi bila wewe.*

Wanamuziki Skool Fizz na Daluta katika wimbo wao *Kenya ni Yetu* (2008), wanasema kuwa ni aibu kubwa kuwa na mapigano nchini Kenya. Hii inatokana na sababu kuwa katika bara la Afrika, hasa Afrika Mashariki, nchi ya Kenya kwa miaka mingi ilijulikana kama yenye amani na utulivu na kwa hivyo ikawa kioo cha Afrika:

*1. Hapo majuu, tulitembea vichwa juu,*
*Tukidai si Wakenya, Waliokamilika,*
*Nchi yenye amani, na kioo cha Afrika,*
*Siasa zaendelea, na watu pamoja,*
*Lakini sasa vichwa chini ya meza,*
*Aibu kubwa, twaulizwa Kenya kulikoni?*
*Hatuna majibu, nyie wapeni jibu,*
*Wakenya vipi? Mbona kumalizana?*
*Chuki ya nini, wote si twafaana?*
*Eti twakatana tena, eti kwa mapanga,*
*Si wote sisi maendeleo twayataka?*
*Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu,*
*Nyinyi viongozi, mkae chini myaongee,*
*Kuna kuelewana, kuna kutoelewana,*
*Maandamano yakomeshe, yasizidi kuendelea,*
*Mwananchi asiye na hatia, asizidi kuumia.*

Skool Fizz na Daluta wanatumia toni ya kuomboleza katika wimbo wao. Wanalenga kuteka hisia za hadhira yao na kuifanya kuwaza juu ya visababishi vya vita, hasara na athari zake katika jamii kwa ujumla.

Millenium Band (2011) kupitia wimbo *Amani Kenya*, nayo inasema kuwa ni aibu kubwa kimataifa kwa wananchi wa Kenya kupigana na kuharibu nchi yao wao wenyewe. Hili linajitokeza katika ubeti wa tano ambapo wanaeleza:

*5. Kupigana ni aibu sana*
*Aibu kuhaingaishana X2*
*Tutetee heshima zetu X2*
*Aibu – kimataifa X2*
*Aibu - huharibu Kenya X2*

Vita na mapigano yanapotokea katika nchi yanafanya nchi isiendelee (Mara, 2009). Masai Worriors katika wimbo wao *Kenya Moja* (2009) wanawarai wananchi kuwacha vita ili kuhakikisha kwamba jamii inaendelea. Katika wimbo huu wanaeleza:

*1.We don't have to fight, yapasa tuungane,*
*Tushirikiane ili tusonge mbele, hamna haja kuuana,*
*Kuumizana, kutengana*
*You are my brother, Iam your sister,*
*Basi tuache vita, Sema No kwa siasa mbaya,*
*Ili tuweze kwenda mbele, Sema No No kwa siasa mbaya.*
*Kenya moja X2 - Kenya moja tushirikiane X2*
*Wenye nchi X2 - Wenye nchi tushikane*
*Wenye nchi - Wenye nchi tupendane*
*Tushikane tudumishe – tudumishe amani*

*2.Please vijana wenzangu, amkeni kumekucha*
*Fanya kazi kwa bidii, sababu miaka inasonga,*
*Msidanganywe na wanasiasa, ili fujo ufanye*
*Kwani wewe hujui, ndiye kiongozi wa kesho,*
*Wenye nchi wazalendo, tuwe sisi kitu moja,*
*Tuishi kwa amani, kama chanda na pete,*
*Chakula tukule pamoja, na tucheze pamoja,*
*Taifa ni moja, na watu iko damu moja,*
*Wimbo wa taifa, tunaimba mmoja,*
*Basi sisi Kenya moja*
*Kijana hapana uliza, vile nchi atasaidia,*
*Wewe uliza, vile utasaidia nchi,*
*December to December, amani tushikilie,*
*Tujivunie kuwa Wakenya, Wakenya ile napenda amani,*
*Tushikane sisi wote, tuwe sisi kitu moja,*
*Na tujivunie kuwa Wakenya, au sio?*

*3. Tudumishe amani na upendo, yaani sisi sote ni kwa vitendo.*
*Tusijifanye eti kuwa tunaweza kukumbuka, desturi za ukoloni,*
*Hapana tumekataa, tupinge Ubabiloni na tuwe na bidii,*
*Kama Mkenya, fuata historia ili tuweze kupenya,*
*Ndani ya mitaa, kama happy people,*
*Tuungane, tuonyeshane upendo na umoja,*
*Tusahau desturi za ukoloni, kwani siku zilizopita hatutaki tena,*
*Watu walipigana wakauana, damu ikamwagika machozi yakatiririka,*
*Tumesahau hiyo maneno maanake, Kenya mpya ni amani na upendo.*

*4. Daima mimi Mkenya, na nyuma mimi sirudi,*
*Yaliyopita si ndwele, Wakenya tusonge mbele,*
*Tuwe sisi kitu moja, hakuna aliyezuia,*
*Sisi wote wanadamu, maskini tajiri, bila Mungu hatuko sawa,*
*Tusahau na ukabila, ili tudumishe amani, tushirikiane everyday,*
*Kama ulimi na mate, Wakenya wazalendo,*
*Tupendane kila siku, nchi yetu tuipende,*
*Facebook na twitter, amani pia twasambaza.*
*Mashinani mitaani, amani pia twasambaza*
*Nairobi Kenya – amani tudumishe*
*Rift Valley Kenya – amani tudumishe*
*Nyanza na Pwani – amani tudumishe*
*Eastern na Western – amani tudumishe*
*North Eastern, Central – amani tudumishe*
*Tunataka Kenya moja, Kenya moja tupendane.*

Katika kuwasilisha ujumbe wao, lugha imetumika kutekeleza majukumu mawili makuu; kuhimiza na kutahadharisha. Wanawahimiza vijana waache tabia hii ya kuzua fujo na kuwatahadharisha kuwa wao ndio viongozi wa kesho na kwa kuharibu nchi yao, basi hawatakuwa na kile watakachokiongoza. Katika kufanya hivi, wanawakejeli vijana kwa kuonyesha kinaya kilichopo. Ni kama kwamba kwa kuzua vurugu nchini na kluharibu mali ya watu wanaharibu mali yao wenyewe.

Kwa maoni ya waimbaji hawa, vijana ndio mara nyingi hutumiwa kusababisha fujo nchini Kenya. Hii hutokea baada ya wao kudanganywa na wanasiasa. Waimbaji hawa wanawahimiza vijana waache tabia hii ya kuzua fujo kwa kuwaambia vijana wenzao waamke kwa kuwa kumekucha.

Katika ubeti wa tatu, hawa waimbaji wanasema kuwa mapigano yalikuwa ni desturi ya wakati wa ukoloni na siku hizo zilipita kitambo. Wakati huo, watu walipigana, wakauana, damu ikamwagika na machozi yakatiririka. Wanaongezea kuwa nchi ya Kenya ni mpya na haistahili kuzirejelea desturi za zamani ambapo watu walipigana na kuuana kiholela.

Isitoshe, wanawahimiza Wakenya kuhusu matumizi ya Facebook na Twitter katika kusambaza amani. Kwa muda mrefu sasa, watu wengi wamekuwa wakitumia mfumo huu wa kuwasiliana kwa kutuma jumbe za chuki na za kuzua uhasama miongoni mwa Wakenya (NCIC, 2013). Jumbe za aina hii hupelekea watu kuchukiana na hatimaye kupigana kwa urahisi. Hivyo basi itakuwa bora iwapo wanaotumia mifumo hii ya mawasiliano, wengi wakiwa vijana (asilimia 40 kwa mujibu wa utafiti wa Africa Review, Jan, 10. 2012), wataitumia kuhubiri amani na maridhiano miongoni mwa wakenya.

Mwanamuziki Naxis anahisi kwamba mapigano nchini Kenya hutekelezwa kikabila. Katika wimbo wake wa mwaka wa 2009 *Kenya Ni Yetu*, Naxis anaimba:

*1. Can't you see kuwa inakuwanga scandalous?*
*Politicians hao hawajali wanajibamba marvelous,*
*Maguzzlers, ma one-pack na polygamous,*
*Bei za vitu zimepanda tena viserious,*
*Natamani siku moja akili zetu ziwe fit,*
*Tuwachange hii balaa ya kuchoma nchi hii,*
*Kuvunja kwa maduka na kuiba maTV,*
*Kupanda juu ya miti na kurusha mikuki,*
*Kuingia kwa maboma na kunajisi mabinti,*
*Kupewa 50bob kufikiri we ni tajiri,*
*Weka panga down na AKs kwa pipa,*
*Mikuki na mishale twazichoma kama kuni,*
*Hii story imechapa jamaa, amka man,*
*Niaje unanihanda kwa sababu ya lugha yangu?*

*Nisikize tu kize, Kenya hii ni yetu wee,*
*Wakati imefika tujipangeni wasee.*

2. *Tumeishi miaka mingi kama ndugu na dada,*
*Shida tumezikumba kama jamii moja,*
*Hata wakoloni hawakutambua makabila,*
*Walitutawala sisi wote kama wakenya,*
*Ukabila ni siasa za maibilisi wachache,*
*Ambao hawaoni raha hadi mambo yachache,*
*Miaka minne inapita mteja hapatikani,*
*Wa tano ukikaribia wako tele mitaani,*
*Na sera zao nyingi na ahadi za utani,*
*Nafasi wakishapata hao wanaingia mitini,*
*Wakati ndio umefika wakenya kuendelea,*
*Tuongezeni bidii na tuzidi jitolea,*
*Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu,*
*Tudai uongozi mwema na pia uadilifu,*
*Yalopita si ndwele basi tupangeni yajayo,*
*Kama sera ni nzuri basi tufuateni nyayo.*

3. *Kenya hii ni yetu,*

*Amkeni tuichukueni sote,*
*Wameshatuchochea siku mingi, I say.*
*Wakati imefika tuichukue sote,*
*Eeh, eeh, ooh, ooh.*
*Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu,*
*Akili zetu ziwe fiti sisi sote kama wakenya,*
*Chanukeni wasee.*

Katika ubeti wa kwanza, Naxis anauliza: “Ni aje unanihanda (kwa maana ya unanipiga) kwa sababu ya lugha yangu? Nisikize tu kisee (mwenzangu), Kenya ni yetu wee.”

Kulingana na Naxis, ingawa Kenya ina watu wanaozungumza lugha nyingi kutokana na makabila mengi tofauti, hii haistahili kuwa chanzo cha mapigano. Badala yake anasema kuwa Kenya ni ya kila mmoja wao na pasiwe na mapigano yoyote baina yao.

Katika ubeti wa tatu, Naxis anawadokezea Wakenya namna watakavyokomesha mapigano miongoni mwao. Anahoji kuwa:

*3.Kenya hii ni yetu,*
*Amkeni tuichukueni sote,*
*Wameshatuchochea siku mingi, I say.*
*Wakati imefika tuichukue sote,*
*Eeh, eeh, ooh, ooh.*
*Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu,*
*Akili zetu ziwe fiti sisi sote kama wakenya,*
*Chanukeni wasee.*

Kwa kusema kuwa "Kenya hii ni yetu, amkeni tuichukueni sote," Naxis anawahimiza Wakenya kujua kuwa wote wako sawa na kusiwe na kabila lolote litakalojiona kuwa bora kushinda makabila mengine. Naxis aidha anawahimiza Wakenya wawe na upendo miongoni mwao kwa kukubali kuishi pamoja bila mapigano yoyote kati yao. Naxis hatambui moja kwa moja wale wanaowachochea Wakenya kupigana, anaposema kuwa "Wameshatuchochea siku mingi." Lakini anapotumia kiwakilishi kiambata 'wa' katika kitenzi wameshatuchochea, mwimbaji huyu huenda anamaanisha wanasiasa. Katika utafiti huu, waimbaji wengi wamewatambua viongozi wa kisiasa nchini Kenya kama wachochezi wakubwa wa mapigano mengi yanayotokea baina ya wananchi (Kwa mfano; Zak Mtumishi katika *Sitaki Noma (2012)* anatambua wanasiasa kuwa wachpochezi anaposema: "…mapoliticians wa kuincite watu, wakenya tuwatie zii…"). Naxis anawahimiza Wakenya kupendana na kuwa na umoja kwa kusema kuwa umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Kwa msanii huyu, kutakuwa na shida nyingi nchini Kenya wananchi wasipokubali kuishi pamoja na waache kupigana. Anaongezea kwa kusema kuwa "Akili zetu ziwe 'fiti' sisi sote kama Wakenya" kumaanisha kuwa Wakenya wawe

timamu na wenye akili zilizokamilifu. Inatarajiwa kuwa, watu wenye akili kamilifu hawastahili kupigana bila sababu.

Mapigano yanapotokea, wanaoumia zaidi ni wananchi wa kawaida anavyosema mwimbaji Jublak katika wimbo wake *Spoken Word* wa mwaka wa 2009. Katika ubeti wa kwanza wa wimbo huu, yeye anasema kuwa "…fahari wawili wakipigana, nyasi ndizo huumia…" Nyasi zinazoumia kulingana na wanamuziki tofauti katika uchunguzi wetu ni wananchi wa kawaida. ambao wanajumuisha kundi la watu walio na uwezo mdogo wa kujinusuru kunapotokea shida mbalimbali katika jamii kama vile mapigano.

Mwanamuziki Kachela katika ubeti wa kwanza wa wimbo *Amani Tunataka* (2012), anahoji kuwa Wakenya hawapaswi kupigana wao wenyewe huku ikikumbukwa kuwa waliungana kupigania uhuru wa nchi yao. Mwimbaji huyu anaimba ifuatavyo:

*Si'i wote ni kitu kimoja, Tusiuane tupendane,*
*Mbona tumwage damu kwenye nchi yetu?*
*Na Kenya ilipata uhuru, Zamani za kale walitupigania,*
*Mabeberu tukapata amani Kenya.*
*Na sa'a hivi twapigana si wenyewe, Viongozi wetu si'i mtupe amani?*
*Sina baba wala mama, mashaka yamenipata nitafanya nini mi mkenya?*
*Kaka na dada washatoweka kama sina haki mie Mkenya basi niambie,*
*Niwe Mturkana au Kikuyu, Jaluo, Maasai si'i wote ni kitu kimoja,*
*Japo kabila tofauti mradi si'i wote ni Wakenya,*
*Tuishi pamoja na amani.*

Kachela anazidi kuwapa viongozi wa Kenya changamoto kwa kusema kuwa wao ndio wanaostahili kuwaletea wananchi amani. Anaongezea kuwa Wakenya hawastahili kujiona kama ni wa kabila fulani kama vile Mturkana, Mkikuyu, Mjaluo au Maasai bali wajione na waishi kama kitu kimoja.

Katika nyimbo nilizotumia katika tasnifu hii, ilibainika kuwa kuna mambo badala ambayo Wakenya wanaweza kujihusisha nayo kando na kupigana ili yachangie kuleta amani miongoni mwa wananchi. Mwimbaji Rabbit katika sehemu ya ubeti wa pili ya wimbo wake *Uhuru* (2012) anaimba kuwa:

> *Aaaa ni mambo nyingi tunaeza fanya tujenge hospitali, barabara,*
> *Aaaa tuanze zetu biashara yee.*

Kutokana na wimbo huu, Rabbit anawachochea wananchi watafute mambo mengi tofauti ambayo wanaweza kujihusisha nayo ili yaweze kuwa ya manufaa kwao. Baadhi ya mambo hayo ni kama vile ujenzi wa hospitali, barabara na kuanza biashara za kuwaendeleza.

Uchunguzi huu pia uligundua kuwa vita baina ya wananchi nchini Kenya huzuka kutokana na propaganda inayoendeshwa kati ya wananchi wenyewe. Mwimbaji Aram Ara katika wimbo *Ukabila* wa mwaka wa 2012, anauliza hivi:

> *Mbona unanipanga na propaganda nishikie bro panga?*

Katika kuwahimiza Wakenya wasipigane, mwimbaji huyu, katika ubeti wa kwanza wa wimbo wake, anaweka bayana kuwa Wakenya hawawezi kujenga nchi yao iwapo kutakuwa na vita baina yao:

*In the making of a nation bloodshed si lazima, kunego tu-peace, si-vita…* (**Tafsiri**: *Katika ujenzi wa taifa, umwagikaji wa damu haustahili kuwepo. Tuzungumzie amani na wala si vita.)*

Mwimbaji Erick Omondi katika wimbo *Raundi hii* (2012) anasema:

*1. Lets love one another, don't kill your brother*

*One Kenya, one nation, God bless Kenya*

*Aaaa Kenya nchi yangu nakupenda*

*Is this what you've been waiting for, a brand new song for my country*

*2013, wakenya tusimame*

*Nakumbuka 1963, Kenya got to be free*

*We all know we agreed, we gonna make Kenya nice place to be*

*2. And I have a dream, to live in peace, let it be*

*Amani lazima watu wote*

*Mbona sasa wakenya tutengane*

*Mbona sasa wakenya tuchukiane*

*Mbona tuachane, mbona tupigane*

*Uchaguzi nasema sio vita*

*Naomba raundi hii tujali maisha*

*Naomba raundi hii tushirikiane pamoja*

*Raundi hii tupige kura bila ukabila*

*Naomba raundi hii tusing'oe mareli*

*Naomba raundi hii tusipore maduka*

*3. Raundi hii, raundi hii*

*Raundi hii, tupendane*

*Raundi hii, tusiuane*

*Raundi hii, tufanye uchaguzi kwa amani*

*raundi hii, tupendane, tusiuane*

*raundi hii, tusitupe maisha juu ni yetu*

*na wahenga walinena, yaliyopita si ndwele*

*lakini bado mimi, roho yangu yaumia*

*mawazo yanikumba, machozi yanilenga*

*mimi bado nalia, I still keep on crying*

*Think about the past*

*Watu wengi walikufa, wengine walikatwa*

*Some got burnt, women got raped*

*Watoto kupotea, vyumba vilichomwa*

*Hadi leo IDP's, mbona tena wakenya tulaumiane*

*Mbona mambo haya tusiyakatae*

*Mbona raundi hii wakenya tusiungane*

*Mbona sisi wenyewe tusifikiri.*

*4. Wanasiasa mimi nawaomba tuweke Kenya mbele Pliz*

*No going back, twende mbele kazi iendelezwe*

*Omba kura bila chuki, ah, wacha matusi*

*Tusipowacha ukabila, tutabaki bila*

*Elimisha wananchi, badala ya kuwapiganisha*

*Raundi hii wanasiasa tushauriane*

*Raundi hii wanasiasa tupendane*

*Raundi hii wanasiasa tusipigane*

*Raundi hii wanasiasa tuimbe amani*

*Raundi hii ni Kenya moja milele*

*5. Raundi hii, raundi hii*

*Wakenya wote tupendane, bila ukabila tuchague*

*When we stand together as one, we can move and change the world,yeeh*

*Tupendane, tupendane, tupendane oh oh*

*Tusiuane, tusiuane, tusiuane eh eh*

*Tusimame, tusimame, tusimame wote*

*Tushikane, tushikane, tushikane wote*

*Tuungane, tuungane, tuungane wote*

*Tusiuane tusiuane, tusiuane tena.*

Kutokana na wimbo huu, mwimbaji huyu katika kuwaonya Wakenya dhidi ya kupigana, anadokeza yafuatayo yatimizwe:

i). Let's love one another, don't kill your brother

(**Tafsiri**: *Tupendane na usimuue mwenzako*).

ii). Mbona tuachane? Mbona tupigane?

iii). Naomba raundi hii tujali maisha.

(**Tafsiri**: *Naomba wakati huu tujali maisha)*.

iv). Raundi hii tusiuane.

(**Tafsiri**: *Wakati huu tusiuane*).

v). Raundi hii tupendane tusiuane

(**Tafsiri**: *Wakati huu tupendane tusiuane*)

Erick Omondi anapotumia maneno ‘Raundi hii’, anamaanisha wakati wa uchaguzi wa mwaka wa 2013. Katika uchaguzi uliokuwa umetangulia huu, yaani ule wa mwaka wa 2007, Wakenya walipigana baada ya utata kuzuka kuhusu kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi huo. Omondi anawaomba Wakenya wasirudie yale yaliyotokea katika uchaguzi wa mwaka wa 2007.

Mwimbaji mwingine aliyekuwa na ujumbe sawa na ule wa Erick Omondi ni Zak Mtumishi. Katika wimbo wake *Sitaki Noma*,(2012), anaimba :

*1. Raundi hii nimeamua baada ya uchaguzi sitaki noma,*
*Last time tulizusha noma na maze kulithuka sitaki noma X2*
*Nishindwe au nishinde, sitataka kutumiwa vibaya*
*Kuchoma hao za watu, kuvunja ndae na mawe,*
*Kupigana kikabila*
*Raundi hii X2 Sitaki noma haa.*
*2. Machali, madame na wazee Wakenya sote tumesema sitaki noma,*
*Msee wa kuleta fitina, aende tumemkataa, Sitaki noma X2*

*3. We don’t want to see, shedding of innocent blood again.*
*Mapoliticians wa kuincite watu, Wakenya tuwatie zii, zii zii zizizi,*
*Mayouth tushikane, tukatae kutumiwa na viongozi wabaya,*
*Tunataka amani, Kenya ni yetu,*

*Sote hatutaki noma, wacha kila mtu aseme sitaki noma X2*

*Mayouth wamesema - Sitaki noma*

*Raila amesema – Sitaki noma*

*Hata Ruto pia amesema – Sitaki noma*

*Uhuru naye amesema – Sitaki noma*

*Hata naye Karua – Sitaki noma*

*Wanasiasa wote – Sitaki noma*

*Zak Mtumishi anasema – Sitaki noma*

*Sisi wote tumeamua – Sitaki noma.*

Zak Mtumishi ananatumia neno ‘noma’ kwa maana ya mapigano au fujo. Yeye anawahimiza Wakenya hivi:

i). Raundi hii nimeamua baada ya uchaguzi sitaki noma.

ii). Last time tulizusha noma na maze kulithuka (mwenzangu mambo yakaharibika).

(**Tafsiri**: *Wakati wa uchaguzi uliopita tulifanya fujo na mwenzangu mapigano yakatokea*).

iii). Nishindwe au nishinde, sitataka kutumiwa vibaya.

Kifungu “…sitataka kutumiwa vibaya” kinamaanisha kuchochewa na viongozi ili kuzua ghasia na machafuko.

iv). We don’t want to see shedding of innocent blood again.

(**Tafsiri**: *Hatutaki kuona umwagikaji wa damu ya Wakenya wasio na hatia yoyote)*.

Licha ya kuchukua mielekeo tofauti kujadili maudhui ya wakenya kuwacha kupigana, wanamuziki hawa wameyaelezea maudhui haya kwa utendeti. wametumia lugha kama kifaa cha kutekelezea majukumu mbalimbali ambayo yanalenga kuhimiza haja ya kuwacha kupigana na badala yake wakenya waishi kwa amani.

**4.2 Ukabila**

Ujumbe mwingine uliotokea katika nyimbo za utafiti huu ni ule iliohusu ukabila. Kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004) ukabila ni dhana inayorejelea matendo au mawazo ya mtu yaliyotawaliwa na kuthamini kabila lake tu na kubagua makabila mengine. Ogechi (2012) anaeleza kuwa nchi ya Kenya ina jumla ya makabila arobaini na mawili. Kuwepo kwa makabila mengi nchini Kenya kumetumiwa na baadhi ya watu, hasa viongozi wa kisiasa, kuwatenga wananchi na hivyo kukwamiza juhudi za kuleta umoja nchini. Kuna Wakenya ambao wamekuwa wakitumia kisingizio cha ukabila ili kuzua fujo kwa muda sasa. Kwa mfano, mnamo mwaka wa 2008, makabila yaliyohusika zaidi katika vita vilivyoshuhudiwa nchini yalikuwa ni yale yaliyokuwa na mwaniaji wa kiti cha urais au waliounga mkono mwaniaji wa kabila fulani na kupinga wa kabila lingine. Mwimbaji Jimw@at katika wimbo *Stand Up* (2008) katika ubeti wa kwanza anaimba:

*1. Ndugu zangu, dada zangu nisikizeni*
*uzuri wa mama yetu Kenya ni tabaka tofauti*
*arobaini na mbili tulizopewa na mwenyezi mungu*
*kwa amani na upendo tushikane tusitengane*
*tukuzane tusiuane,tusitengane tusichukiane*
*maana wokovu wetu ni sisi; mimi na wewe.*

Kulingana na mwimbaji huyu, Wakenya wanastahili kujivunia makabila arobaini na mawili ambayo kulingana na anavyosema yalitolewa na Mungu. Yeye anawahimiza Wakenya wasiuane, wasitengane, wasichukiane bali wakuzane. Katika ubeti wa nne wa wimbo huu, mwimbaji huyu anaweka wazi kuwa si kosa la mkenya yeyote kuwa wa kabila lolote lile. Kwa hivyo anasema kuwa inafaa Wakenya wote wajengane. Anasema:

*4. ...mi ni binadamu tu na mkenya kama wewe*
*kama nilikukosea basi poleni sana*
*si kosa langu kuwa wa lingine kabila*
*amani na upendo hatuwezi*
*ndugu yangu ukinigeuka, nigeukie nani*
*badala ya kutengana, inafaa tujengane.*

Baada ya kugundua kile ambacho ukabila ulisababishia nchi ya Kenya katika mwaka wa 2007 kiasi kuwa karibu nchi iangamie, mwimbaji Eric Wainaina katika ubeti wa pili wa wimbo wake *Daima Mimi ni Mkenya* (2008) anaimba kuwa:

*2. Chuki na ukabila, hatutaki hata kamwe*
*Lazima tuungane tuijenge nchi yetu,*
*Pasiwe hata mmoja anayetenganisha,*
*Kwa uchungu na mateso, kwa vilio na huzuni.*
*Tulijinyakulia uhuru na mashujaa wa zamani,*
*Hawakushtushwa na risasi, au kufungwa gerezani,*
*Nia yao ukombozi na kuvunja pingu za ukoloni.*

Katika wimbo huu, Wainaina anasisitiza kuwa Wakenya wasikubalie chuki na ukabila miongoni mwao kwa kuwa katika kuijenga nchi yao, ni lazima Wakenya waungane licha ya kuwa wao ni wa makabila tofauti tofauti.

Mwimbaji Joey katika ubeti wa kwanza wa wimbo wake *Mwanzo Mpya* (2009), anaelezea ukabila kuwa chanzo cha mapigano yaliyotokea baina ya Wakenya katika mwaka wa 2007. Katika wimbo huu, Joey anaimba ifuatavyo:

> *Ukabila chanzo cha vita ya 2007*
>
> *Kupoteza mali, makao na vifo,*
>
> *Hauzaliwi ukiwa mkabila mwenye chuki, mhuni, unajifunza,*
>
> *Pia jifunze kuishi kwa upendo amani na umoja,*
>
> *Mafunzo ya mama nawapa,Onyesha upendo kwa wote usipime.*

Kando na mwimbaji Joey kuonyesha ukabila kuwa chanzo cha mapigano yaliyotokea nchini Kenya, aidha anaonyesha matokeo ya mapigano hayo kuwa ni pamoja na kupoteza mali, kupoteza makao na kusababisha vifo. Katika kuwahimiza Wakenya wakatae ukabila, Joey anawakumbusha Wakenya kuwa hawakuzaliwa wakiwa wakabila wenye chuki na wahuni bali wanajifunza kuwa na hizo sifa. Changamoto yake kwa Wakenya kuhusu hili ni kuwa wajifunze kuishi kwa upendo na umoja namna wanavyojifunza kuwa wakabila.

Nchi ya Kenya haiwezi kudumisha amani miongoni mwa wananchi wake iwapo wanananchi wenyewe hawawezi kuacha kujihusisha na ukabila. Kikundi cha waimbaji cha Masai Worriors kiliimba ifuatavyo kuhusu ukabila katika ubeti wa nne wa wimbo wa *Kenya Moja* (2009):

*4. Daima mimi Mkenya, na nyuma mimi sirudi,*

*Yaliyopita si ndwele, Wakenya tusonge mbele,*

*Tuwe sisi kitu moja, hakuna aliyezuia,*

*Sisi wote wanadamu, maskini tajiri, bila Mungu hatuko sawa,*

*Tusahau na ukabila, ili tudumishe amani, tushirikiane everyday,*

*Kama ulimi na mate, Wakenya wazalendo,*

*Tupendane kila siku, nchi yetu tuipende,*

*Facebook na twitter, amani pia twasambaza.*

*Mashinani mitaani, amani pia twasambaza*

Waimbaji hawa wanaposema, "Tusahau na ukabila ili tudumishe amani, tushirikiane everyday kama ulimi na mate, Wakenya wazalendo," wanamaanisha kuwa hakutazuka mapigano baina ya Wakenya iwapo wataacha ukabila. Uzalendo wa Wakenya utadhihirika tu kutokana na kushirikiana kwao kila wakati na isitoshe wapendane kama ulimi na mate, yaani kupendana kwa dhati.

Ukabila unatajwa kuwa wa maibilisi na mwimbaji Naxis. Katika wimbo wake *Kenya ni Yetu* wa mwaka wa 2009, Naxis anaimba ifuatavyo katika ubeti wa pili:

*2. Tumeishi miaka mingi kama ndugu na dada,*

*Shida tumezikumba kama jamii moja,*

*Hata wakoloni hawakutambua makabila,*

*Walitutawala sisi wote kama wakenya,*

*Ukabila ni siasa za maibilisi wachache,*

*Ambao hawaoni raha hadi mambo yachache,*

*Miaka minne inapita mteja hapatikani,*

*Wa tano ukikaribia wako tele mitaani,*

*Na sera zao nyingi na ahadi za utani,*

*Nafasi wakishapata hao wanaingia mitini,*

*Wakati ndio umefika wakenya kuendelea,*

*Tuongezeni bidii na tuzidi jitolea,*

*Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu,*

*Tudai uongozi mwema na pia uadilifu,*

*Yalopita si ndwele basi tupangeni yajayo,*

*Kama sera ni nzuri basi tufuateni nyayo.*

Katika wimbo huu, Naxis anadokeza wazi kuwa ukabila haustahili kuwepo katika nchi ya Kenya kwa sababu hata wakoloni hawakutambua Wakenya kwa makabila yao. Anasema kuwa ukabila ni siasa za maibilisi wachache ambao hawaoni raha hadi yachache. Kulingana na mwimbaji huyu, kuna wale wanaofurahia sana wakiona Wakenya wakizozana wa hata kupigana.

Himizo kuu kwa Wakenya katika nyimbo nyingi za amani na maridhiano katika kipindi baina ya mwaka wa 2008 hadi mwaka wa 2012 ni kuwa Wakenya wasijitambue kwa makabila yao mbalimbali bali wajione kama watu wa nchi moja. Matokeo ya kufanya hivyo ni kuwa hakutakuwa na vita kati yao. Ujumbe sawa na huu ulitolewa na DJ Parexy katika wimbo *Amani Kenya* (2010) katika ubeti wa tatu. Anaimba:

*Wakenya tuinuke, maze tujanjaruke*

*Ukabila tufunike, kuumizana tuepuke.*

Kwa kuwahimiza Wakenya “wainuke na wajanjaruke”, mwimbaji huyu anamaanisha kuwa Wakenya wanastahili kufahamu na kujifunza madhara ya ukabila. Iwapo watafanya hivyo, hawataumizana kupitia mapigano yanayotekelezwa kikabila.

Wakenya wana wajibu mkubwa wa kujenga nchi yao. Mwanamuziki Juliani kupitia wimbo wake *Kenya Yetu* (2010) anaimba ifuatavyo:

*1. Sisi sote ni Wakenya, tuilete amani Kenya,*
*Tuijenge Kenya yetu, Kwani ndio wajibu wetu,*
*Tusiwe na ukabila wala chuki, tujenge Kenya, Harambee! Harambee!*
*Kenya yetu – tuipende*
*Kenya yetu – tuijenge*
*Kenya yetu – tuilinde.*
*2. Let us stand together as one nation, let us stand together as one people,*
*Let us unite within our boundaries, for we are Kenyans, one tribe,*
*Sisi wote lugha moja, kabila letu Kikenya.*

*3. Bila umoja hatuwezi songa mbele, bila amani tutavunja Kenya yetu,*
*Lazima tudumishe ndoto ya mababu, tujenge Kenya.*

Katika beti mbili za mwanzo za wimbo huu, Juliani anasema kuwa katika kutekeleza wajibu wao wa ujenzi wa taifa, wakenya wasiwe na ukabila na chuki. Ufanisi katika shughuli hii utakuwepo tu iwapo tu wataungana kama wakenya kwa kuzungumza lugha moja huku kabila lao kuu likiwa ni Kenya.

Mwimbaji Jua Cali na wenzake katika wimbo *Kenya we Pray* (2011) wanaimba ifuatavyo katika sehemu ya ubeti wa sita:

> *….Roho inauma ukabila ni kitu kubwa,*
> *Unanibaguaje na damu haina lugha?*

Kwa waimbaji hawa, ni jambo la kutamausha sana inapotokea kuwa ukabila ni kitu kinachotukuzwa sana nchini Kenya. Wanahoji kuwa Wakenya hawastahili kubaguana kwa misingi ya kikabila kwa sababu damu waliyonayo wote ni sawa na damu haina lugha. Kuongezea haya, mwimbaji Skippa Mistari anawahimiza Wakenya wasizingatie sana makabila yao bali waishi pamoja kwa amani. Katika ubeti wa kwanza wa wimbo *Mkenya Daima* (2012), anaimba:

> *Lahaja istutenge, panga na jembe,*
> *Suti ama kitenge, kijana nina nywele,*
> *kilichobaki tu ni kichana,*
> *inaniuma sana wangwana wakipigana,*
> *juu ya rangi ya kimwili.*

Anaposema "Lahaja isitutenge… inaniuma sana wangwana wakipigana juu ya rangi ya kimwili," mwanamuziki huyu anawashauri Wakenya wasitengane na wasipigane kwa misingi ya makabila yao tofauti.

Kuhusu uchaguzi ambao ungefanywa katika mwaka wa 2013, mwimbaji Erick Omondi katika wimbo *Raundi hii*, anawahimiza Wakenya wapige kura bila ukabila. Anaposema "...wakati huu tupige kura bila ukabila…," anarejelea uchaguzi wa mwaka wa 2013.

Anaomba kura za mwaka wa 2013 ziwe tofauti na za miaka iliyotangulia ambapo Wakenya walichagua viongozi wao kwa misingi ya kikabila. Anatoa hukumu ya kile kitakachotokea wakenya wasipoacha kupiga kura kikabila. Katika ubeti wa nne anaimba:

*…tusipowacha ukabila, tutabaki bila.*

Kwa kusema hivi, Omondi anaashiria kuwa ukabila ni kitu kibaya ambacho kinaweza kuangamiza nchi. Hivyo hakutakuwepo na nchi iwapo ukabila utaendelea kukita mizizi yake nchini. Nchi itakwama kiuchumi, kijamii na hata kisiasa..

**4.3 Uchochezi**

Katika uchunguzi huu, ilijitokeza kuwa vingi vya visa vya kuzorotesha amani baina ya Wakenya huchochewa na wanasiasa. Wanapofanya hivyo, lengo kuu huwa ni kujinufaisha wao wenyewe. Mara (2011), anasema kuwa wanasiasa ni watu ambao wanaweza kufanya chochote katika kutimiza malengo yao hata kama mambo watakayoyafanya yatasababisha vifo.

Katika ubeti wa pili wa wimbo wa mwanamuziki Joey, *Mwanzo Mpya* (2009), inabainika wazi kuwa wanasiasa huwalipa wananchi ili wateleleze vitendo viovu vya kuharibu amani nchini. Anasema kuwa: “Wanasiasa wanakulipa lakini mwisho ni msiba.” Hatima ya haya yote ni kuwa kunatokea shida nyingi katika nchi baada ya wanasiasa kuchochea wananchi. Wakati mwingine, hata hawa wanaochochea wananchi kuangamizana nao huangamia au kuathiriwa kwa namna fulani.

Kikundi cha Masai Worriors kupitia wimbo wao *Kenya Moja*, (2009) ubeti wa pili, wanaimba ifuatavyo katika kuwasihi Wakenya wasikubali kudanganywa na wanasiasa:

*2. Please vijana wenzangu, amkeni kumekucha*

*Fanya kazi kwa bidii, sababu miaka inasonga,*

*Msidanganywe na wanasiasa, ili fujo ufanye*

*Kwani wewe hujui, ndiye kiongozi wa kesho.*

Katika wimbo huu, Masai Worriors wanawarai wale wanaokubali kudanganywa na wanasiasa, hasa vijana, kuzua fujo wasikubali kutumiwa na wanasiasa kuharibu mali. Wanawaambia vijana kuwa mali wanayoharibu ni yao na inaweza kutokea kuwa wao watakuja kuwa viongozi wa nchi ile ile ambayo wanaharibu.

Kikundi cha Rhumba Success nacho katika wimbo *Amani Kenya* (2010), kinawahimiza Wakenya wasikubali kuchochewa na wanasiasa na mwisho wakaangamizana wenyewe. Wanasema kuwa wanaonufaika katika hali hiyo huwa ni wanasiasa. Katika ubeti wa kwanza wanaimba hivi:

*1. Wananchi wazalendo sikilizeni leo, nitaleta rhumba ili tuelimishane X 2*

*Tuungane sote ili tumpinge adui mkubwa wa maendeleo – ufisadi X2*

*Tusidanganyike na wanasiasa, tuangamizane kwa ajili ya faida yao X2*

Mwanamuziki Skippa Mistari anawaambia Wakenya kuwa wanasiasa hawawapendi. Hili linajitokeza katika ubeti wa tatu wa wimbo *Mkenya Daima* (2012). Katika wimbo huu, Skippa anasema kuwa kile ambacho wanasiasa wanapenda kwa wananchi ni kura zao. Baada ya uchaguzi, wanasiasa huwasahau wananchi na kuhamia mijini huku wananchi wakibaki kwenye ghetto (makazi duni ya watu maskini), wakiishi maisha ya kisoto (maisha ya umasikini na duni). Anaimba:

*Viongozi hawatupendi, wanapenda kura zetu,*

*Baada ya uchaguzi ni talaka, wanahamia mjini,*

*Maisha ya thamani, tunabaki kwenye ghetto, life ya kisoto.*

Kuhusu wanasiasa wanaowachochea wananchi, mwimbaji Zak Mtumishi anaelekea kutoa jawabu kuhusu kinachopasa kufanywa na Wakenya. Katika ubeti wa tatu wa wimbo *Sitaki Noma* (2012), Mtumishi anawahimiza wanajamii na kuwarai vijana kushiriki katika kuleta amani. Anaimba ifuatavyo:

*3. We don't want to see, shedding of innocent blood again.*

*Mapoliticians wa kuincite watu, Wakenya tuwatie zii, zii zii zizizi,*

*Mayouth tushikane, tukatae kutumiwa na viongozi wabaya,*

*Tunataka amani, Kenya ni yetu,*

*Sote hatutaki noma, wacha kila mtu aseme sitaki noma X2*

Mwanamuziki huyu anawahimiza Wakenya wawakatae kabisa wanasiasa wale wanaowachochea kwani uchochezi wao hupelekea umwagikaji wa damu wa Wakenya wasio na hatia yoyote. Himizo la kipekee ni kwa vijana ambao ndio hutumiwa zaidi na wanasiasa kuzua vurugu, waungane na kuwakataa viongozi wanaowatumia vibaya. Iwapo haya yote yatatimizwa, kutakuwa na amani nchi Kenya na Kenya itakuwa ya watu wote.

### 4.4 Wakenya waishi kwa upendo

Nchi yoyote ile itakuwa thabiti ikiwa wananchi wake wataishi kwa amani, upendo na utangamano (Waki 2008). Hizi ni nguzo muhimu kwa nchi kuendelea. Katika uchunguzi

huu, tuligundua kuwa muziki wa amani ulioimbwa na Wanamuziki nchini Kenya kati ya mwaka wa 2007 na mwaka wa 2012 ulikuwa na ujumbe maaulumu ulionuia kuwahimiza Wakenya waishi kwa umoja.

Mwimbaji Brasso kupitia wimbo *Wakenya Tumeamua Kuishi kwa Amani* (2008), anaimba ifuatavyo:

*Wakenya tumeamua, kuishi kwa furaha*
*Wakenya tumeamua, kuishi kwa upendo*
*Wakenya tumeamua, kuishi kwa umoja*
*Wakenya tumeamua, kuishi kwa amani*
*Wakenya – tumeamua sote*
*Wakenya – tushikane mikono*
*Wakenya – wameamua wote*
*Wakenya – tuishi kwa pamoja*
*1.Mimi hapa ni Mkalenjin, na wewe una kabila lako*
*Lakini tushikane mikono, na tule mavuno yetu*
*Kalenjin atoe maziwa na, Mkisii atoe matoke na*
*Jaluo alete samaki na, Kikuyu alete mukimo na*
*Tukae kwa kiti moja moja, tule kwa pamoja*
*Tuishi kwa pamoja, Kenya nchi moja.*

*2. Amani amani – Wakenya wenzangu*
*Amani amani – hatutaki vita*
*Amani amani – hatutaki chuki*
*Amani amani – hatutaki wizi*
*Amani amani – hatutaki shida*
*Amani amani – tuishi kwa furaha*
*Amani amani – tuishi kwa upendo*
*Amani amani – tuishi kwa umoja.*

*3. Amani ndio sisi tuna-advocatia, Tuishi vizuri kama tumetulia*
*Kuwa Wakenya hatutavumilia, Bali tutakuwa sisi tunajivunia*
*Kuwa Wakenya wanaopendana, Sio kila saa tu kuzozana*
*Ambapo tunapata watu wanapigana, Badala ya kugonga tu na kuelewana*
*Unapata watu wengi wanatengana, Mbona tuelewane halafu si tupigane*
*Wakenya halafu mnajivunia kuwa Wakenya.*

4. *Amani – yaleta fanaka*
*Amani – yaleta furaha*
*Bila amani tutakuwa na vita, Bila amani tutakuwa na shida*
*Sote tuishi pamoja, tuungane tujenge Kenya*
*Mungu abariki Kenya, Kenya familia moja*
*Kabila moja, nchi moja.*

Brasso anaposema kuwa "Tumeamua sote," analenga kuonyesha kuwa makabila yote nchini Kenya yameamua kuishi kwa amani na upendo. Himizo hili lake lilitokea katika mwaka wa 2008, baada ya Wakenya kukubali kukomesha mapigano baina yao. Mapigano haya yalitokana na malalamishi ya wananchi wengi kuhusu matokeo yaliyozua utata baada ya kura za uchaguzi wa mwaka 2007.

Mwimbaji huyu kupitia wimbo huu anaonyesha kuwa Wakenya wataishi kwa upendo ikiwa miongoni mwa mambo mengine, hakutakuwa na vita baina yao, hakutakuwa na visa vya ufisadi miongoni mwao na hakutakuwa na shida zozote kati yao.

Akiendelea, Brasso anaonyesha Wakenya manufaa ya kuishi kwa upendo. Kutakuwa na fanaka kwa yote watakayoyafanya, kutakuwa na furaha kati yao na hakutakuwa na vita. Haya yote yatawafanya waishi pamoja huku wakiwa wameungana katika ujenzi wa nchi yao.

Mwimbaji Eric Wainaiana katika ubeti wa kwanza wa wa wimbo *Daima Mimi ni Mkenya* (2008) anaimba kuwa:

*Umoja ni fahari yetu*

*Undugu ndio nguvu.*

Kwa kusema kuwa “umoja ni fahari yetu”, Wainaina anakusudia kuonyesha kuwa kukiwa na umoja miongoni mwa Wakenya, watafanikiwa kutekeleza yote na watafaulu katika kuliendeleza taifa lao. Akiongezea, anasema kuwa “undugu ndio nguvu.” Undugu baina ya Wakenya utakuwepo tu iwapo pana amani na maelewano baina yao. Wakiwa na undugu, Wakenya watakuwa na nguvu ya kutekeleza lolote lile kati yao hata kama litakuwa gumu kiasi gani kwa kuwa umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu wanavyosema wanamuziki kama vile Naxis na DJ Parexy.

Mwimbaji Dogo Biggie katika ujumbe wake kwa Wakenya kuishi kwa pamoja kwa amani kupitia wimbo *Amani Kenya* (2008), ubeti wa tatu, anaimba hivi:

*3. Oh Wanakenya tupendane wote pamoja,*
*Umoja nguvu, tusiachane milele na milele,*
*Tukusanyike kama kuku anavyokusanya vifaranga vyake,*
*Kwani unapomuua mwenzako, wewe unajua utaenda wapi?*
*Njia ni moja, tuwe na amani tupendane.*

Ujumbe wa Dogo Biggie katika wimbo huu ni kuwa Wakenya wapendane wote pamoja na wasiachane milele na milele. Anatumia taswira ya kuku kuwakusanya vifaranga wake wote chini ya mbawa zake kama ishara ya Wakenya wote kuishi pamoja kwa kupendana. Iwapo Wakenya watafanya hivyo, watakuwa na nguvu na uwezo wa kutekeleza yote wanayohitajika kufanya kwa umoja kama Wakenya.

Kikundi cha waimbaji cha Masai Worriors kupitia wimbo *Kenya Moja* (2009), kinaimba ifuatavyo katika ubeti wa pili:

*Wenye nchi wazalendo, tuwe sisi kitu moja,*
*Tuishi kwa amani, kama chanda na pete,*
*Chakula tukule pamoja, na tucheze pamoja,*
*Taifa ni moja, na watu iko damu moja,*
*Wimbo wa taifa, tunaimba mmoja,*
*Basi sisi Kenya moja.*

Kwa muda mrefu sasa isipokuwa pale ambapo mapigano ya hapa na pale yamekuwa yakitokea baina ya wananchi, nchi ya Kenya imekuwa ikishuhudia umoja kati ya wananchi wake katika kutekeleza shughuli mbalimbali za ujenzi wa nchi. Masai Worriors wanawahimiza wananchi waendeleze amani na upendo kwa kuishi pamoja kama chanda na pete na washiriki katika mambo mengine ya kitaifa kwa pamoja. Wanasema kuwa wakenya hawana budi kufanya hivyo kwa kuwa wote wana damu sawa na wanaimba wimbo mmoja wa taifa.

Anavyoshauri DJ Parexy katika wimbo *Amani Kenya* (2010) Wakenya hawastahili kujitambulisha kupitia makabila yao na lugha wazitumiazo. Katika ubeti wa pili, anaimba:

*2. Sina haya kusema mi mkenya, language na kabila sio hoja*
*Japo kuishi kwa pamoja, tusonge mbele kwa pamoja*
*Umoja ni nguvu utengano udhaifu, ukabila sio jibu aah aaah*
*Kwa furaha na upendo tuungane, nchi bora tuijenge*

*Together as one we can make it, Kenya.*

Fanaka kwa mambo ambayo Wakenya watayafanya itaonekana pale ambapo Wakenya watafaulu kuishi pamoja kwa upendo pasi na ukabila miongoni mwao. Hii itawawezesha Wakenya wastawi katika ujenzi wa taifa bora.

Mwimbaji Juliani anaimba ifuatavyo katika ubeti wa tatu wa wimbo *Kenya Yetu* (2010):

*3. Bila umoja hatuwezi songa mbele, bila amani tutavunja Kenya yetu,*

*Lazima tudumishe ndoto ya mababu, tujenge Kenya.*

Katika wimbo huu, Juliani anatoa hukumu kwa Wakenya iwapo hawataishi kwa amani na umoja. Yeye anasema kuwa iwapo wakenya hawatakuwa na umoja na amani, watavunja nchi yao na haitasonga mbele. Anaongezea kuwa kwa Wakenya kuishi pamoja, watakuwa wanatimiza ndoto ya mababu wao iliyokuwepo tangu kitambo. Hii ndoto ilinuia kuwawezesha Wakenya kutekeleza majukumu muhimu ya kitaifa, likiwepo lile la ujenzi wa taifa lao.

**4.5 Wakenya wasiharibu mali**

Baadhi ya matokeo ya mapigano baina ya Wakenya baada ya uchaguzi uliozua utata kufuatia kura za mwaka wa 2007 yalikuwa ni uharibifu mkubwa usiokadiriwa wa mali. Maendeleo ya nchi yoyote ile huonekana kupitia mali yaliyopo katika taifa hilo. Mali hayo huwa yamemilikiwa na ama na taifa au watu binafsi. Katika mazingira ambamo mali ya watu binafsi huharibiwa kiholela na watu wengine, huwa ni rahisi mapigano kutokea. Hii ni kwa sababu huchukua juhudi nyingi na muda mrefu kwa watu kuwa na mali waliyonayo hivi kwamba kuyapoteza ni sawa na kupoteza uhai wao. Nchini Kenya mali mengi yaliharibiwa yakiwemo maduka ya jumla, miundomsingi kama vile reli kung'olewa, barabara kuharibiwa, nyumba za watu kuchomwa na mimea mashambani kuharibiwa. Hali hii ilitatiza maendeleo ya nchi kiasi kwamba uchumi wa nchi ulidorora kutoka aslimia 7.1 katika mwaka wa 2007 na bado athari za halii zipo kufikia mwaka wa 2012 ambapo uchumi ulikuwa kwa kiwango cha asilimia 3.8 (Election Dispatch; 2012). Uharibifu huu ndio unaokemewa na wasanii katika miziki yao. Kwa mfano; mwimbaji Naxis katika wimbo *Kenya ni Yetu* (2009), ubeti wa kwanza, anawahimiza Wakenya ifuatavyo:

*Tuwachange hii balaa ya kuchoma nchi hii,*

*Kuvunja kwa maduka na kuiba maTV.*

Mapigano yaliyotokea nchini Kenya yalishuhudia uharibifu wa mali nyingi. Maduka yalivunjwa na vilivyokuwemo kama vile televisheni vikaibiwa. Aidha, nyumba za watu na majengo makubwa katika miji mbalimbali yalichomwa. Haya yote yalirudisha nyuma

nchi ya Kenya kimaendeleo. Athari hizi zilipatikana katika sekta mbalimbali za kiuchumi kama vile ukulima, utalii na hata sekta ya viwanda nchini hali iliyosababisha watu wengi, takriban 400,000 kupoteza kazi (Kitiabi, 2012).

Waimbaji wa millennium Band kupitia wimbo *Amani Kenya* wa mwaka wa 2011 ubeti wa tatu wanatoa mchango wao kuhusu uharibifu wa mali unaofanywa mapigano yanapotokea nchini Kenya:

*3. Babu walisema tazama kila kitu hapa ni mali yenu, mnayaharibu kwa nini?*
*Barabara, nyumba, reli, yote Ni Mali yenu, kwa nini mnayaharibu?*

Waimbaji hawa wanashangaa ni kwa nini Wakenya waharibu mali huku wakiwa wanafahamu vizuri kuwa mali yote yaliyo katika nchi ya Kenya ni yao. Rai hii ni sawa na ile ya Erick Omondi katika wimbo Raundi hii wa mwaka wa 2012, ubeti wa pili:

*Naomba raundi hii (**Tafsiri: wakati huu**) tusing'oe mareli*
*Naomba raundi hii (**Tafsiri: wakati huu)** tusipore maduka.*

Mwaka wa 2012 ulikuwa ni mwaka wa maandalizi ya kupiga kura za uchaguzi ambao ungefanywa katika mwaka wa 2013. Mwimbaji Zak Mtumishi aliimba wimbo ambao ulionyesha ahadi zake kuhusu uchaguzi wa mwaka wa 2013. Ubeti wa kwanza na kiitikio cha wimbo *Sitaki Noma* anaimba ifuatavyo:

*1. Raundi hii nimeamua baada ya uchaguzi sitaki noma,*
*Last time tulizusha noma na maze kulithuka sitaki noma X2*
*Nishindwe au nishinde, sitataka kutumiwa vibaya*

*Kuchoma *hao za watu, kuvunja *ndae na mawe,*

*Kupigana kikabila*

*Raundi hii X2 Sitaki noma haa.*

**(*Hao- nyumba**

***Ndae- magari)**

Katika wimbo huu, Mtumishi anasema kuwa katika kura zozote zile zilizo na washindani, ni lazima kutakuwa na mshindi na mshinde. Kwa hivyo, haijalishi matokeo yatakuwa vipi lakini Wakenya wasikubali kutumiwa na wale ambao huenda watashindwa katika uchaguzi kwa kuchoma nyumba za watu na kuvunja magari kwa mawe. Hili litakuwa jambo muhimu ili kuhakikisha kuwa nchi ya Kenya ina amani na kwamba maendeleo ya haja yanapatikana ili kutatua changamoto na matatizo yanayowakabili wananchi kisiasa, kiuchumi na hata kijamii.

### 4.6 Ufisadi

*Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004) inafafanua ufisadi kuwa ni maovu au uharibifu. Ujelezi huu licha ya kuwa ni finyu unajumuisha dhana za ulaji na utoaji rushwa, kupendelea watu kwa misingi ya kikabila miongoni mwa dhana nyingine. Kwa miaka mingi sasa, Wakenya wengi nchini wamekuwa wakilalamikia visa vingi vinavyoendeshwa na viongozi wa serikali. Nchi ya Kenya ni miongoni mwa nchi zilizoorodheshwa kama zilizo na visa vingi zaidi vya ufisadi duniani. Transparency international (2013) wanaiorodhesha nchi ya Kenya kuwa nambari nne ulimwenguni kote. Katika eneo la Afrika mashariki, nchi ya Kenya ndiyo iliyoongoza katika ufisadi, ambapo asilimia 70 ya watu wanahusika katika visa vya ufisadi, huku Rwanda ikiwa na

visa vichache zaidi vya ufisadi, vikiwa ni asilimia 13. Maendeleo ya nchi hukwamizwa pale viongozi na wananchi wanajihusisha katika visa vya ufisadi. Kwa mujibu wa jarida la masuala ya kiuchumi, Economy Watch (2010) ufisadi ndio kizingiti kikuu kwa maendeleo ya kiuchumi nchini Kenya. Visa vya ufisadi huwafanya watu wengi kuona kuwa haki haitendwi katika kuwahudumia wananchi wote kwa njia ya uwazi na iliyo sawa. Katika hali hii, huwa ni rahisi sana kwa mapigano kutokea baina ya watu wanaolilia haki kutendwa katika nchi yao.

Baadhi ya waimbaji kupitia nyimbo zao za amani kati ya mwaka wa 2007 na mwaka wa 2012 waliimba kuhusu ufisadi nchini Kenya. Mathalan, kikundi cha Rhumba Success katika mwaka wa 2010 kupitia wimbo *Amani Kenya* wanaimba hivi katika beti mbili za mwanzo za wimbo wao:

*1.Wananchi wazalendo sikilizeni leo, nitaleta rhumba ili tuelimishane X 2*
*Tuungane sote ili tumpinge adui mkubwa wa maendeleo – ufisadi X2*
*Tusidanganyike na wanasiasa, tuangamizane kwa ajili ya faida yao X2*
*Wananchi tusimame kidete, tuungane sote tuwe na amani,*
*Tusimkubalie mtu yeyote atutenganishe kwa kuwa umoja ni nguvu X2*
*Wananchi tusimame kidete, tuungane sote tuwe na umoja,*
*Tusimkubalie mtu yeyote atutenganishe kwa kuwa umoja ni nguvu X2*
*2. Ufisadi mbaya tuuache, rushwa na hongo, tuhubiri amani,*
*Let us fight corruption, tupilia mbali ufisadi,*
*Let us preach peace amongst us, tuhubiri amani,*
*Let us love each other, tupendane Wakenya.*

Inadhihirika wazi kupitia wimbo huu kuwa ufisadi ni adui mkubwa wa maendeleo nchini Kenya. Kunapokosekana maendeleo katika nchi huwa ni rahisi kwa wananchi kujiingiza kwa vitendo viovu ambavyo vinaweza kusababisha kuzorota kwa hali ya amani (Waki, 2008). Kwa ajili ya amani katika nchi, waimbaji hawa wanawahimiza wananchi wote waungane katika kupinga visa vya ufisadi.

Katika ubeti wa pili, waimbaji hawa wanawaomba Wakenya watupilie mbali visa vyote vya ufisadi kama vile rushwa na hongo na wahubiri amani.

Ili kuonyesha namna ufisadi ulivyokithiri nchini Kenya, mwimbaji Jua Cali na wenzake wanawakashifu wale wanaoshikilia nyadhifa kubwa serikalini na huwapa watu wasiohitimu kazi kupitia ufisadi. Katika ubeti wa sita wa wimbo *Kenya we Pray*, waimbaji hawa wanaimba:

*6. Vijana tuamke wote tujisaidie,*
*Leaders wa tomorrow ni uongo usiwaskize,*
*Zile kazi walisema ziko wapi?*
*Zile promise walitoa ziko wapi?*
*Vile mi naona tutaendelea bado kuumia.*
*Huku mtaani hakuna Mp anashughulika,*
*Hewa chafu, mamitaro zinaziba,*
*Ni noma makarau pia wanaiba,*
*Kila siku tunashindwa tunakimbilia nani*
*After kila election, naomba kukuwe na amani.*
*Roho inauma ukabila ni kitu kubwa,*
*Unanibaguaje na damu haina lugha?*

*Nipe kazi nimequalify kuifanya.*

Nchini Kenya kuna uhaba mkubwa sana wa ajira, asilimia 40 kufikia mwaka 2012 (Election Dispatch, 2012). Vijana wengi waliosoma hata kufikia kiwango cha chuo kikuu hawajapata kazi. Linakuwa jambo la kukera kuona mtu asiyehitimu kupewa kazi na yule aliyesoma kuachwa nje kutokana na mapendeleo sanasana kwa misingi ya kikabila. Waimbaji hawa wanawapa moyo vijana wenzao kwa kuwaomba wavumilie kwa kupenda nchi yao na siku moja Mungu atawafungulia milango ya kupata kazi walizosomea.

### 4.7 Wakenya Wasameheane

Nchi ya Kenya imeshuhudia visa vingi vya mapigano baina ya wananchi tangu ijinyakulie uhuru wake mnamo mwaka wa 1963 huku vile vya mwaka wa 2008 vikichacha zaidi. Kutokana na ripoti ya tume iliyochunguza vita vya baada ya uchaguzi mkuu wa 2007, ili nchi ipate kuendelea na kusonga mbele, kunahitajika msamaha miongoni mwa wananchi (Waki, 2008). Katika baadhi ya nyimbo za utafiti huu, waimbaji wanawaomba wananchi kutolipiza kisasi na wasemeheane ili kudumisha amani katika nchi yao. Kwa mfano, Jimw@t anaimba ifuatavyo katika ubeti wa pili wa wimbo *Stand Up* (2008):

*2. Moyo wangu kweli wakulilia, japo nafsi yangu bado kutulia*
*machozi yangu yote yatiririka, damu yetu ovyo ikimwagika*
*kwa nini tusahau uchumi wetu, even in this hate we’ve gone through*
*we need one’s strength, tuweze kuziona siku zetu za usoni*
*bila wewe, mimi  bila wewe, mimi bila wewe sasa bila wewe kusamehe*
*bila kusamehe,bila kusamehe, itakuaje.*

Jimw@t anawashauri Wakenya kusameheana kwa kuwa kila mmoja anamhitaji mwenzake katika kuendeleza nchi yao. Anasema kuwa Wakenya hawastahili kusahau uchumi wa nchi yao ambao unahitaji kukuzwa na kuendelezwa kwa ushirikiano wa wakenya wote licha ya mabaya yote waliyotendeana.

Masai Worriors nao katika mwaka wa 2009 kupitia wimbo *Kenya Moja*, ubeti wa nne wanawahimiza Wakenya wasameheane kwa kuwa hakuna aliyezuia yaliyotokea kati yao katika mwaka wa 2007.

*4. Daima mimi Mkenya, na nyuma mimi sirudi,*

*Yaliyopita si ndwele, Wakenya tusonge mbele,*

*Tuwe sisi kitu moja, hakuna aliyezuia,*

*Sisi wote wanadamu, maskini tajiri, bila Mungu hatuko sawa,*

*Tusahau na ukabila, ili tudumishe amani, tushirikiane everyday,*

*Kama ulimi na mate,Wakenya wazalendo,*

*Tupendane kila siku, nchi yetu tuipende,*

*Facebook na twitter, amani pia twasambaza.*

*Mashinani mitaani, amani pia twasambaza*

*Nairobi Kenya – amani tudumishe*

*Rift Valley Kenya – amani tudumishe*

*Nyanza na Pwani – amani tudumishe*

*Eastern na Western – amani tudumishe*

*North Eastern, Central – amani tudumishe*

*Tunataka Kenya moja, Kenya moja tupendane.*

Wanatumia methali “Yaliyopita si ndwele tugange yajayo,” kuwahimiza Wakenya wasameheane na waungane katika kuendeleza nchi yao. Aidha, wanawarai wananchi kutoka pembe zote za Kenya kuungana na kudumisha amani.

**4.8 Uchaguzi wa Amani**

Mojawapo ya visababishi vya mapigano baina ya Wakenya mwanzoni mwa mwaka wa 2008 ilikuwa ni utata uliokumba kura za uchaguzi wa mwaka wa 2007 (Waki, 2008). Wawaniaji wakuu wa wadhifa wa urais katika uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2007 walielekea kujipigia upatu kwamba wao ndio walioibuka washindi. Tume iliyosimamia uchaguzi huo (ECK) ilishindwa kudhibiti viwango vya kuridhisha vya uwazi katika uchaguzi kiasi kwamba hakuna aliyejua mshindi wa kura ya urais alikuwa nani. Hata mwenyekiti wa tume hii, Marehemu Samuel Kivuitu, alinukuliwa kusema kuwa, hakujua mshindi alikuwa nani. Suitafahamu hii ndiyo iliyowafanya “walioshindwa” katika kura hiyo kudai kwamba uchaguzi haukuwa huru wala wenye haki. Matokeo ya hali hii yalikuwa ni kughadhabika kwa wafuasi wa mirengo yote miwili huku uhasama ukizidi na kuishia katika vita vilivyoshuhudiwa mwanzoni mwa mwaka wa 2008.

Katika uchunguzi wa nyimbo za miaka mitano tuliyoishughulikia katika utafiti wetu, ilidhihirika kuwa ujumbe kwa Wakenya kufanya uchaguzi wa amani ulijitokeza katika nyimbo za miaka miwili ya mwisho kati ya ile miaka mitano tuliyoichunguza, yaani mwaka wa 2011 na 2012. Hali hii tunaweza kuinasibisha na hoja kuwa walilenga kuwahimiza wakenya kudumisha amani katika uchaguzi uliotazamiwa kuwepo mwaka wa 2013. Wanamuziki walioimba kuhusu uchaguzi wanasema kuwa mapigano hayatakuwepo tena nchini Kenya iwapo Wakenya watafanya uchaguzi wa amani. Katika

kujadili ujumbe huu, mawazo ya Ngugi (2000) yanaafiki hali hii ambapo anaeleza kwamba muziki una uwezo wa kuunda "usasa" ambao hubadilika na kuwa "ukale" na kutuelekeza kufahamu historia yetu na kwa hivyo usasa huu hutusaidia katika kutabiri "ukesho" wetu na kujua namna ya kukabiliana na ulimwengu ujao. Kwa mfano Erick Omondi katika wimbo wake *Raundi Hii* (2012) anaeleza ifuatavyo katika ubeti wa tatu:

*Raundi hii, raundi hii*
*Raundi hii, tupendane*
*Raundi hii, tusiuane*
*Raundi hii, tufanye uchaguzi kwa amani*
*raundi hii, tupendane, tusiuane*
*raundi hii, tusitupe maisha juu ni yetu*
*na wahenga walinena, yaliyopita si ndwele*
*lakini bado mimi, roho yangu yaumia*
*mawazo yanikumba, machozi yanilenga*
*mimi bado nalia, I still keep on crying*
*Think about the past*
*Watu wengi walikufa, wengine walikatwa*
*Some got burnt, women got raped*
*Watoto kupotea, vyumba vilichomwa*
*Hadi leo IDP's, mbona tena wakenya tulaumiane*
*Mbona mambo haya tusiyakatae*
*Mbona raundi hii wakenya tusiungane*
*Mbona sisi wenyewe tusifikiri.*

Anawakumbusha wakenya historia yao (kipindi cha mapigano ya baada ya uchaguzi mnamo mwaka wa 2008) ambayo ni "ukale" wa nchi ya Kenya na kuwarai kuwa wasikubali mambo yale yajirudie "raundi hii" kwa maana ya uchaguzi uliotazamiwa kufanyika mnamo mwaka wa 2013. Huu ndio "ukesho" ambao Ngugi (2000) anaeleza kuwa tutaweza kukabiliana nao tukizingatia ukale wetu.

Millemium Band wanaimba ifutavyo katika wimbo *Amani Kenya* (2011) ubeti wa nne:

*4. Haki yetu ni haki yetu, tukipiga kura, tupate matokeo sahihi*

*Nikikushinda ukubali, ukinishinda nitakubali, kwa nini tuweke uhasama?*

Katika wimbo huu, wao wanasema kuwa ni haki ya kila Mkenya kupiga kura katika uchaguzi wowote ule unaohusisha Wakenya. Hata hivyo wanatoa tahadhari zifutazo Wakenya wanaposhiriki katika uchaguzi:

i). Ni lazima Wakenya wapewe matokeo sahihi wakati wa kura – hii ni changamoto kwa tume zitakazosimamia chaguzi za baadaye kwa vile tume ya awali ilichangia kwa kutowajibika vilivyo katika kazi yao kama ilivyobainishwa katika ripoti ya Waki, 2008.

ii). Ni muhimu Wakenya wakubali matokeo ya kura na wasiweke uhasama wowote kati yao. Suala la kutokubali matokeo lilichangia pakubwa kuwepo kwa vita nchini mnamo mwaka wa 2008. Hii ni baada ya waliotangazwa kuwa wameshindwa kukinai matokeo hayo jambo lililosababisha wafuasi wao kuanza vita. Hata hivyo, hoja kuhusu kukubali matokeo ya uchaguzi inafungamana na kutegemea kuwepo kwa uwazi na haki katika kura jambo linalotegemea utoaji wa matokeo sahihi.

Mwimbaji Jua Cali na wenzake katika ubeti wa sita wa wimbo *Kenya we Pray* wanaongezea haya kwa kwa kusema kuwa:

*After kila election, naomba kukuwe na amani.*

*(**Tafsiri:** Naomba kuwe na amani baada ya kila uchaguzi).*

Skippa Mistari katika wimbo *Mkenya Daima* (2012) anaimba kuwa hakustahili kuwa na ila wala njama zozote za kuharibu kura uchaguzi unapofanywa. Ujumbe wake katika ubeti wa tatu ni:

*Nazidi kutangaza, kushinda uchaguzi,*
*Ni kwa wingi wa kura, sio mawe na bunduki, mishale na mikuki,*
*Mwaka huu nimesema, sitakuwa kibaraka,*
*Huku mtaani tukizidi kupigana, viongozi kwa ikulu wanapop champagne*
*na kugawana mamlaka, Tunataka peace, yes kura kwa amani.*

Katika wimbo huu, Skippa anawahimiza Wakenya wakubali matokeo ya kura za uchaguzi wa 2013. Anasema kuwa mshindi ni yule atakayepata idadi nyingi ya kura zilizopigwa. Anawakemea Wakenya dhidi ya kupigana kwa mawe na bunduki kwa sababu ya kura. Mwimbaji huyu anawakumbusha Wakenya kuwa wao wanapopigana, viongozi wanaopigania kwa upande mwingine huwa wako ikulu wakisherehekea na kugawana mamlaka. Hapa anarejelea ule ugawanyaji wa mamlaka uliotokea baina ya wawaniaji wawili wakuu wa urais,Kibaki na Raila, baada ya kura za mwaka wa 2007. Kwa hivyo anawaomba Wakenya wapige kura za mwaka wa 2013 kwa amani.

Ujumbe mwingine kuhusu uchaguzi wa amani ni katika wimbo *Raundi hii* wa mwaka wa 2012 ulioimbwa na Erick omondi. Wimbo huo unasema:

*1. Lets love one another, don’t kill your brother*
*One Kenya, one nation, God bless Kenya*
*Aaaa Kenya nchi yangu nakupenda*
*Is this what you’ve been waiting for, a brand new song for my country*

*2013, wakenya tusimame*

*Nakumbuka 1963, Kenya got to be free*

*We all know we agreed, we gonna make Kenya nice place to be*

*2. And I have a dream, to live in peace, let it be*

*Amani lazima watu wote*

*Mbona sasa wakenya tutengane*

*Mbona sasa wakenya tuchukiane*

*Mbona tuachane, mbona tupigane*

*Uchaguzi nasema sio vita*

*Naomba raundi hii tujali maisha*

*Naomba raundi hii tushirikiane pamoja*

*Raundi hii tupige kura bila ukabila*

*Naomba raundi hii tusing'oe mareli*

*Naomba raundi hii tusipore maduka*

*3. Raundi hii, raundi hii*

*Raundi hii, tupendane*

*Raundi hii, tusiuane*

*Raundi hii, tufanye uchaguzi kwa amani*

*raundi hii, tupendane, tusiuane*

*raundi hii, tusitupe maisha juu ni yetu*

*na wahenga walinena, yaliyopita si ndwele*

*lakini bado mimi, roho yangu yaumia*

*mawazo yanikumba, machozi yanilenga*

*mimi bado nalia, I still keep on crying*

*Think about the past*

*Watu wengi walikufa, wengine walikatwa*

*Some got burnt, women got raped*

*Watoto kupotea, vyumba vilichomwa*

*Hadi leo IDP's, mbona tena wakenya tulaumiane*

*Mbona mambo haya tusiyakatae*

*Mbona raundi hii wakenya tusiungane*

*Mbona sisi wenyewe tusifikiri.*

*4. Wanasiasa mimi nawaomba tuweke Kenya mbele Pliz*

*No going back, twende mbele kazi iendelezwe*

*Omba kura bila chuki, ah, wacha matusi*

*Tusipowacha ukabila, tutabaki bila*

*Elimisha wananchi, badala ya kuwapiganisha*

*Raundi hii wanasiasa tushauriane*

*Raundi hii wanasiasa tupendane*

*Raundi hii wanasiasa tusipigane*

*Raundi hii wanasiasa tuimbe amani*

*Raundi hii ni Kenya moja milele*

*5. Raundi hii, raundi hii*

*Wakenya wote tupendane, bila ukabila tuchague*

*When we stand together as one, we can move and change the world,yeeh*

*Tupendane, tupendane, tupendane oh oh*

*Tusiuane, tusiuane, tusiuane eh eh*

*Tusimame, tusimame, tusimame wote*

*Tushikane, tushikane, tushikane wote*

*Tuungane, tuungane, tuungane wote*

*Tusiuane tusiuane, tusiuane tena.*

Anaposema kuwa 2013 Wakenya tusimame, mwimbaji Omondi anawashauri Wakenya wawe tayari kufanya uchaguzi wa amani usio wa vurugu kama ule wa mwaka wa 2007. Katika ubeti wa pili, Omondi anawapa Wakenya changamoto kuwa uchguzi si vita. Ili amani idumishwe wakati wa uchaguzi wa 2013, Omondi anawahiza Wakenya washirikiane na wasipige kura kwa misingi ya kikabila na wasingo'e reli wala kupora maduka ya watu wakati wa uchaguzi.

Mwimbaji huyu katika ubeti wa nne anawakumbusha Wakenya kuhusu yaliyotokea katika uchaguzi wa mwaka wa 2007. Anasema kuwa wakati huo, watu wengi walikufa, wengine walikatwa, wengine walichomwa, wanawake walibakwa, watoto walipotea, makazi ya wengi yalichomwa kiasi kwamba hadi leo baadhi ya wahasiriwa wanaishi katika hema kwa kukosa makazi.

Omondi akiendelea katika ubeti wa nne, anawashauri wale viongozi watakaosimama katika uchaguzi waombe kura bila chuki na waache matusi. Haya ni mambo yanayoweza kuzua kutoelewana kati ya Wakenya na kwa hivyo kusababisha mapigano kwa urahisi. Anawahimiza wanasiasa kuwaelimisha wananchi badala ya kuwapiganisha. Juu ya yote, Omondi katika ubeti wa tano anawaomba wafanye uchaguzi bila kuzingatia misingi yao ya kikabila.

Naye mwimbaji Zak mtumishi katika wimbo *Sitaki Noma* (2012) aliimba hivi:

*1. Raundi hii nimeamua baada ya uchaguzi sitaki noma,*

*Last time tulizusha noma na maze kulithuka sitaki noma X2*

*Nishindwe au nishinde, sitataka kutumiwa vibaya*

*Kuchoma hao za watu, kuvunja ndae na mawe,*

*Kupigana kikabila*

*Raundi hii X2 Sitaki noma haa.*

*2. Machali, madame na wazee Wakenya sote tumesema sitaki noma,*

*Mzee wa kuleta fitina, aende tumemkataa, Sitaki noma X2*

*3. We don't want to see, shedding of innocent blood again.*

*Mapoliticians wa kuincite watu, Wakenya tuwatie zii, zii zii zizizi,*

*Mayouth tushikane, tukatae kutumiwa na viongozi wabaya,*

*Tunataka amani, Kenya ni yetu,*

*Sote hatutaki noma, wacha kila mtu aseme sitaki noma X2*

*Mayouth wamesema - Sitaki noma*

*Raila amesema – Sitaki noma*

*Hata Ruto pia amesema – Sitaki noma*

*Uhuru naye amesema – Sitaki noma*

*Hata naye Karua – Sitaki noma*

*Wanasiasa wote – Sitaki noma*

*Zak Mtumishi anasema – Sitaki noma*

*Sisi wote tumeamua – Sitaki noma.*

Anaposema "**Raundi hii** (wakati huu) **nimeamua baada ya uchaguzi sitaki noma** (vita)," katika ubeti wa kwanza, Mtumishi alilenga kuzungumzia uchaguzi wa 2013 akiwaomba Wakenya wapige kura kwa amani. Anawakumbusha Wakenya kuhusu yale

yaliyotokea wakati wa uchaguzi wa mwaka wa 2007 ambapo kulitokea mapigano makali yaliyosababisha shida nyingi kufuatia kura za mwaka huo. Kwa kuyatumia majina ya wanasiasa mashuhuri nchini Kenya na ambao walikuwa wameonyesha nia ya kuwania urais wakati wa uchaguzi wa mwaka wa 2013, kama vile Raila, Karua, Uhuru, na Ruto, Zak Mtumishi alinuia kuteka hisia za wafuasi wengi wa wanasiasa hawa. Iwapo wanasiasa hawa wangekubali kufanywe uchaguzi wa amani katika mwaka wa 2013, basi wafuasi wao wangefuata ushauri wao na kuzuia vurugu za aina yoyote ile baada ya uchaguzi. Hata hivyo, wakenya wenyewe ndio wenye uwezo wa kuhakikisha kwamba amani ipo na inadumu nchini Kenya.

**4.9 Ujenzi wa Taifa**

Jumbe zote za amani katika nyimbo za miaka mitano tulizozichunguza katika utafiti huu zilinuia kufanikisha ujenzi wa nchi thabiti. Nchi thabiti tunaichukulia kuwa ni nchi ambapo kuna amani kwa wananchi wake kuendeleza shughuli zao bila kizuizi chochote na katika mazingira ya upendo.

Mwimbaji Brasso, katika wimbo *Wakenya Tumeamua Kuishi kwa Amani* (2008), ubeti wa nne anaimba kuwa:

*4. Amani – yaleta fanaka*
*Amani – yaleta furaha*
*Bila amani tutakuwa na vita, Bila amani tutakuwa na shida*
*Sote tuishi pamoja, tuungane tujenge Kenya*
*Mungu abariki Kenya, Kenya familia moja*
*Kabila moja, nchi moja.*

Brasso anawahimiza Wakenya wapendane na wakubali kuishi pamoja na waungane katika ujenzi wa nchi yao.

Mwimbaji Eric Wainaina kupitia ubeti wa pili wa wimbo *Daima Mimi ni Mkenya* (2008) anasema:

*2. Chuki na ukabila, hatutaki hata kamwe*
*Lazima tuungane tuijenge nchi yetu,*
*Pasiwe hata mmoja anayetenganisha.*

Kulingana wa Wainaina, ni lazima Wakenya waungane katika kujenga nchi yao. Kwa kutumia neno lazima, Wainaina anaonyesha kuwa Wakenya hawana uchaguzi ila ni jambo la shuruti kwao kuungana katika ujenzi wa nchi yao.

Katika wimbo *Amani* wa DJ Parexy ulioimbwa mwaka wa 2010, ubeti wa pili una ujumbe wa ujenzi wa nchi ufuatao:

*Umoja ni nguvu utengano udhaifu, ukabila sio jibu aah aaah*
*Kwa furaha na upendo tuungane, nchi bora tuijenge*
*Together as one we can make it, Kenya.*

DJ Parexy anawahimiza Wakenya kuwa ujenzi wa taifa lao utafanikiwa tu iwapo wataungana. Ili wafanikiwe kuungana sharti wawe wenye furaha na upendo. Iwapo wakenya wana furaha na wanapendana, basi watafanikiwa kuijenga nchi yao.

Kwa mujibu wa mwimbaji Juliani katika wimbo *Kenya Yetu* (2010), jukumu la kujenga nchi ya Kenya si la mtu mmoja bali ni la wananchi wote kutekeleza kwani ndio wajibu wa kila mwananchi. Ubeti wa kwanza unaimba ifuatavyo:

*1. Sisi sote ni Wakenya, tuilete amani Kenya,*
*Tuijenge Kenya yetu, Kwani ndio wajibu wetu,*
*Tusiwe na ukabila wala chuki, tujenge Kenya, Harambee! Harambee!*

Katika ujenzi wa taifa msanii Juliani anashauri kuwa hapastahili kuwepo na ukabila wala chuki baina ya wananchi.

Ujumbe sawa na uliotolewa na Juliani kuhusu ujenzi wa nchi ulitolewa na Jua Cali na wenzake katika wimbo *Kenya we Pray* (2011), ubeti wa tatu:

*3. Kenya ni we na mi,*
*Unangojea nani kaa si we kuinua jamii?*
*Unangojea kusaidiwa umepotea nani,*
*Na we ndio wa kusaidia, jitolee nani,*
*Juu Kenya hii, Kenya hii,*
*Ilitolewa na mayouth kwa mkono wa mkoloni,*
*Na mi ni youth nimejitolea, so call on me,*
*Ile Kenya nataka italetwa na mi.*

Waimbaji hawa wanasema kuwa nchi ya Kenya ni ya kila Mkenya na kwa hivyo yeyote asingojee mtu mwingine awajengee nchi yao bali wao wenyewe washirikiane katika kuinua na kuijenga nchi yao.

Mwimbaji Erick Omondi anawaomba wanasiasa wakubalie ujenzi wa nchi uendelee. Katika ubeti wa nne wa wimbo *Raundi hii* (2012), anaimba kuwa:

*4. Wanasiasa mimi nawaomba tuweke Kenya mbele Pliz*
*No going back, twende mbele kazi iendelezwe*
*Omba kura bila chuki, ah, wacha matusi*
*Tusipowacha ukabila, tutabaki bila*
*Elimisha wananchi, badala ya kuwapiganisha*
*Raundi hii wanasiasa tushauriane*
*Raundi hii wanasiasa tupendane*
*Raundi hii wanasiasa tusipigane*
*Raundi hii wanasiasa tuimbe amani*
*Raundi hii ni Kenya moja milele.*

Omondi anawashauri wanasiasa waombe kura bila chuki na waache matusi. Aidha waache ukabila na wawaelimishe wananchi kuhusu mambo muhimu ya kujenga nchi badala ya kuwapiganisha. Kwa kufanya hayo yote, ujenzi wa taifa utaimarika hasa kuelekea kutimiza sera na mipango ya serikali kama vile ruwaza ya 2030.

## 4.10 Hitimisho

Katika sura hii, tasnifu hii imechunguza jumbe za amani na maridhiano katika jamii. Imebainika kuwa jumbe hizi zimewasilishwa kupitia kwa maudhui mbalimbali. Maudhui haya yamewasilishwa kwa dhamira tofauti yakiwemo yanayohimiza wananchi kuzingatia mambo chanya katika jamii kama vile ujenzi wa taifa, kuwa na umoja, kuishi kwa amani pamoja na kufanya uchaguzi wa amani. Kwa upande mwingine, baadhi ya maudhui

yanakemea maovu na kuitahadharisha jamii dhidi ya masuala hasi kama vile, kupigana wenyewe kwa wenyewe, kutukuza ukabila, kuendeleza ufisadi pamoja na kuwahimiza wanasiasa kusita kuwachochea wananchi. Kupitia kwa maudhui haya, majukumu mbalimbali ya lugha katika jamii yamedhihirika.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI WA MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Azma ya utafiti huu imekuwa kuchunguza lugha ya amani na maridhiano katika muziki ulioimbwa kati ya mwaka wa 2008 na mwaka wa 2012. Katika kufikia lengo hili, tasnifu imehakiki nyimbo mbalimbali zilizosheheni jumbe za amani na maridhiano katika kipindi hiki kwa kusisitiza uteuzi wa lugha katika ngazi ya maneno, vishazi na sentensi pamoja na kufafanua jumbe za amani na maridhiano katika miziki hii.

## 5.1 Muhtasari wa Utafiti

Katika sura ya kwanza, suala la utafiti limefafanuliwa kwa kuelezea usuli wake huku tafiti zilizohusu amani zilizoendeshwa katika maeneo mbalimbali ulimwenguni katika nyakati tofauti zikiangaziwa. Aidha, suala la amani nchini Kenya liliangaziwa kwa kina tangu nchi ya Kenya ilipojinyakulia uhuru wake. Hii ni kutokana na hoja kuwa dhana ya amani nchini Kenya ilikuwa mojawapo ya vichocheo vilivyochangia uteuzi wa mada ya utafiti. Nadharia ya majukumu ya lugha ya Halliday (1973) imekuwa mhimili muhimu uliosaidia kufikia malengo ya utafiti huu. Isitoshe, utafiti umehusisha mawazo ya Fairclough (1992) kuhusu uchanganuzi makinifu hususan kipengele kuhusu dhima ya muktadha katika kuchanganua matini yoyote ile.

Sura ya pili imejadili uamilifu wa muziki katika jamii. Katika kufanya hivyo, nguzo tatu muhimu ambazo hukamilisha maisha ya mwanadamu katika jamii zimerejelewa; nazo

zikihusu masuala ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Tafiti za awali zilizorejelewa zilibainisha kuwa, muziki humwathiri binadamu kiuchumi, kisiasa na kijamii. Katika kushughulikia mada muhimu ya utafiti huu iliyohusu amani na maridhiano, utafiti huu umeegemea kwa kiasi kikubwa, uamilifu wa muziki kijamii. Hii ni kwa sababu, uamilifu huu ndio ulioegemea zaidi kwa suala la amani na maridhiano ikilinganishwa na uamilifu wa muziki kiuchumi na kisiasa. Aidha, uchanganuzi uliofanywa na utafiti huu uliangazia matini teule kwa kuzihusisha na jamii ambamo matini hizi zilizalishwa na hadhira iliyolengwa.

Katika sura ya tatu, tasnifu imeshughulikia matumizi ya kipekee ya lugha katika ubunaji wa wanamuziki katika miziki teule. Maneno, vishazi na sentensi yalizingatiwa ili kulifikia lengo hili. Katika sura hii,  muziki uliohusu amani na maridhiano nchini Kenya kati ya mwaka wa 2008 hadi mwaka wa 2012 umedhihirishwa. Muziki huo umeorodheshwa na wasanii wake kubainishwa. Uteuzi wa maneno umechanganuliwa kwa kuangazia uhusiano wima wa maneno yaliyotumiwa na kuyalinganisha na mengine ambayo yangechukua nafasi yake. Katika kuchanganua uteuzi wa vishazi na sentensi, uhusiano mlalo wa maneno umetumiwa na uteuzi uliofanywa kuelezewa kwa kuuhusisha na hadhira iliyolengwa.

Sura ya nne ya utafiti huu imeangazia jumbe za amani na maridhiano zilizowasilishwa katika nyimbo mbalimbali kati ya mwaka wa 2008 na mwaka wa 2012 zilizoimbwa na wasanii tofauti. Katika kufafanua jumbe hizi,  maudhui mbalimbali yaliyolenga kuhimiza amani na maridhiano kama yalivyojitokeza katika nyimbo zilizoshughulikiwa

yameangaziwa. Nadharia ya majukumu ya lugha ya Halliday (1973) imefaa utafiti huu katika kubainisha dhamira za wasanii mbalimbali katika uwasilishaji wa jumbe zao.

## 5.2 Matokeo ya Utafiti

Kupitia kwa utafiti huu, imebainika kuwa, amani na maridhiano ni nguzo muhimu katika maendeleo ya jamii; kisiasa, kijamii, na hata kiuchumi . Hivyo basi, juhudi zozote zile za kuhimiza jamii kuishi kwa amani na maridhiano ni muhimu zitambue ukweli huu. Lugha kama nyenzo imetumiwa na wasanii hawa kuwasilisha ujumbe wa amani na maridhiano. Utafiti huu uligundua kuwa wanamuziki hufanya uteuzi wa kipekee wa maneno katika muziki wao. Wanamuziki hawa hufanya hivi ili kutimiza lengo mahususi walilokuwa nalo katika utunzi wa nyimbo zao. Kilichobainika wazi kutokana na uteuzi huu wa maneno ni kuwa ni sharti uhusishwe na muktadha katika kupata maana kamili iliyolengwa kuwasilishwa na wasanii tofauti katika nyimbo husika. Ilibainika kuwa neno moja linaweza kuwa na maana tofauti kutegemea na muktadha ambamo neno hilo limetolewa.

Uteuzi wa lugha umebainishwa kuwa wenye upekee katika ngazi ya maneno pamoja na miundo ya vishazi na sentensi (Taz. Sehemu 3.3.2 na 3.3.3 mtawalia). Hii ni licha ya kuwa wasanii hawa huenda hawana ufahamu wa upekee huu na uzito wa lugha wanayotumia katika kuwasilisha ujumbe wao. Kwa mfano, utafiti umebainisha kwamba, maneno katika muziki ulioshughulikiwa yamesheheni matumizi mengi ya visawe, vinyume na hiponimu. Imebainika kuwa, vinyume vimetumika hasa pale wasanii wanapolenga kukemea maovu yanayosababisha uhasama na ukosefu wa amani miongoni mwa wanajamii. Kwa upande mwingine, visawe vimetumiwa pale ambapo msanii

analenga kuielimisha jamii kuhusu dhana fulani na hivyo matumizi ya maneno yenye maana sawa yanasaidia kushadidia ujumbe anaowasilisha. Katika kufanya hivi, baadhi ya muziki wa wasanii umesheheni matumizi ya hiponimu ambapo maneno na vifungu mbalimbali vinavyohimiza amani na maridhiano vimewekwa ndani ya neno moja kuu kisha ufafanuzi kutolewa katika vifungu vinavyofuata.

Aidha, utafiti umebainisha kuwa, uteuzi wa lugha wakati mwingine unategemea hadhira inayolengwa. Jambo hili limedhihirika kupitia matumizi ya misimbo isiyo sanifu kama vile Sheng' pamoja na mbinu za uchanganyaji na ubadilishaji msimbo. Mitindo hii imeweza kunasibishwa na hadhira inayolengwa na wanamuziki hawa, vijana. Hadhira hii ni muhimu katika kujadili suala la amani na maridhiano kwa vile kama ilivyobainishwa kwenye tasnifu, hili ndilo kundi linalotumiwa zaidi kusababisha vita na hivyo kuvuruga amani katika nchi.

Majukumu mbalimbali ya lugha yamebainika katika muziki wa wasanii hawa yakiwemo; kuelimisha, kuelekeza, kuhimiza, kuonya, kuhukumu pamoja na kukemea. Katika kuangazia ujumbe wa amani na maridhiano, nyimbo hizi zimewasilisha ujumbe kuhusu haja ya kuwepo kwa amani na maridhiano kupitia kwa maudhui mbalimbali. Katika kufanya hiyo, waimbaji wamehimiza jamii au wanasiasa kuzingatia maudhui hayo au kukemea na kuionya jamii na wanasiasa kuepuka maudhui fulani. Kwa mfano, wasanii wengi wamejadili na kuhimiza haja ya kuishi kwa umoja, kusameheana, kufanya uchaguzi wa amani na kujenga nchi. Kwa upande mwingine, wamekemea na

kutahadharisha dhidi ya masuala kama vile ufisadi, ukabila, uchochezi pamoja na uhasama unaosababisha vita nchini.

Kupitia kwa muziki na uteuzi wa kipekee wa lugha iliyotumika, wananchi wanapewa wasia wa jinsi ya kuhakikisha kwamba nchi ya Kenya inapata amani ya kudumu na kunakuwepo na maridhiano miongoni mwa wananchi. Baadhi ya mambo yanayozungumziwa ni pamoja na haja ya viongozi wa kisiasa kuwajibika na kuwaongoza wananchi badala ya kuwachochea na kuwapiganisha wenyewe kwa wenyewe kwa manufaa ya kibinafsi. Aidha, taasisi mbalimbali nchini, hasa zinazoshughulikia masula ya kisiasa kama vile uchaguzi, zinapewa changamoto ya kuwajibika katika majukumu yake ili kuwahudumia wananchi wote kwa namna yenye haki na usawa. Hata hivyo, kinachobainika kutokana na muziki huu ni kwamba, amani ya kudumu na maridhiano yamo mikononi mwa wananchi wenyewe iwapo wataamua kuishi kwa upendo, umoja, undugu na wawe wazalendo dhabiti.

## 5.3 Hitimisho

Kinachobainika kupitia utafiti huu ni kuwa, nyimbo hazipaswi kupuuzwa tu kama shughuli ya kisanaa ya kuburudisha na kupitisha wakati bali zinaweza kuchangia katika maendeleo ya jamii. Kwa kutumia nyenzo kadhaa kama vile muziki, maadili na mambo mengine muhimu ya kijamii yataimarishwa. Miongoni mwa mambo haya ni masuala ya amani, kampeni dhidi ya ugonjwa hatari wa UKIMWI, ujirani mwema, malezi bora ya watoto, shughuli tofauti za kujiendeleza kiuchumi na kadhalika.

**5.4 Mapendekezo ya Utafiti**

Utafiti huu umeangazia lugha katika nyimbo (za Kiswahili) na uamilifu wake katika kuendeleza amani na maridhiano miognoni mwa wanajamii jambo ambalo ni mojawapo tu ya masuala chanya ambayo yanaweza kutekelezwa kuptia kwa nyimbo katika jamii. Tafiti za baadaye zinaweza zikaangazia namna lugha imetumiwa katika nyimbo zinazolenga masuala mengine katika jamii kama vile masuala ya kiuchumi kwa kutumia nyimbo zilizoimbwa kwa lugha mbambali kando na Kiswahili. Aidha, utafiti unaweza kuendeshwa kuhusu ujumi katika lugha kwenye muziki unaolenga masuala muhimu katika jamii yakiwemo ya kisiasa, kijamii na kiuchumi.

Kutokana na utafiti huu, inapendekezwa kuwa asasi mbalimbali nchini zinazoshughulikia masuala ya amani na maridhiano katika jamii hazina budi ila kujumuisha nyimbo katika kampeni zake. Hii ni kutokana na uwezo wa nyimbo kunata hisia za hadhira, hasa vijana, pamoja na kuwasilisha maudhui mazito kwa namna ya kuburudisha, ikilinganishwa na nyenzo kama vile warsha au makongamano.

Uwajibikaji wa wananchi pamoja na viongozi wa kisiasa katika matumizi ya lugha utasaidia katika kuhakikisha kuwa nchi ya Kenya ina amani na kuna maridhiano ya kudumu miongoni mwa wananchi.

**MAREJELEO**

Agovi, K. (1989). The Political Relevance of Ghanaian Highlife Songs Since 1975, *Research In African Literature*, 20, 2:194-201.

Akombo, D.O. (2006). *Music and healing across cultures*. Ames: Culicidae Press.

_________(2009). Music and Healing During Post-Election Violence in Kenya. *Voices: World Forum for Music Therapy,* Vol 9, No. 2.

Akuno, E.A. (1999). A Conceptual Framework For Research in Music Education within a Cultural Context. Paper presented at Cultural Week Seminar, Kenyatta University, Nairobi.

Alexander, N. (2003). The African Renaissance, African languages and African education with Special reference to South Africa. In H.E Wolf (ed.). *Tied Tongues*, 21-37. Munster: Lit.

Amuka, P. S. O. (2008). Fundamentalism and the Search for Human(e) Order. In: Idangasi, H. & H. Masumi (Eds.). *Daisaku Ikeda and Voices for Peace from AFRICA*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Barber, K. (1997). *West Africa Popular Theatre*. Bloomington: Ind.

Barry, P. (2008). Results of post election violence in Kenya. Retrived on 9th February 2013 from http://www.hollandhelpt.org.

Bateson, G. (1972). *Steps to an Ecology of Mind: Collected Essays in Anthropology. Psyciatry, Evolution and Epistemology.* Chicago: University of Chicago Press.

Bohlman, P. V. (2002). *Rupture, Resistance, and Revival in the Re-membering of German and American History.* Cambridge: Cambridge University Press.

Brandel, R. (1995). *The Music of Central Africa. An Ethnomusicology study*. London: Methuen.

Chachage, S. L. C. (2004). *'Ndani ya Bongo': Utandawazi wa migogoro ya utamaduni.* Dar es Salaam: TUKI

Chumbow, B.S (1987). Towards a Language Planning Model for Africa. *Journal of West African Languages* XVII/I: 15-22.

Duranti, A. (1997). *Linguistic Anthropology*. London: Cambridge University Press.

Economy Watch (2010). *Internal Displacement and Local Peacebuilding in Kenya: Challenges and Innovations.* Special Report 251. United States Institute of Peace.

Ekuam, E. D. (2006). Conficts, Confict Resolution and Peace Building: the Role of pastoral Women. In: Creighton, C. S., F. Yieke, J. Okely, L. Mareri & C. Wafula (eds.). *Gender Inequalities in Kenya*. UNESCO.

Elischer, S. (2008). Ethnic Coalitions of Convinience and Commitment: Political Parties and party systems in Kenya. *German Institute of Global and Areas Studies (GIGA) Working Papers* No.68

Fair, L. (1997). 'Music, Memory and Meaning: The Kiswahili Recordings of Siti Binti Saad.' *Paper read at the Annual Meeting of the African Studies Association.* Columbus: Ohio.

Fairclough, N. L. (1992). "Discourse and Text. Linguistic Intertextual Analysis within Discourse Analysis" In: *Discourse and Society*. 3:193-217.

__________ (1992). *Discourse and Social Change*. Cambridge: Polity Press.

__________ (1995). *Critical Discourse Analysis: The Critical Study of language*. London: Longman.

Finnegan, R. (1989). *The Hidden Musicians.* London: Cambridge University press.

Gabriel, A. & P. N. Juslin (2003). Emotional expression in music. In: Handbook of affective Sciences, (ed). R.J.Davidson, K.R. Scherer & H.H. Goldsmith, pp. 503- 34. Oxford University Press.

Gekau, K. (1993). 'The 1980's Background to the Popular Political Songs of the Early 1990's in Kenya.' In. *Media, Democratization and Identity*. Harare: Department of English, University of Zimbabwe.

Githinji, P. (2009*). Sheng, styleshifting and construction of multifaceted identities: Discursive practices in the negotiation of meaning*. Saarbruecken: VDM Verlag.

Githiora, C. (2002). Sheng: Peer Language, Swahili Dialect or Emerging Creole? *Journal of African Cultural Studies*, 15(2): 159-81.

Halliday, M. A. K. (1973). *Explorations in Language Study: Explorations in the Functions of Language.* Edward Arnold (publishers) Ltd.

Halliday, M.A.K. (1978). *Language as social semiotic. The social interpretation of language and meaning*. London: Edward Arnold.

Hofmeyr, I. (2004). 'Popular Literature in Africa: Post – Resistance Perspctives.' In. *Social Dynamics.* 30(2).

Hubley, J. *(1995*). *The AIDS Handbook. A guide to the understanding of AIDS and HIV.* London: MacMillan Education Ltd.

Hymes, D. (1974). *Language in Culture and Society*. New York: Harper & Row Inc.

Kandagor, M, K. Kiprono & P. Simotwo (2012). The Perspective of Youth in Peace Building, Healing and Reconciliation in Eldoret – Kenya. *International Journal of Humanities and Social Science* Vol. 2 No. 12 [Special issue -June 2012].

Kawoya, V., & Makokha, J. S. (2009). The Case for Kiswahili as a regional broadcasting language reform in East Africa. *The Journal of Pan African Studies*, 2(8), 11-35.

Kerlinger, F.N. and Lee, H.B. (2000). Foundation of behavioral research. New York: Holt and Rinehart.

Kiplang'at, J. & Lagat, C. (2009). *Kenya National Heritage: Music and Culture.* Paper presented at Fulbright Hays Group Projects Abroad program, Moi University, Nairobi Campus, 7th July 2009.

Kitiabi, K. M. (2012). *The Impact of Election (2007/2008) Violence on Kenya's Economy: Lessons Learned?* Election Dispatch No.6. ISSN 2012-2006

Kofie, N. N. (1994). *Contemporary African Music in World Perspective.* Accra: Ghana University Press.

KNCHR & KHRC. (2006). *Behaving Badly*: *Deception, Chauvinism and Waste during the Referendum Campaigns.* Nairobi: KNHR (Kenyan National Commission on Human Rights).

Konde-Lule, J. K. et al. *HIV Prevention in Rakai, Uganda*. Int. Conf. Aids (Germany) June 6-11, 1993; 9(2): 791 (Abstract No. PoD02-3440).

Kwaramba, A. D. (1997). Popular Music and Society: *The Language of Protest in Chimurenga Music: The Case of Thomas Mapumo in Zimbabwe*. IMK Report No. 24. University of Oslo.

Laing, D. (1996). The Economic Importance of Music in the European Union. London: University of Westminister Press.

Magnarella, P. (1994). Explaining Rwanda's 1994 Genocide in: A review of Mahmood Mamdani, *When Victims Become Killers: Colonialism, Navitism, and the Genocide in Rwanda*. Princeton, NJ: Princeton University Press, 2001. pp 364.

Makky, N. (2007). Song in the Anti-Apartheid and Reconciliation Movements in South Africa. Unpublished M.A Thesis, Ohio State University.

Mara, J. (2009). *Conflict Analysis of the 2007 Post Election Violence in Kenya.* Downloaded on 22-08-2012 from: www.internetworldstats.com

Massamba, D.P.B (2004). Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha. Dar es Salaam: TUKI

Masumi, O. H. (2008). The Role of Women in Peace-making: Daisaku Ikeda's Re-Intepretation of the Role of Women in the Twenty-first Century. In: Idangasi, H.

& H. Masumi (eds.). *Daisaku Ikeda and Voices for Peace from AFRICA*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mdee, S., A. Shafi, J. Kiango, & K. Njogu (eds.) (2009). *Kamusi Kamili Ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn.

Moto, F. (2004). Towards a study of the lexicon of sex and HIV/AIDS. *Nordic Journal of African Studies*. 13, 3: 343-362.

Momanyi, C. (2009). The effects of 'Sheng' in the teaching of Kiswahili in Kenyan Schools. *The Journal of Pan African Studies, vol.2, no.8.*

MOYAS. Retrieved from http//www.myd.govt.nz/ on 12th October 2012.

Mukhongo, L. L. (2009). The Kenyan media: Confronting state terror and atrocities. *Journal of Communication and Language Arts.* Special Issues or Media and Democracy, 3. 26-43.

Mutahi, K and W. Kabira (1998). *Gikuyu Oral Literature.* Nairobi: Heinemann.

Mutua, (2008). *Kenya's quest for democracy: taming the levithian*. London: Lynne Rienner Publishers.

Mwangi, M. (1992) When KBC says No Way! Daily Nation, 24th July 1992.

Nangulu, A. (2007). Ethnic Conflicts and Cattle Raids Between the pokot and their neighbours in Northwest Kenya, 1963-2000. In MAARIFA: *A Journal of Humanities and Social Sciences*, Vol. 2, No. 1, pp 226-235.

Negus, K. (1997). *Popular Music in Theory: An Introduction*. Hanover, NH: University Press of New England.

Ngugi, P. M. Y. (2000). *Nafasi ya Muziki Uliopendwa Katika Fasihi ya Kiswahili.* AAA 64: Swahili Forum VII. 145-152.

Njogu, K. (2012). Media and the Politics of Hate: The case of Vernacular Radio Stations In Kenya. In: Sandra, S, K, Wanjogu & A, Oluseye (eds.) *Language in African Performing and Visual Arts.* Yale (2012).

Ntabo, M. N., & Ogechi, N. O. (2009). *Siege politics: The underlying problem in Kenyan crisis.* Paper presented at the Moi University-Indiana University Purdue University Indianapolis Conference at Moi University, June 2009.

Ntarangwi, M. (2007). Music, Idenity and Swahili Networks of Knowledge. Ktk: K. Njogu & G. Oluoch-Olunya (Eds.) *Cultural production and social change In Kenya: Building bridges*. Nairobi: Twaweza Communications. Kur 19-23.

Nyairo, J. & J. Ogunde (2005). 'Popular Music, Popular Politics: Unbwogable and the Idioms of Freedom in Kenyan Popular Music', *African Affairs,* 104(415): 225-49.

Oduori, W. R. (2009). *Uchanganuzi Makinifu wa Lugha na Siasa Nchini Kenya: 2005*. PhD Thesis. Eldoret: Moi University.

Oettler, A. (2006). Guatemala in the 1980's: A Genocide Turned into Ethnocide. *German Institute of Global and Area Studies (GIGA) Working Papers No. 19.*

Ogechi, N. O. (2004). *Lexicalization in Sheng*. Alternation 11 (2): 325-342.

__________ (2005). Does Sheng have a Kiswahili grammar? *APAL Annual Publication in African Linguistics* 3: 3-25.

__________ (2011) "Double Edged Sword": The case of Swahili. In. *Themes in Language, Education and Development.* Nairobi: Nsemia.

Ogechi, N.O. & E. Bosire-Ogechi (2011). Identity and the New Communication Technologies: Evidence from Kenya. In: Wachanga D. (ed.) *Cultural Identity and New Communication Technologies. Political, Ethnic and Ideological Implications.*

Ogechi, N. O. (2012). The language situation and language harmonization in Kenya. In: Ogechi N. O, J. A. N. Ngala Oduor & P. Iribemwangi (eds.). *The Harmonization and Standardization of Kenyan Languages. Orthography and Other Aspects*. Cape Town: The Centre for Advanced Studies of African Societies (CASAS).

Ogosia, K. (2008). *Soldier turns to music to heal nation*. Retrieved on 18-07-2012 from http://allafrica.com.stories

Olwage, G. (2008). *Composing Apartheid. Music for and Against Appartheid.* Johannesburg: Withatersrand University Press.

Omondi, W.A. (1998). The Lyre in Luo Society: an Observation. African Musicology, 1(1), p. 41-44.

Partisau, D.S. (2006). *Sounds of Change and Reform: The Appropriation of Gospel Music and Dance in Political Discourses in Kenya*. In Journal of Religion and Popular Culture, Vol XIV, Fall 3.

Peace-net Kenya (2010). Retrived on 25th October 2012 from http//www.peacenetkenya.or.ke/

Pollard, A. B. (1999). *"Rhythms of Resistance." This is How We Flow: Rhythm in Black Cultures*. Ed. Angela M. N. Columbia, SC: University of South Carolina Press, 1999. 98-124.

Reagan, T.G. (1992). *Language function and language variation: analytic models for the South Africa Context.* South African Journal of African Languages Vol.12, Supplement1, pp.35-45.

Reddy, S. (2004). *Safe sex or safe love? Competing discourse within the context of HIV/AIDS*. Alternation, 11, 2: 440-453.

Saussure, F. (1916). *Course in General Linguistics*. New York: McGraw-Hill Book Company.

Sekella, M. (1995). Kiswahili katika Muziki wa Tanzania, katika *Kiswahili na Vyombo vya Habari*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Situma, K. E. & J. H. Ndeta (2010). *Nurturing Nationhood through Peace Media.* PeaceNet- Kenya.

Street, J. (1997). *Politics and Popular Culture.* Cambridge: Polity Press.

The Kenya Red Cross Society, 2012. Retrived on 25-10-2012 from htt://www.kenyaredcross.org/index-php?option=com-content&view=article&id=374.

The Kriegler Report on *The Post Election Violence in Kenya, 2008.*

The National Cohesion and Intergration Commission (2013). Retrived on 6th November 2012 from http//www.cohesion.or.ke/

The Waki Report on *The Post Election Violence in Kenya, 2008.*

Thompson, A. (2007). *The media and the Rwanda Genocide.* Kampala: Fountain Publishers.

Transparency International (2013). Retrived on 24th October 2012 from http//www.tikenya.org/

TUKI (1990). *Kamusi ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

TUKI. (2006). *English-Kiswahili Dictionary 2nd Edition*. Dar es Salaam: TUKI

Wanyama, N. M. (2006). Music Education: An Unexploited Goldmine in Kenya. *International Jounal of Community Music.* pp.1-10.

Wamitila, K.W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi.* Nairobi: Focus Publications Ltd.

Wekesa, W. P. (2002). "The Politics of Marginal Forms: Popular Music, Cultural Identity and Political Opposition in Kenya." *Paper Presented at CODESRIA General Assembly, December 2002*. Kampala.

Wells, A. & E. A. Hakanen (1991). The emotional uses of popular music by adolescents. *Journalism Quarterly* 68:445-54 [arPNJ].

Whiteley H. W. (1974). The Classification and Distribution of Kenya's African Languages. In: Whiteley H. W. (ed.) *Language in Kenya*. Nairobi: Oxford University Press.

Wodak, R. (1995). *Critical Linguistics and Critical Discourse Analysis*. In: Verschuerch, J. et al (eds.). Handbook of Pragmatics. Pp. 204-210. Amsterdam: Joun Benjamins.

# VIAMBATISHO

## KIBALI CHA UTAFITI



CONDITIONS

1. You must report to the District Commissioner and the District Education Officer of the area before embarking on your research. Failure to do that may lead to the cancellation of your permit.
2. Government Officers will not be interviewed with-out prior appointment.
3. No questionnaire will be used unless it has been approved.
4. Excavation, filming and collection of biological specimens are subject to further permission from the relevant Government Ministries.
5. You are required to submit at least two(2)/four(4) bound copies of your final report for Kenyans and non-Kenyans respectively.
6. The Government of Kenya reserves the right to modify the conditions of this permit including its cancellation without notice.

GPK6055t3mt10/2011

REPUBLIC OF KENYA

RESEARCH CLEARANCE PERMIT

(CONDITIONS—see back page)

PAGE 2

THIS IS TO CERTIFY THAT:
Prof./Dr./Mr./Mrs./Miss/Institution
[illegible] Ndemo Watara
of [illegible] University
P.O.Box [illegible], Eldoret
has been permitted to conduct research in

[illegible] Location
[illegible] District
[illegible] Province

on the topic: [illegible]
[illegible] (2003 - 2012)

for a period ending: 31st December, 2013.

PAGE 3

Research Permit No. NCST/RCD [illegible]
Date of issue [illegible] January, 2013
Fee received KSH. 1,000



Applicant's Signature

Secretary
National Council for Science & Technology

REPUBLIC OF KENYA

# NATIONAL COUNCIL FOR SCIENCE AND TECHNOLOGY

Telephone: 254-020-2213471, 2241349, 254-020-2673550
Mobile: 0713 788 787 , 0735 404 245
Fax: 254-020-2213215
When replying please quote
secretary@ncst.go.ke

P.O. Box 30623-00100
NAIROBI-KENYA
Website: www.ncst.go.ke

Our Ref:
**NCST/RCD/14/013/48**

Date:
**28th January, 2013**

Philip Ndemo Watara
Moi University
P.O.Box 3900-30100
Eldoret.

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

Following your application dated ***21st January, 2013*** for authority to carry out research on ***"Lugha ya amani na maridhiano katika muziki nchini Kenya (2008-2012)."*** I am pleased to inform you that you have been authorized to undertake research in **Kisii District** for a period ending **31st December, *2013*.**

You are advised to report to **the District Commissioner and the District Education Officer, Kisii District** before embarking on the research project.

On completion of the research, you are expected to submit **two hard copies and one soft copy in pdf** of the research report/thesis to our office.

DR M.K. RUGUTT, PhD, HSC.
DEPUTY COUNCIL SECRETARY

Copy to:

The District Commissioner
The District Education Officer
Kisii District.